

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 26 Juni, 2003

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (k.n.y. MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2003/2004.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 110

Kuanzishwa kwa Mkoa wa Manyara

MHE. DAMAS P. NAKEI (k.n.y. MHE. OMAR S. KWAANGW') aliuliza:-

Kwa kuwa kuanzishwa kwa Mkoa wa Manyara ni changamoto kwa maendeleo, kuboresha utawala na kuweka mipango endelevu katika kujenga Mkoa huo; je, Serikali imeweka mikakati gani yenye mipango na dira sahihi katika kuimarisha na kujenga Ofisi ya Mkoa, Hospitali ya Mkoa na kuimarisha huduma za jamii na za kiuchumi katika Mji wa Babati?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Manyara ulianzishwa baada ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kuamua kuugawa Mkoa wa Arusha. Shughuli za Serikali katika Mkoa huu mpya zilanza rasmi tarehe 1 Julai, 2002 na mnamo mwezi Agosti, 2002 Mheshimiwa Rais alimteua Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara yalipoanzishwa katika Mji wa Babati, miundombinu mingi haikuwa na hadhi ya Mkoa. Kwa mfano, hapakuwepo jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ikulu Ndogo na Hospitali ya Mkoa. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeshaweka mkakati wa kujenga jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kama ifuatavyo:-

- (i) Eneo lenye ukubwa wa hekta nne limepatikana ndani ya Mji wa Babati; na
- (ii) Uchoraji wa ramani ya jengo hilo umekamilika na makisio ya gharama za ujenzi wa jengo hilo ni Sh.600 milioni, makadirio haya yamekwishawasilishwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa unategemewa kuanza katika mwaka wa fedha 2003/2004. Kiasi cha Sh.300 milioni kimetengwa kwa madhumuni hayo. Ujenzi huu utakwenda pamoja na ujenzi wa nyumba za watumishi na Ikulu Ndogo. Kukamilika kwa kazi hii kutategemea kwa sehemu kubwa uwezo wa Serikali kupata fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, miundombinu yote inayohitajika itaendelea kujengwa kulingana na uwezo wa fedha Serikalini. Aidha, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali haina mpango wa kujenga jengo jipya la Hospitali ya Mkoa hivi sasa, badala yake Hospitali ya Wilaya iliyopo itaendelea kuimarishwa. Hata hivyo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imesharidhia kuifanya Hospitali ya Dareda kuwa ni Hospitali Teule na kwa mara ya kwanza tutakuwa na Hospitali ya aina hiyo katika ngazi ya Mkoa.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Babati ndio Makao Makuu ya Mkoa na hapa Dodoma ndio Makao Makuu ya Nchi na watu wa Manyara kila mara lazima wasafiri kuja hapa Dodoma kupitia Kondoa na barabara ya kutoka Babati - Kondoa - Dodoma ni mbaya, Serikali ina mpango gani kuiimarisha barabara hiyo ili watu wa Babati na Manyara waweze kusafiri vizuri?

SPIKA: Hilo ni swali jipya lilitwe kwa njia ya kawaida, Mheshimiwa Marmo nilikuona.

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuwa na miundombinu katika Makao Makuu ya Mkoa ni suala moja, lakini jambo tofauti kabisa ni namna ambavyo Makao Makuu haya yatafikiwa na Wilaya nyingine, je, mbona katika Bajeti ya mwaka huu hakuna ongezeko lolote lile linaloonekana kwamba miundombinu ya Mkoa huu mpya itaimarishwa?

SPIKA: Hata hilo ni swali jipya kwa kweli, maswali ya nyongeza yatokane na swali la msingi, Mheshimiwa Losurutia.

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Mheshimiwa Spika, kutokana na swali la msingi kama ulivyo sema, Babati ni Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara na kwa kawaida Makao Makuu ya Mkoa ndio yanafanya kuwa mji, je, ni lini Babati itageuzwa kuwa mji na Jimbo kamili?

SPIKA: Aah! Naona leo maswali ya nyongeza yanapoteza dira. Swali linalofuata, Mheshimiwa Esther Nyawazwa. (*Kicheko*)

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA aliuliza:-

Kwa kuwa Kata za Ng'hungumalwa, Nyamilama, Malya na Kituo cha Mwamashimba kwenye Wilaya ya Kwimba hazina gari la kuhudumia wagonjwa wala Kliniki kwa ajili ya kutoa huduma kwa watoto na akina mama wajawazito:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga Kliniki kwa ajili ya watoto na akina mama wa Kata hizo?
- (b) Je, ni lini Serikali itazipatia Kata hizo gari la kubeba wagonjwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kumbukumbu tulizonazo katika Ofisi yetu, hatuna Kata inayoitwa Mwamashimba isipokuwa ipo Kata ya Bupamwa ndani ya Tarafa ya Mwamashimba na kipo Kituo cha Afya ndani ya Tarafa hiyo kinaitwa Mwamashimba.

Mheshimiwa Spika, suala la lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga Kliniki kwa ajili ya akina mama wajawazito na watoto katika Kata za Ng'hungumalwa, Nyamilama, Malya na Bupamwa Wilayani Kwimba halipo, kwa kuwa Serikali ilikwishabaini umuhimu huo siku nyingi na kujenga Kliniki kama ifuatavyo:-

(i) Kata ya Hungumarwa yenye vijiji sita inazo Kliniki katika Zahanati tatu za vijiji hivyo. Aidha, Zahanati moja itakayokuwa na huduma ya Kliniki imeanza kujengwa mwezi Januari, 2003 katika Kijiji cha Kibitilwa kwa kushirikiana na TASAF na itakamilika mwezi Oktoba, 2003. Vile vile maandalizi ya kujenga Zahanati katika Kijiji cha Ng'hungumalwa kwa kushirikiana na Shirika la Dini la *Christ's For All People* yameanza;

(ii) Kata ya Nyamilana yenye vijiji vitano inazo Kliniki mbili katika Zahanati mbili katika vijiji nya Nyamilana na Mwankulwe;

(iii) Kata ya Malya yenye vijiji vinne inacho Kituo cha Afya cha Malya ambacho kina Kliniki. Aidha, tangu mwaka 2001 wananchi wa Kijiji cha Mwitambu wanaendelea kujenga Kliniki kwa kujitolea; na

(iv) Kata ya Bupamwa yenye vijiji vitano inacho Kituo cha Afya katika Kijiji cha Bupamwa ambacho kina Kiliniki pia. Aidha, ipo Zahanati ya Kijiji cha Kiliwi ambayo pia inayo huduma ya Kliniki.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa gari la wagonjwa haliko katika Kata hizi tu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, tatizo la gari ni kubwa kwa Wilaya nzima ya Kwimba, ambayo kwa sasa haina gari la aina hiyo. Hata hivyo, Halmashauri imeshaanza kufanya mazungumzo na wadau mbalimbali wakiwemo JICA, pamoja na Shirika lisilo la Kiserikali nichini Japan, Ilijulikanalo kama *Transport Aid*. Wahisani wameonyesha nia ya kutaka kusaidia. Vile vile katika kuboresha huduma za Rufaa, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imefanya mawasiliano na Shirika la CARE, ambalo limethabitisha kuwa litafunga *Radio Call* katika Hospitali ya Ngudu na Sumve, pamoja na Vituo vya Afya vya Mwamashimba na Malya. Hivyo kama gari litapatikana, kwa kweli itakuwa ni busara likae katika Makao Makuu ya Wilaya hiyo, yaani Ngudu, ili liweze kuhudumia Kata nyingine zote.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba, gari ni muhimu sana kwa maeneo aliyoyataja, je, Serikali haiwezi kutenga fedha kidogo kwa ajili ya kununua gari (*Second-hand*) ili kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema tatizo ni Ɂdha lakini nia ya Serikali ipo pale pale kuhakikisha kwamba, magari haya yanapatikana ili yaweze kuhudumia wananchi kwa namna inavyopendeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hili wazo la kujaribu kutenga fedha kidogo, ninaloweza kusema ni kwamba, pengine kwa sasa hatuwezi katika mazingira ambayo bajeti imeshakamilika, ni wazo ambalo linaweza kutazamwa kwa mwaka kesho tuone kama inawezekana.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza. Kwa kuwa kero ya magari katika Vituo vya Afya katika nchi yetu imekuwa ni sugu na Vituo vya Afya na Zahanati ziko mbali sana na Hospitali za Wilaya na kumekuwa na matatizo makubwa sana ya usafiri hasa kwa akina mama wajawazito kusafiri karibu kilometra 50, je, Serikali haioni sasa imefika wakati kuwa na Mpango Maalum kama ilivyofanya katika elimu kuwa na mpango wa MMEM ili lipatikane gari moja, moja tu katika kila Kituo cha Afya katika nchi nzima ili kuondoa tatizo hili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Spika, bado Serikali ina nia ya kujaribu kutazama mpango huu ambaeo unazungumzwa na Mheshimiwa Bendera. Hata kwa mwaka huu tulilitazama lakini kikwazo kimekuwa ni ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, tutaendelea kulifkiria na pengine bajeti ikiwa ahueni tunaweza kukamilisha wazo hilo ambalo na sisi tunalo.

Na. 112

Madhara ya Simu za Mkononi kwa Watumiaji

MHE. DAMAS P. NAKEI aliuliza:-

Kwa kuwa maendeleo ya teknolojia yameleta mafanikio makubwa kwa mwananchi lakini pia maendeleo hayo yameleta madhara makubwa kwenye sehemu nyingine yanapotumika vibaya kama ilivyo kwa teknolojia ya *nuclear* na kwa simu za mkononi (*Mobile Phones*):-

- (a) Je, ni madhara gani ya kiafya yanayotokana na simu za mkononi?
- (b) Kwa kuwa matumizi ya simu za mkononi yanakua kwa kasi kubwa, je, ni tahadhari gani zinatakiwa zichukuliwe kwa watumiaji wa simu hizo?
- (c) Je, kuna tofauti gani kati ya madhara yaletwayo na simu za kawaida (*Land Lines*) na zile za mikononi (*Cell Phones*) na kuna ukweli gani juu ya madhara ya simu za mkononi na jinsi ambavyo *safeguard E.M.W* zinazouzwa madukani zinavyoweza kusaidia?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, maendeleo ya teknolojia hasa mawasiliano yameleta mafanikio makubwa kwa wananchi. Aidha, maendeleo yoyote yapatikanayo kwa binadamu yanaweza kuleta madhara kwenye sehemu nyingine hasa yanapotumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na utafiti wa kisayansi uliokwishafanyika, hadi sasa utafiti umeonyesha kuwa hakuna madhara yoyote yatokanayo na matumizi ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utafiti huo, tumeshauriwa kuwa endapo watumiaji wataona ni vema kuchukua tahadhari, basi wapunguze muda wa mazungumzo, hasa kwa watoto au watumie vifaa vinavyowezesha simu kuwa mbali na kichwa au mwili.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Afya Duniani (*WHO*), likishirikiana na Shirika la Mawasiliano ya Simu Duniani (*ITU*), yanaendelea kufanya utafiti zaidi. Serikali kupitia Tume ya Mawasiliano na Tume ya Mionzi Tanzania na *TBS*, inafuatilia kwa karibu maendeleo ya utafiti huo na kuchukua hatua zifaazo pale hoja inapojitokeza kufanya hivyo.

Na. 113

Madhara ya Simu za Mkononi

MHE. ZAHOR J. KHAMIS aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Watanzania wengi hutumia huduma ya simu za mkononi na kwa kuwa inasemekana kuwa katika simu hizo ipo mionzi inayoathiri ubongo kwa watumiaji wa simu hizo:-

- (a) Je, ni tahadhari gani ambazo Serikali imechukua za kuwatahadharisha na kuwaelimisha wananchi wake?
- (b) Je, ni kwa muda gani madhara hayo huweza kujitokeza kwa mtumiaji wa simu hizo na ni kinga gani ya uhakika inaweza kumhusuru mwananchi kuepukana na madhara hayo?
- (c) Kwa kuwa katika maeneo ya mijini watumiaji wa simu hizo ni wengi, je, wananchi wengine amba si watumiaji wa simu hizo lakini wanaishi katika mazingira ambayo simu hizo hutumika, hawawezi kudhurika na mionzi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mbunge wa Chumbuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, simu za mkononi hazitoi mionzi inayoweza kuathiri ubongo wa binadamu. Utafiti uliofanywa chini ya usimamizi wa Shirika la Afya Duniani, umeonyesha kwamba, kiwango cha mionzi itokanayo na matumizi ya simu za mkononi ni cha chini sana ukilinganisha na masafa ya mionzi inayoweza kuharibu ubongo.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliokwishafanyika umeonyesha kwamba, nishati inayotoka katika simu ya mkononi ni ndogo sana ambayo ni kati ya 0.2 na 0.6 watts. Redio za mawasiliano aina ya *walkie-talkie* zinatoa nishati ya watts 10 au zaidi. Nishati hii humezwa na mwili na kutoa joto ambalo mwili hulidhibiti na kulitoa nje kwa process inayoitwa *Thermoregulatory*.

(b) Mheshimiwa Spika, kiwango hiki cha nishati kinachotokana na simu za mkononi ni kidogo mno kiasi cha kuweza kusababisha joto mwilini na hakuna utafiti uliokwishafanyika kuonyesha kuwa kuna madhara. Hata hivyo, Shirika la Afya duniani kama nilivyoleza hapo awali, linaendelea kufanya utafiti zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutoptaka na utafiti wa kisayansi uliokwishafanyika hadi sasa, utafiti hauonyesha umuhimu wa tahadhari au wa kuwa na kinga katika kutumia simu za mkononi. Hata hivyo, wenye simu wapunguze muda wa kuzungumza, wapunguze matumizi ya simu za mkononi kwa watoto na watumie vifaa vinavyowezesha simu kuwa mbali na kichwa au mwili kama tahadhari tu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Mawasiliano, imekwishachukua hatua za kuwaelimisha wananchi kupitia vyombo vyao habari na majarida yake yanayoitwa *The Regulator* kuwa hakuna madhara yoyote yanayoletwa na matumizi ya simu za mkononi. Katika maeneo ya mijini

wananchi wanaoishi katika mazingira ambayo simu za mkononi hutumika au karibu na mitambo ya simu (*Mobile Base Stations*), hawawezi kuathirika na mawimbi ya redio kwani *antenna* za mitambo hiyo huwekwa juu ya nyumba au mnara wenye urefu wa kati ya mita 15 hadi 50. Mawimbi ya redio yanayotoka kwenye *antenna* huwa ni membamba na huelekezwa juu kiasi kwamba, hayawezi kuleta madhara.

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuuliza swalii la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, vipo vifaa fulani ambavyo vinauzwa na kubandikwa katika simu na katika viplastiki hivyo kuna maelezo yanayoonyesha kwamba vinakinga mionzi ambayo inaharibu ubungo wa mtumiaji wa simu, je, Serikali inatuambia nini juu ya viplastiki hivyo, kuna ukweli wowote?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, vipo vifaa ambavyo unatakiwa uvipachike kwenye simu na uweke kwenye sikio, hivi ni vifaa ambavyo vinatolewa kama tahadhari. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hadi sasa katika tafiti zote zilizofanywa hakuna ilivoonyesha kwamba simu za mkononi zina madhara. Kwa kupitia Bunge lako Tukufu, napenda niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu siku hizi wengi mna-surf kwenye *internet* kama mna kalamu chukueni hii *website* mka-surf ili mjidhihirishie wenyewe kama tunayozungumza hapa yana ukweli, [ww.who.int/inffs.enfact19183.hotmail](http://www.who.int/inffs.enfact19183.hotmail). Baadhi ya *information* zinapatikana kutoka Shirika la Afya Ulimwenguni.

MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa amesema kwamba, nishati ndogo ndio inayotoka na haina madhara, je, kidogo kidogo mwishowe si huwa nydingi, je, haileti madhara?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swalii msingi, nishati ile ndogo inayotoka humezwa na mwili na kutoa joto, kwa hiyo, haileti madhara yoyote katika mwili.

Na. 114

Matumizi ya Sheria ya Uhamiaji

MHE. MOHAMED H. MISSANGA (k.n.y. MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO) aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Uhamiaji inautambua uraia wa Tanzania kwa kuzaliwa au kwa kuandikishwa na kwa kuwa wapo baadhi ya watu wamenyimwa uraia kwa kuwa ama wamezaliwa nje ya nchi au mmoja kati ya wazazi si Mtanzania:-

- (a) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kumkubali mtu kuwa raia wa Tanzania?
- (b) Je, ni mzazi yupi kati ya wazazi wa mwombaji anakubaliwa ili mtoto wao atambulike kisheria awe raia wa nchi hii?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Uraia wa Tanzania Na.6 ya mwaka 1995, pamoja na Kanuni zake za mwaka 1997, uraia wa Tanzania upo katika makundi matatu:-

- (i) Uraia wa kuzaliwa;
- (ii) Uraia wa kurithi; na
- (iii) Uraia wa Tajinisi (kuandikishwa).

Mheshimiwa Spika, kila kundi lina vigezo vyake kama ifuatavyo:-

(i) Uraia wa kuzaliwa inatakiwa awe amezaliwa nchini na wazazi wake wote wawili wawe ni Watanzania. Kama amezaliwa nchini lakini mmoja wa wazazi wake, baba au mama ni raia wa nje, mhusika atakuwa na uraia wa nchi mbili wa kuzaliwa Tanzania na wa kurithi kwa mmoja wa wazazi wake. Hivyo, mhusika atatakiwa kuukana uraia mmojawapo pindi akifikisha umri wa miaka 18;

(ii) Uraia wa kurithi anatakiwa awe amezaliwa nje ya nchi na wazazi wake wote wawili ni Watanzania. Awe amezaliwa nje ya nchi kwa baba raia wa Tanzania na mama raia wa nje au kinyume chake.

(iii) Uraia wa kuandikishwa, raia wa nje atapata uraia wa Tanzania wa kuandikishwa kwa kuomba kwa Waziri mwenye dhamana ya uraia na pia ombi lake liwe limekidhi masharti yote ya kisheria ambayo ni:-

- Awe amekaa nchini mfululizo kwa kipindi kisichopungua miaka 10;
- Awe ni mwenye manufaa kwa Taifa kiuchumi, kisayansi, kiteknolojia, maendeleo ya jamii au utamaduni;
- Awe na uwezo wa kuongea kwa ufasaha lugha ya Kiswahili au ya Kingereza au lugha zote mbili;
- Awe ni mwenye tabia njema na alipojitangaza kwenye gazeti hakutolewa pingamizi na mtu yoyote; na
- Baada ya kupata uraia aonyeshe utii kwa nchi na nia ya kuishi nchini muda wote.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Na.6 ya mwaka 1995 na Kanuni zake za mwaka 1997, wazazi wote wawili yaani baba na mama wanakubalika kisheria kuwarithisha uraia watoto wao.

Mheshimiwa Spika, naomba pia ikumbukwe kuwa raia wa nje anapoomba uraia wa Tanzania, siyo haki yake kupewa uraia huo, hivyo hana haki ya kudai au kulazimisha apewe uraia wetu, kama ambavyo kwa Watanzania hatuna haki ya kudai au kulazimisha tupewe uraia wa nchi nyingine.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

- (i) Kwa kuwa Tanzania tumerithi sheria nyingi za Kikoloni hasa za Waingereza waliotutawala; je, Sheria hii ya Uhamiaji inalingana na Sheria za Uingereza au na Sheria za nchi za *Commonwealth*?
- (ii) Kwa kuwa nchi nyingine duniani mgeni anapooa au kuolewa na raia wa nchi husika basi hufuata utaratibu wa kupewa uraia, je, Tanzania hatuvezi kuwa na utaratibu kama huo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza, Sheria zetu za Uhamiaji kwa kiasi fulani zinalingana na sheria za nchi nyingine za *Commonwealth*, lakini hazilingani kwa asilimia mia kwa mia. Kuna baadhi ya nchi za *Commonwealth* zinakubali mtu awe na uraia wa nchi mbili hata tatu, lakini sisi sheria yetu inataka uwe Mtanzania tu. Hiyo ni moja ya tofauti yetu na baadhi ya nchi za *Commonwealth*.

Mheshimiwa Spika, pili, kama mgeni akioa au akiolewa na Mtanzania, sheria yetu inasema nini? Sheria yetu inasema kwamba, kama Mtanzania mwanaume akioa mwanamke wa kigeni yule mwanamke ataomba uraia lakini taratibu zake zinakuwa nyepesi, nyepesi, mwanamke akiolewa na mwanaume mgeni huyu mgeni naye ataomba uraia lakini taratibu zake hazitakuwa nyepesi, nyepesi.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa kielelezo cha wazi kabisa cha kujulisha uraia wa mtu katika nchi ni kumiliki *Passport* na kwa kuwa katika nchi yetu kupata *Passport* ni kitu kigumu sana, je, ni lini Wizara yake itarahisisha masharti ya kupata *Passport* ili Watanzania wengi waweze kumiliki hati hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kupata *Passport* hakuna masharti magumu kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu unajaza fomu huko huko Mkoani uliko na fomu zipo wala haziuzwi, ukishakamilisha kujaza na masharti yote yaliyomo zinaletwa Uhamaaji Makao Makuu na *Passport* inatolewa. Kwa hiyo, kwa kweli masharti sio magumu kama Mheshimiwa Mbunge anavyotaka ielewewe.

SPIKA: Kanuni zinasema maswali ya nyongeza yasizidi matatu kwa hiyo bado moja tu, Mheshimiwa Janet Kahama. (*Kicheko*)

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa katika nchi nyingine mama anapojifungua ndani ya ndege au akiwa katika anga ya nchi ile yule mtoto hutambulika kuwa ni mtoto wa nchi ile, je, sisi Tanzania mtoto anapozaliwa katika anga ya Tanzania na katika chombo cha Tanzania anakuwa raia wa Tanzania? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama mtoto atazaliwa ndani ya ndege au treni na ndege au treni hiyo ikiwa ndani ya nchi yetu, atakuwa raia iwapo tu kama wazazi wake wote wawili ni Watanzania na sio vinginevyo.

Na. 115

Sheria Zilizopitwa na Wakati Mambo ya Ndani

MHE. ALI MACHANO MUSSA aliuliza:-

Kwa kuwa katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hasa kwenye Jeshi la Polisi kuna sheria ambazo zimepitwa na wakati na kwa kuwa sheria hizo zinawafanya baadhi ya wafanyakazi kutopata maslahi kama wafanyakazi wa Idara na Mashirika mengine na matokeo yake maaskari hushawishika kufanya vitendo vilivyo kinyume na maadili ya kazi zao:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kuzibadili baadhi ya sheria ambazo zimepitwa na wakati na kuweka sheria zinazokidhi hali ya sasa?
- (b) Je, Serikali tangu tupate uhuru wa nchi yetu, ni mara ngapi imewahi kubadili sheria zinazoweza kuwasaidia askari kufanya kazi zao kwa ufanisi na kupata maisha mazuri?
- (c) Je, kama mawazo hayo ni sahihi, Serikali inatoa tamko gani ili kuwaambia Askari Polisi na raia ambao wanaathirika na hali hiyo kwa kuwapa muda ambao sheria hizo zitabdalishwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mbunge wa Tumbatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge kwamba, sheria zinazotumiwa na Jeshi la Polisi zimepitwa na wakati na hivyo kuwafanya askari kukosa maslahi kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine katika Idara zingine za Serikali na hivyo hushawishika kufanya vitendo vilivyo kinyume na maadili ya kazi zao. Ukweli ni kwamba, Askari Polisi kama ilivyo kwa watumishi wengine Serikalini, wanalipwa maslahi ambayo kwa kiasi fulani hayalingani na hali halisi ya maisha.

Tatizo hili halitokani na utumiaji wa sheria zilizopitwa na wakati bali chimbuko lake ni uwezo mdogo wa uchumi wa nchi wa kutoa maslahi mazuri zaidi.

Aidha, sheria zinazohusu Jeshi la Polisi, kama zilivyo sheria zingine nchini, Serikali huzirekebisha kila inapokuwepo haja ya kubadili ili kwenda na wakati au kutunga sheria mpya na kufuta iliyokuwepo. Yote haya hufanyika kupitia Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, sheria ambazo zinahusu utendaji na maslahi kwa Jeshi la Polisi, ambazo zimekuwa zikitumiwa tangu Tanzania ipate uhuru ni tatu, yaani Sheria ya Pensheni (*The Pensions Ordinance, Cap. 371*), Sheria ya Jeshi la Polisi (*The Police Force Ordinance Cap.322*) na Sheria ya Fidia (*Workmen's Compensation Ordinance, Cap. 263*). Hadi kufikia mwaka 1993 sheria hizo ziliwu zimefanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) *Pension Ordinance, Cap. 371*, ilifanyiwa marekebisho mara 17 na sasa imefutwa na Sheria Na. 2 ya 1999 (*Public Service Retirement Benefits Act*);

(ii) *Police Force Ordinance, Cap. 322*, imefanyiwa marekebisho mara 11; na

(iii) *Workmen's Compensation Ordinance Cap. 263*, imefanyiwa marekebisho mara 9.

Marekebisho yote haya yamefanywa ili kuziwezesha sheria hizo kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, mbali na sheria hizo za zamani ambazo zimekuwa zikifanyiwa marekebisho ya mara kwa mara, Serikali imeweza kutunga sheria zingine mpya ambazo ni Sheria ya Tume ya Polisi na Magereza (*The Police Force and Prison Service Commission Act No. 8 of 1991*), ambayo katika kifungu Na. 21 inazungumzia haki ya Askari Polisi kulipwa fidia anapoumia au kufariki akiwa kazini. Aidha, chini ya kifungu Na. 22 cha Sheria hii, zimetungwa kanuni ambazo katika sehemu ya 7 zinaelezea kuhusu posho mbalimbali ambazo Askari Polisi anapaswa kulipwa. Katika ujumla wake sheria zote hizo zinaonyesha jinsi Serikali inavyojali maslahi ya Askari Polisi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuzifanyia marekebisho sheria mbalimbali kila itakapoona kuwa upo ulazima wa kufanya hivyo kwa maslahi ya Askari Polisi na Taifa kwa jumla.

MHE. ALI MACHANO MUSSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba, wamebadilisha baadhi ya Sheria na kwa kuwa nina uhakika Waziri mpya wa Wizara hiyo kuna tegemeo kwamba atatembelea Mikoa yote yenye Vituo vya Polisi. Je, atakuwa tayari kuwaeleza Maaskari Polisi kwenye vituo hivyo kuwa wana mabadiliko na watajibowi majibu kama hayo aliyonijibu mimi hapa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Waziri wetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani atatembelea Mikoa yote, ni wajibu wake na ameshaanza kutembelea. Ni juzi tu alikuwa katika Mkoa wa Singida na katika ziara hizo anakutana na askari na katika kuhimiza shughuli mbalimbali za Jeshi la Polisi vile vile ataeleza na mabadiliko haya ambayo nimeyataja sasa hivi. (*Makofi*)

Na. 116

Serikali kulipia Wanafunzi Dola 10 za Kimarekani

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2001 Serikali ilifuta shilingi 2,000/= za UPE zilizokuwa zinalipwa na wazazi kwa kila mwanafunzi kwa lengo la kuwapa unafuu wazazi; na kwa kuwa Serikali iliahidi kuwapa unafuu wazazi; na kwa kuwa Serikali iliahidi kwenye bajeti yake kuwa italipa dola 10 za Kimarekani kwa kila kichwa cha mtoto:-

- (a) Je, Serikali imeshatoa dola ngapi kwa kila kichwa cha mtoto kwa kila mwaka yaani 2001, 2002 na 2003 na imetoa fedha hizo kwa awamu ngapi?
- (b) Je, Wilaya ya Karatu imepelekewa fedha kiasi gani kwa kila kichwa cha mtoto kwa miaka ya 2001, 2002 na 2003 na kwa awamu ngapi?
- (c) Kama fedha hizo hazikupelekwa kama ilivyoahidiwa, je, ni matatizo gani ya msingi yaliyoifanya Serikali ishindwe kutimiza ahadi yake?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2001/2002, Serikali kwa kushirikina na Wahisani ilitoa ruzuku ya uendeshaji jumla ya shilingi 30,264,846,830/= ambazo ni sawa na shilingi 5,084.23 au Dola 5.65 za Kimarekani kwa mwanafunzi. Mwaka wa pili 2002/2003 hadi Juni, 2003 zimetolewa jumla ya shilingi 34,644,777,898.20 ambazo ni sawa na shilingi 5,823.38 karibu dola 6.47 kwa kila mwanafunzi. Utumaji wa fedha hizo kwenye Halmashauri ulitegemea lini fedha zilipatikana kutohana na vyanzo tofauti vya fedha hizo. Kwa upande wa fedha za Serikali, fedha zilitumwa kila robo ya mwaka, yaani Julai - Septemba, Oktoba - Desemba, Januari - Machi na Aprili - Juni kwa mwaka wa kwanza na kwa mwaka wa pili. Fedha hizo zilitumiwa kwa kadri zilivyopatikana. Hata hivyo, Serikali tayari imekubaliana na wahisani wa mpango huu kutoa fedha zao kwa utaratibu wa robo mwaka na yako matumaini ya ongezeko la uhisani kutuwezesha kufikia lengo la Dola 10 kabla ya mwisho wa mwaka huu.
- (b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu katika mwaka wa kwanza 2001/2002, ilipelekewa fedha za ruzuku ya uendeshaji jumla ya shilingi 196,417,544/= ambazo ni sawa na shilingi 4,503/= sawa na dola tano za Kimarekani kwa mwanafunzi. Aidha, katika mwaka wa pili 2002/2003, Halmashauri hiyo imekwishatumiwa jumla ya shilingi 273,347,028/= ambazo ni sawa na shilingi 6,266.30 au dola 6.47 kwa mwanafunzi. Kati ya hizo jumla ya shilingi 13,150,598.68 ni ruzuku kwa ajili ya kugharamia usimamizi na ufuatiliaji katika ngazi ya Wilaya, Kata na mafunzo ya Kamati za Shule na ukaguzi wa shule katika Wilaya hiyo. Fedha zote hutumwa kwa Halmashauri zote kwa wakati mmoja.
- (c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba fedha za ruzuku ya uendeshaji hazikupatikana kufikia kile kiwango cha dola kumi zote kama ilivytarajiwa katika bajeti za miaka miwili ya mwanzo. Sababu kubwa ya msingi ni kwamba, fedha kutoka kwa wahisani hazikupatikana zote kwa wakati uliotakiwa kama ilivytarajiwa. Lakini zilizopatikana zilitosheleza mahitaji ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa maana ya daftari, chaki, kalamu, peni na vifaa vya michezo, sawa na shilingi 1,800/= kwa mwanafunzi kwa mwaka na pia za vitabu vya kiada na ziada ambazo ni sawa na shilingi 3,600/= kwa mwaka kwa mwanafunzi. Jumla shilingi 5,400 kwa mwaka. Hata hivyo, Serikali na wahisani tunaendelea kujitahidi kufikia lengo la Dola kumi kwa mwanafunzi katika mwaka huu wa shule.

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kina. Pamoja na hayo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Walimu Wakuu ndiyo wanaotekeleza hasa kazi zilizotakiwa zitekelezwe na fedha hizo na kwa kuwa fedha hizo zinapopelekwa mara nyingi walimu hao huwa hawapati taarifa zilizoainisha. Je, ni vizuri sasa katika taarifa inayotolewa na Serikali ikaainisha ni zip i zinakwenda moja kwa moja kwa Kamati za Shule ili hata zikichelewesha Walimu Wakuu waweze kuzifuatilia? Kwa sababu sasa hivi taarifa zilizopo ni kwamba Walimu Wakuu katika sehemu zote wanalamika kwamba fedha hizo hazikufikishwa lakini inawezekana zimefika Wilayani lakini kule kunakotakiwa hazikufika.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Waziri na takwimu alizozitoa pia zinaonyesha kwamba kwa miaka mitatu kiasi kilichotolewa ni kama Dola kumi badala ya kufika Dola thelathini kwa miaka mitatu. Sasa katika hali hiyo, je, kwa kuwa hizo fedha ni muhimu Waziri anasemaje

kuhusu kutenga fedha maalum kutoka kwenye bajeti yetu ya ndani kwa elimu ndiyo tegemeo na uhai wa Taifa ili hata za nje zikikosekana tusiweze kuathirika kwa kiwango chochote kile? (*Makofî*)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika baadhi ya Halmashauri hawapeleki taarifa kwa Kamati za Shule na kwa Walimu Wakuu kueleza fedha ambazo zimekwishatumwa. Kwa hiyo, hii ni kasoro ambayo napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Elimu kwamba, kila wanapopokea fedha inabidi watoe *Circular* za kuwataarifu Walimu Wakuu na Kamati za Shule kwamba fedha zilizopokelewa ni kiasi hiki kwa kila mwanafunzi ili kila shule na Kamati yake wajue fedha zile zilizopatikana. Nadhani huu utakuwa ni utaratibu ulio mzuri na sahihi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalî la pili kwamba kiasi hakikutosha na kwamba pengine tungezipanga zote kwa bajeti ya ndani. Napenda nikumbushe kwamba, mpango huu wa MMEM uliandaliwa na ikafahamika kwamba fedha setu za bajeti ya ndani hazitatosheleza mahitaji ya mpango wote na ndiyo maana sehemu ya fedha zinatokana na misaada, pamoja na mkopo kutoka Benki ya Dunia. Lakini kwa kadri hatua zinavyochukuliwa chini ya Uongozi wa Serikali ya CCM, tumeona uchumi wetu sasa unakua kwa asilimia 6.2. Tukiendelea kufanya hivi tutaongeza uwezo wa ndani wa kuweza kubeba bajeti nzima ya elimu ambayo tunaipanua hivi sasa. (*Makofî*)

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalî dogo la nyongeza. Katika kujibû swalî la msingi Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba, Serikali imekuwa ikitoa fedha pungufu ya zile ilizokusudia kutokana na kwamba wahisani wamekuwa wakiwapatia fedha kidogo namna hiyo. Sasa kwa kuwa lengo la fedha hizo lilikuwa ni kuwasaidia kuwapa nafuu wazazi na kwa kuwa shule zilikwishaweka mipango, je, Serikali itakuwa tayari kulipa hiyo tofauti ya fedha ambazo imekuwa haizipeleki pindi wahisani watakapeweza kuwa wametupatia fedha hizo? (*Makofî*)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, ni kweli nimekiri kwamba, kiwango hakikufikiwa, lakini napenda nichukue nafasi hii kulikumbusha Bunge kwamba, kabla ya mpango huu kuanza, bajeti ya Serikali ilikuwa inatoa shilingi 900/= kwa mwanafunzi. Kwa hiyo, hata kama hatukufikia, lakini tumetoka shilingi 900/= tumekwenda juu mara tano mpaka kufikia shilingi 5,000/=.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda nikumbushe kwamba, niliwahi kutoa kauli pengine nitarudia tena kwamba, niliwahi kutoa kauli hapa Bungeni ya kutoa ufanuzi juu ya mafungu ya mpango huu. Mle ndani ya kauli nilisema kwamba, katika zile Dola kumi mgawanyo wake, vifaa vya kufundishia au kujifunzia shuleni kwa maana ya daftari, chaki, kalamu, peni na vifaa vya michezo ni dola mbili, sawa na shilingi 1,800/= kwa mwanafunzi. Vifaa na mambo ya utawala nikasema ni dola moja sawa na shilingi 900/= kwa mwanafunzi. Majaribio ya mitihani ya shule na Kata dola moja sawa na shilingi 900/= kwa mwanafunzi. Jumla ya hizi nilizozitaja ni dola nne na nikasema hizi ndiyo zinatakiwa ziende moja kwa moja zikapangiwe matumizi pale shuleni. Halafu nikasema kuagiza vitabu vya kiada na ziada yaani vitabu vinavyohitajika shuleni kwa maana *text books* sawa na dola nne kwa mwanafunzi, tukasema hizi zinaweza zikabakia Wilayani ili Wilaya ipate majumuisho ya mahitaji. Lakini pia inatakiwa Halmashauri ziziambie shule kwamba fedha zimekuja dola fulani kwa ajili ya *text books* kwa mwanafunzi. Halafu nikasema matunzo ya majengo ni dola mbili. Jumla ukimjumlisha ni dola kumi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, huu ndiyo mgawanyo wa mafungu haya. Sasa ile sehemu ya kwanza ya kwenda shuleni katika miaka miwili iliopita zimeletwa kwa ukamilifu, upungufu kidogo unaweza ukawa katika hizi fedha za matunzo. Kwa hiyo, mimi naamini kwamba, kama fedha hizi zimepangwi vizuri, hatutakiwi tuwe na upungufu wa vifaa vile muhimu kama vile madaftari na chaki, vinavyowezesha walimu waweze kufundisha vizuri na wanafunzi kujifunza vizuri. (*Makofî*)

Kwa kuwa Serikali imedhamiria kupanua na kuboresha elimu nchini ili kuhimili ushindani wa utandawazi na mazingira ya karne ya 21 ya maendeleo ya sayansi na teknolojia; na kwa kuwa kulingana na hali hiyo utaji wa elimu unalazimu matumizi ya kompyuta kuanzia shule za awali na kuendelea; na kwa kuwa ili kukamilisha azma hiyo zipo raslimali za kutosha zinazotokana na msamaha wa madeni, lakini pia kwa kuzingatia hatua za mpito kabla ya kupatikana kwa umeme wa *Grid* ya Taifa ili kuendelea na utaratibu wa utoaji wa elimu hiyo kwenye baadhi ya shule ambazo hazina umeme:

Je, Serikali itakuwa tayari kuzipatia umeme wa *Generator* sekondari za Mweli na Dakama zilizoko Jimboni Kahama na haziko kwenye maeneo ya njia ya umeme wa *Grid* ya Taifa?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, karne hii ni ya sayansi na teknolojia na kwamba ni muhimu kutilia mkazo mafunzo ya kompyuta kwenye shule zetu kuanzia shule za msingi. Matumizi ya kompyuta yanalaizimu kuwa na umeme. Kuna shule nyingi za sekondari ambazo wananchi wamejenga maeneo ambayo bado hayajapata huduma ya umeme wa *Grid* ya Taifa. Kwa kuwa mfumuko wa shule zilizoanzishwa kwa nguvu za wananchi ambazo hazina umeme ni mkubwa na kwa kuwa umeme wa jenereta ni ghali sana, hasa ukizingatia bei ya mafuta na vipuli vya mashine, uwezo wa Serikali kifedha wa kuzipatia jenereta shule zote zisizokuwa na umeme wa *Grid* ni mdogo. Kwa hiyo, inashauriwa kuwa kule ambako umeme wa *Grid* ya Taifa haujafika waendelee kutumia karabai kwa ajili ya mwanga na endapo itaamuliwa kuanzisha mafunzo ya kompyuta, itabidi suala la umeme kwa ajili ya kompyuta lizingatiwe wakati wa kuamua hivyo kwa kuangalia uwezekano wa vyanzo vingine vya umeme kama vile nguvu ya mwanga wa sua (*Solar Energy*), kwa ajili ya matumizi ya kompyuta.

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini imeonekana wazi kwamba Waziri anaewela kwamba umeme ni moja ya vitu muhimu katika shule za sekondari. Sasa katika mpango wake ndani ya Wizara na Serikali ili kuendana na juhudii na nguvu za wananchi kwa sababu elimu wote tunataka tuiendeleze na tuiinue, ina mpango gani madhubuti wa kuungana na wananchi kuhusiana na suala zima la umeme katika shule za sekondari nchini? (*Makofii*)

SPIKA: Swalii linahusu umeme ngoja lijibiwe na Waziri mhusika Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Elimu katika maeneo ambayo hayana umeme wa *Grid* kuna vyanzo vingine vya kupata nishati hii ya umeme. Kwa kuwa Kahama ni moja ya maeneo ya wafugaji na maeneo kama Kahama kuna malighafi nzuri sana ambayo inaweza kutumika katika uzalishaji wa umeme, nayo ni *biogas*. Tunafahamu wote kwamba, kuna ng'ombe wa kutosha na ndugu zangu pia wa Kisukuma kule ni wengi, kwa hiyo, mchanganyiko wa malighafi hii kutoka kwa ng'ombe na binadamu inaweza ikasaidia katika kuanzisha umeme wa *biogas* ambayo ni nafuu katika maeneo ambayo umeme wa *Grid* ya Taifa haupo. (*Kicheko/Makofii*)

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza dogo la nyongeza. Kwa kuwa elimu ya msingi ni kitu cha msingi katika kuweka utaratibu wa kuwapeleka wanafunzi katika viwango vingine vya elimu na kwa kuwa Waziri wa Elimu hawezitutaja hata nchi moja hapa duniani iliyoendelea kwa kuendeleza tu elimu ya msingi. Sasa kwa kuwa jenereta moja inanunuliwa kwenye shilingi milioni tatu na shule ambazo hazina umeme ni kama mia tatu, hivi Serikali itapata hasara gani kwa kutenga shilingi milioni mia tisa tu kununua jenereta katika shule zote hizo za sekondari? (*Makofii*)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema kwamba elimu ya msingi ni muhimu na pia elimu ya sekondari ni muhimu lakini pia lazima tufahamu kwamba, tuna shule za msingi karibu 12,000 katika nchi yetu. Kwa hiyo, unapozungumzia kupeleka umeme kwa kila shule ya msingi kila unapozifanya hesabu utumie jumla hiyo ya shule, kama sikumsikia vizuri hakusema

sekondari, ni muhimu pia kujua tuna shule ngapi za sekondari. Sasa hivi tuna sekondari 1,082 na zilizo na umeme hazifikii nusu kutokana na hizi nyingi zilizojengwa na wananchi. Kwa hiyo, mahitaji ya jenereta kwa shule zote hizo ni makubwa sana. Kwa hiyo, napenda ushauri nilioutoa mimi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye namshukuru sana, uzingatiwe kwa sababu unaweza kusaidia.

Lakini Mheshimiwa Spika, mimi nimeziona shule za sekondari katika ujana wangu, utoto wangu, utoto wangu wakati nasoma nilisoma *Malangali Primary School, Malangali Secondary School* kulikuwa hakuna jenereta. Lakini palikuwa na karabai za kutosha na bajeti ya kutosha kuhakikisha yanapatikana mafuta na watu wengi wamesoma pale, wamepata elimu nzuri tu na wengine tunao katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Na. 118

Matengenezo ya Barabara Zilizoharibiwa Wakati wa *El-Nino*

MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA (k.n.y. MHE. KILONTSI M.M. MPOROGOMYI) aliuliza:-

Kwa kuwa barabara nyingi ziliharibika wakati wa mvua za *El-Nino* na madaraja mengi yaliyovunjika kama vile kutoka Nyaruboza hadi Rusaba, Muganza hadi Mwanga, Muyama hadi Kilelema, Janda hadi Mubanga na barabara iendayo Nyankoronko toka kwenye barabara kuu itokayo Kwitanga kwenda Buhigwe.

Je, ni lini barabara hizo zitatengenezwa ili kuwaondolea kero wananchi wa Wilaya ya Kasulu, ambao hupenda kutembelea sehemu hizo ambazo zinazalisha mazao mengi lakini wanashindwa kusafirisha mazao yao kwa sababu ya ukosefu wa barabara?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mvua za *El-Nino* zilizotokea mwaka 1997/98 ziliharibu miundombinu mingi ikiwa ni pamoja na madaraja, barabara, reli na kadhalika hivyo kusababisha kero kubwa kwa wananchi wote nchini. Mara tu baada ya mvua hizo, Wizara yangu kwa kulitambua tatizo hili, iliandaa mikakati ya matengenezo ya barabara zilizoathirika na mvua hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Kigoma mikakati hii ilihuisha matengenezo ya barabara ya Kwitanga hadi Buhigwe yenye urefu wa kilomita 39 ilio kwenye barabara ya Kisili - Buhigwe ambayo ina urefu wa kilomita 60, ambayo imetengenezwa hadi kiwango cha changarawe chini ya mpango wa matengenezo ya dharura ya barabara za Mkoa. Matengenezo hayo yaligharamiwa na fedha za Benki ya Dunia na yalianza tarehe 10 Februari, 2001 na kukamilika 10 Agosti, 2001. Matengenezo haya yalihuisha pia barabara za Kasulu - Manyovu ambapo kilomita 4.8 zilitengenezwa na barabara ya Kakonko - Nyaronga ambapo kilomita 8.15 za barabara zilitengenezwa. Matengenezo ya barabara hizi yaligharimu jumla ya shilingi milioni 529.5.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matengenezo hayo, barabara ya Kisili - Buhigwe ni mojawapo ya barabara za Mkoa ambazo zimepangwa kufanyiwa matengenezo chini ya mpango wa kuondoa umaskini (*HIPC*). Mpango huu unafadiliwa na Mfuko wa Fedha wa *OPEC (OPEC Fund)*, ambapo kilomita 20 za barabara hii zitatengenezwa kwa kiwango cha changarawe. Mawasiliano yanaendelea kufanyika kati ya Serikali na mfadhilli kwa lengo la kupata ukubali wake. Aidha, barabara hizi zitaendelea kupata matengenezo ya kawaida chini ya Wizara yangu kuitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*).

Mheshimiwa Spika, barabara kutoka Nyaruyoba hadi Rusaba, Muganza hadi Mwanza, Muyama hadi Kilelema, Janda hadi Mbunya na barabara iendayo Nyankoronko zinahudumiwa na Halmashauri ya

Wilaya ya Kasulu. Kwa kutumia Mfuko wa Barabara (*Road Fund*), Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu katika mwaka wa fedha 1999/2000 na 2000/2001, ilikamilisha ujenzi wa madaraja mawili kwenye barabara iendayo Nyakakonko kwa gharama ya shilingi milioni 22. Aidha, katika mwaka huo huo wa fedha 2001/2002, kiasi cha shilingi milioni 9.2 kilitumika kugharamia matengenezo ya madaraja kwenye barabara kama ifuatavyo: Daraja moja la mbao lilitengenezwa kwenye barabara ya Mganza - Mwanga kwa shilingi 150,000/=, madaraja mawili ya zege yalijengwa kwenye barabara ya Bihigwe - Nyankoronko kwa shilingi milioni tisa. Katika mwaka wa fedha 2002/2003, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu imeendelea kufanya matengenezo ya barabara ya Buhigwe hadi Nyankoronko kwa gharama ya shilingi milioni 8.24. Kazi zinazoendelea kufanyika ni kuchonga barabara urefu wa kilomita saba na kujenga makalvati matatu. Aidha, Halmashauri hiyo itaendelea kuzifanyia matengenezo barabara katika Wilaya hiyo kadri fedha za Mfuko wa Barabara zitakavyoruhusu.

MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi ambayo yanaonyesha kwamba tangu 1997 hizo barabara hazijawa katika hali nzuri na hizi barabara zilizolezwa ndiyo zinazounganisha hizo barabara za Mwandiga -Manyovu kwa sababu ndiyo barabara kuu. Sasa je, juhudhi hizo zitakamilika lini ili wananchi waweze kupata mawasiliano ambayo yamekatika kwa muda mrefu? Hapo sasa.

SPIKA: Hapo sasa Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba, tunajitahidi kuzungumza na wafadhili wa *OPEC* ili tupate fedha zinazohitajika kutengeneza barabara hii na mazungumzo yanaendelea, pale yatakapokamilika ndiyo mazao ya juhudhi hii yataonekana na barabara hii itatengenezwa.

Na. 119

Fedha za Matengenezo ya Barabara

MHE. JENISTA J. MHAGAMA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hutenga fedha za matengenezo ya barabara kila robo mwaka kwa kila Mkoa na Wilaya hapa nchini na kwa kuwa fedha hizo zinatakiwa zihudumie barabara zote katika eneo husika:-

(a) Je, inakuwaje barabara nyingine zichukue miaka kadhaa bila ya kufanyiwa matengenezo?

(b) Je, Serikali inahakiki vipi katika kuona kama fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara zinatumika kama inavyopangwa?

(c) Je, inapobainika kuwa barabara haifanyiwi matengenezo kwa kipindi kirefu sana, Serikali inachukua hatua gani za kinidhamu kwa mhusika?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania ina eneo la kilomita za mraba zipatazo 945,225 na ina mtandao wa barabara zenye urefu wa kilomita 85,000. Barabara hizi zinajumuisha barabara kuu kilomita 10,300, barabara za Mikoa kilomita 24,700 na barabara za Wilaya na Miji zenye jumla ya kilomita 50,000. Zipo sababu kadhaa zinazokwamisha Serikali kuzifanyia matengenezo ya kutosha barabara zote nchini. Sababu hizo ni pamoja na ukubwa wa mtandao wa barabara, uhaba wa vifaa vya matengenezo ya barabara, uhaba wa wataalam na zaidi ya yote ufinyu wa bajeti ya kutunza barabara unaosababishwa na kiwango kidogo cha fedha kinachotengwa kwa mwaka. Kwa mfano, katika mwaka 2002/2003, Serikali ilitenga shilingi bilioni 64 tu ikilinganishwa na mahitaji halisi yanayokadiriwa kufikia shilingi bilioni 109. Hali

hii inasababishwa na hali duni ya uchumi wetu. Hata hivyo, Serikali itaendelea na juhudi zake za kuboresha mtandao wa barabara kadri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu.

- (a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara zinatumika kama ilivyokusudiwa, watekelezaji (*Implementing Agencies*), hutekeleza kazi za barabara kwa kufuata *Performance Agreements*, zinazosainiwa kati yao na Bodi ya Mfuko wa Barabara. Aidha, Bodi hii hufanya ukaguzi wa kitaalam (*Technical Auditing*) mara mbili kwa mwaka ili kuangalia malengo yaliyofikiwa ukilinganisha na fedha zilizotolewa.
- (b) Mheshimiwa Spika, inapogundulika kuwa fedha za matengenezo ya barabara zimetumika isivyo kusudiwa, Bodi ya Mfuko wa Barabara husitisha utoaji wa fedha kwa Taasisi husika hadi fedha hizo zitakaporejeshwa katika Akaunti ya Mfuko wa Barabara na watendaji waliotumia ovyo fedha hizo, wanaweza kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha za Mfuko wa Barabara zinazopelekwa katika Halmashauri na Manispaa na hatimaye kwenye Majimbo yao na kuwahoji kwa ukamilifu watendaji wakati wa vikao vya Bodi za Barabara za Mikoa.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mikoa yote nchini hutofautiana katika suala la ukubwa kieneo na vilevile hali za kijiografia ambazo mara nyingi hali hizo za kijiografia husababisha matengenezo ya barabara kutokuwa ya kudumu katika maeneo yenyenye mvua nyingi kama vile Mikoa wa Ruvuma:-

- (a) Je, Wizara huwa inazingatia vigezo hivyo vya hali za kijiografia na ukubwa wa maeneo katika kugawa fedha zao?
- (b) Ni Mikoa ipi yenyenye matatizo hayo ya kijiografia na ukubwa wa kieneo iliyoweza kupatiwa fedha za kutosha katika bajeti ya mwaka uliopita na Mikoa ipi yenyenye sababu hizo za kijiografia na kieneo iliyopewa fedha kidogo katika kipindi cha bajeti cha mwaka uliopita?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, sijui kama unazo takwimu hizo lakini jaribu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kabisa Mfuko wa Barabara huzingatia tofauti zilizopo kutoka Mikoa hadi Mikoa kwa kugawa fedha kwa kadri ya Mikoa na matatizo yake. Lakini hata ukijitahidi vipi fedha zitakazotolewa na Mfuko wa Barabara haziwezi kutosheleza mahitaji halisi ya Mikoa hiyo.

Pili, Mheshimiwa Spika, kwa sababu swali lake linahitaji takwimu, ningeomba Mheshimiwa Mbunge, aridhike kwamba nitamletea takwimu hizo sahihi baadaye.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha kwa hiyo, tunaendelea na shughuli nyingine. Matangazo ya vikao vya Kamati kwa leo ni kama ifuatavyo:-

Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti Mheshimiwa Njelu Kasaka, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 5.00 asubuhi hii chumba namba 56 katika vyumba vya Kamati.

Kamati ya pili, ni Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu wakutane leo vilevile saa 5.00 asubuhi chumba namba 84 katika vyumba vya Kamati.

Kamati ya Tatu, ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Kaimu Mwenyekiti, Mheshimiwa Parseko Kone, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, wakutane saa 5.00 ile ile chumba namba 81 katika vyumba vya Kamati.

Tangazo la nne, lakini hii siyo Kamati lakini Mheshimiwa Jenista Mhagama, ameniomba niwatangazie Wabunge wote Wanawake kwamba, wakutane leo saa 7.00 mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge cha asubuhi.

Nitoe taarifa tu kwamba, hoja iliyoko kwenye *Order Paper* leo imepangiwa siku mbili yaani leo na kesho. Orodha ya waliokwisha kuomba kuchangia itawekwa pale mahali pa kawaida ili aliyeomba ajue kwamba jina lake limefika.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Tume ya Utumishi wa Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri, kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

SPIKA: Samahani Mheshimiwa Waziri unayo nusu saa, dakika 30.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:
Mhehsimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhud zake kubwa anazoziedeleza za kufufua uchumi wa nchi hii. Aidha, nampongeza kwa juhud na ushirikiano wake mkubwa katika kuhakikisha kuwa amani inakuwepo ndani ya nchi na katika nchi za Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhud zake za kuendelea kuimarisha Muungano na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kuondoa umaskini. Aidha, napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi wote, ambao wa meshinda katika Chaguzi Ndogo zilizofanyika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mbunge wa Hanang, kwa hotuba yake iliyoeleza mwelekeo wa majukumu ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004. Napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itatekeleza maagizo yaliyomo katika hotuba yake inayozingatia malengo na mikakati tuliojiwekea katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Aidha, naomba niwashukuru na kuwapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Pesambilii Mramba, Mbunge wa Rombo, kwa hotuba zao ambazo zimefafanua hali ya uchumi wa nchi na kufanya tathmini ya Bajeti ya Serikali katika kipindi cha mwaka 2002/2003 na matarajio kwa kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuipongeza Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athuman Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kuchambua kwa kina Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TUMITAA, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri, kwa mwaka wa Fedha 2003/2004. Maoni na ushauri wa Kamati utazingatiwa wakati wa kutekeleza majukumu na malengo yaliyowekwa katika maeneo yote kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nachukua nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwa familia, ndugu na jamaa wa Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafu, Marehemu Francis Nyalali, aliyefariki dunia 2 Aprili, 2003. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. (*Amin*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2002/2003, pamoja na maelezo ya malengo ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TUMITAA, Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa Fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha zoezi la kuandaa Mpango wa Muda wa Kati wa utendaji kazi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeandaa Mkataba wa Huduma kwa Wateja wenyewe kulenga kuboresha ufanisi na tija katika utoaji huduma. Mkataba huu ulizinduliwa rasmi 13 Novemba, 2002 na kuanza kutekelezwa. Nakala za Mkataba huo zimesambazwa kwa wadau wote. Kwa mujibu wa Mkataba huo, Wateja wetu wanakaribishwa kutoa maoni yao kwa shabaha ya kuboresha zaidi.

Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilianda na kutoa mafunzo kwa Viongozi na Watumishi wa ngazi mbalimbali wa Makao Makuu ya Ofisi, Mikoa na Halmashauri. Katika Mpango wa Muda wa Kati wa Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa, umeandaliiwa mkakati wa kuimarisha uwezo wa Sekretarieti za Mikoa ili ziweze kutoa ushauri kwa Halmashauri ipasavyo. Aidha, utaratibu umewekwa wa kuhakikisha kwamba, watumishi wa Sekretariet za Mikoa na Halmashauri wanapata nafasi za kutembelea nchi mbalimbali zenye mipango ya maboresho ya Serikali za Mitaa ili kubadilishana uzoefu na kujifunza kutoka nchi hizo. Kwa utaratibu huu, Serikali ya Japan kwa kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (*JICA*), imekubali kupeleka washiriki 67 Japan kujifunza mikakati mbalimbali ya kutekeleza maboresho ikizingatiwa kuwa Japan walanza maboresho mwaka 1888 na wanaendelea hadi leo hatua kwa hatua.

Hadi sasa washiriki 14 ambao walihusisha Makatibu wa Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri kutoka Mikoa ya Dodoma, Mbeya, Morogoro na Tanga, pamoja na Halmashauri za Manispaa za Dodoma na Mbeya, Halmashauri za Wilaya za Dodoma, Mbeya, Mbozi, Morogoro, Ulanga, Korogwe na Muheza, wameshiriki mafunzo haya.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mafunzo yanayotolewa kwa Viongozi na Watendaji mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (a) Mafunzo ya utunzaji taarifa na mawasiliano kwa kutumia kompyuta kwa Maafisa Waandamizi 40 wa Makao Makuu ya Ofisi;
- (b) Mafunzo ya mbinu na stadi za kusimamia mabadiliko yanayoendeshwa hapa nchini na Chuo cha Menejimenti cha Dublin, Ireland, yanahudhuriwa na Wakurugenzi wote wa Halmashauri. Mafunzo haya niliyazindua rasmi tarehe 7 Aprili, 2003 huko Mwanza na yatakamilika tarehe 11 Julai, 2003. Katika mafunzo haya, uwezo wa utendaji wa Wakurugenzi utapimwa na matokeo yake yatawasilishwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili kubaini wale wenyewe uwezo wa utendaji wathibitishwe katika nyadhifa zao na wale wenyewe mapungufu wataondolewa;
- (c) Mafunzo ya Utawala Bora kwa Makatibu Tarafa 104 kwa Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Kigoma. Mafunzo haya yataendelea kutolewa kwa Makatibu Tarafa waliobakia;
- (d) Mafunzo ya ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu yalitolewa kwa Maafisa Wakuu wa Idara za Halmashauri za Mikoa ya Kagera na Shinyanga;
- (e) Mafunzo ya mbinu na stadi za kazi yalitolewa kwa Maafisa Watendaji wa Kata 1,561. Maafisa Watendaji 976 waliobaki, pamoja na Maafisa Watendaji wa Vijiji watakaoteuliwa, watapatiwa mafunzo katika kipindi kijacho;
- (f) Mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani yalianza Machi, 2003 na yanaendelea;

(g) Mafunzo kwa Viongozi wa Serikali za Mitaa, yaani Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa. Viongozi 71,000 tayari wamepatiwa mafunzo na tathmini inafanywa ili kuboresha maeneo yenyepungufu; na

(h) Semina na warsha mbalimbali zenyenye lengo la kuboresha utendaji.

Mheshimiwa Spika, vitende kazi ni nyenzo muhimu sana katika kuleta ufanisi katika utendaji kazi. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imewapatia watumishi wake vitende kazi kama vile kompyuta na vyombo vya usafiri ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Aidha, baadhi ya Halmashauri zimepatiwa kompyuta, mashine za faksi, balskeli, pikipiki na vifaa vingine muhimu vya ofisi.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha hali ya mawasiliano kati ya Makao Makuu ya Ofisi, Mikoa na Halmashauri, programu ya ufungaji wa mtandao wa mawasiliano kwa kutumia *Internet* inaendelea. Utekelezaji wa programu hiyo utaboresha upatikanaji na usambazaji wa taarifa na takwimu kutoka kwa Wadau mbalimbali. Programu hii inatekelezwa kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataida (*UNDP*) na Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*). Chini ya programu hii, Ofisi yangu imepokea kompyuta na vifaa vya mtandao wa *Internet*, ambavyo vimeanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inayo Maktaba ambayo inatoa huduma kwa watumishi pamoja na wateja wake. Katika mwaka uliopita vitabu na majorida mbalimbali vimenunuliwa ili kuimarisha Maktaba hiyo. Katika kipindi kijacho, inakusudiwa kununua vitabu na nyaraka mbalimbali zinazohusiana na shughuli za Halmashauri. Vifaa vingine vitaendelea kununuliwa ili kuiwezesha ofisi kuweka kumbukumbu za matukio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora unajumuisha Utawala wa Sheria. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepewaa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo kwa lengo la kuweshera uendeshaji wa shughuli za kijamii na za maendeleo. Kwa kawa Sheria Ndogo zinazotungwa na Halmashauri huandikwa kwa lugha ya Kiingereza, ingawa wananchi wengi wanaopaswa kuzielewa na kuzifuata hawajui Kiingereza. Napenda kutumia fursa hii kuziagiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba, kwa kadri inavyowezekana, Sheria Ndogo zinatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na zinasambazwa katika ngazi za Kata na Vijijini. Kila Afisa Mtendaji Kata na Kijiji anapaswa kuwa na Sheria hizi ili aweze kusimamia utekelezaji wake kwa manufaa ya wananchi katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliweza kuitisha Mikutano ya kazi ambayo iliwezesha kuweka mikakati ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali, kubadilishana usoefu na kujadili masuala ya utendaji kazi. Mkutano mmojawapo uliokuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais, uliwhusisha Viongozi Wakuu Serikalini wakiwemo, Makamu wa Rais, Spika, Waziri Mkuu, Mawaziri, Makatibu Wakuu na Viongozi wa ngazi za juu wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri. Dhana ya Utawala Bora ilikuwa ni moja kati ya mada zilizojadiliwa kwa kina katika mkutano huo.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha hali ya utawala na kuongeza usimamizi wa karibu katika utoaji huduma kwa wananchi katika ngazi ya Mtaa, ilipendekezwa kuwepo kwa cheo na nafasi ya Mtendaji wa Mtaa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imekubali kuundwa kwa nafasi ya Afisa Mtendaji wa Mtaa. Aidha, kuanzia Januari, 2004 Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa wataajiriwa na Serikali Kuu. Taratibu za ajira, ngazi za mishahara, madaraja na majukumu ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa zimeandaliiwa. Halmashauri zote nchini zinatakiwa kuzingatia kikamilifu utaratibu wa ajira za Watendaji hususan masharti ya ushindani kama yalivyo katika Sera ya Menejimenti na Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha Utawala Bora katika ngazi ya Wilaya, Wizara ya Fedha itapeleka fedha za matumizi mengineyo moja kwa moja kwenye Ofisi za Wakuu wa Wilaya. Awali, fedha hizo zilikuwa zinakasimiwa na kutolewa ndani ya Fungu la Mikoa na Ofisi za Wakuu wa Wilaya, kugawiwa kiasi ambacho hakikuwa na uhakika. Hii iliwfanya Wakuu wa Wilaya kushindwa kupanga matumizi ya fedha hizo na kuweka utaratibu mzuri wa kufanya kazi zao. Aidha, utaratibu huu uitaandaliiwa

kwa ajili ya fedha za Ofisi za Wabunge ili zitengwe chini ya kifungu cha Ofisi za Wakuu wa Wilaya na kupelekwa moja kwa moja Wilayani. Kwa mwaka 2003/2004, fedha hizi zimetengwa chini ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa. Makatibu Tawala wa Mikoa watahakikisha kwamba, fedha hizi zinatumika kwa ajili ya ukarabati na kuhudumia Ofisi za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, lengo la Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kuainisha maeneo yote yenye mianya ya rushwa. Ofisi yangu, Mikoa, pamoja na Halmashauri, zimebainisha maeneo yenye mianya ya rushwa. Ili kuziba mianya hiyo, ofisi imeendelea kuhakikisha kuwa:-

(a) Ununuzi wa vifaa unazingatia Sheria na Kanuni za manunuizi (*Public Procurement Act.No.3/2001 and Regulations of 2001*);

(b) Ajira na upandishwaji vyeo unafanyika kwa uwazi zaidi kwa kutangaza nafasi wazi na kufanya usaili; na

(c) Kuendesha semina kwa baadhi ya watumishi kuhusu mikakati ya kupambana na rushwa ngazi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, katika mafunzo yote ya Viongozi na Watendaji wa Halmashauri, somo la Vita Dhidi ya Rushwa linatiliwa mkazo.

Lengo kwa mwaka 2003/2004, ni kuendeleza juhudhi za kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inatambua madhara makubwa yanayosababishwa na UKIMWI hususan kupotea kwa nguvu-kazi ya Taifa na kuongezeka kwa umaskini. Hivyo, tunaunga mkono vita dhidi ya UKIMWI inayoendeshwa na Serikali na Asasi nyininge ili kupunguza kasi ya maambukizi mapya na kulinusuru Taifa. Ofisi yangu kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*), imewapatia watumishi mafunzo ya aina mbalimbali kwa lengo la kubadili tabia na imetayarisha vitini vya kuelimisha Viongozi na Watendaji wa Halmashauri kuhusu athari za UKIMWI. Vilevile imeandaa na kuratibu Waraka wa Kuunda Kamati za kusimamia na kuratibu mapambano dhidi ya UKIMWI na pia kuainisha majukumu ya Kamati hizo kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Mtaa na Kitongoji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la matumizi bora ya ardhi, mkazo mkubwa umewekwa katika kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo uliotolewa mwaka 2002 na Ofisi yangu na Sera ya Maendeleo ya Makazi iliyotayarishwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Aidha, Mwongozo wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, katika Kijiji ulioandalowi na Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi umesambazwa katika Halmashauri zote nchini. Sera pamoja na miongozo hii inaelekeza wananchi umuhimu wa kuwa na mipango bora ya matumizi ya ardhi kwa nia ya kuepusha migogoro ya ardhi na kuhifadhi mazingira. Kwa ujumla hali ya migogoro ya ardhi imepungua kwa kiwango kikubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza mwaka 2002 wakati nikitoa hotuba yangu ya Bajeti, juhudi za kuondoa umaskini nchini zitategemea sana kutekelezwa kwa Sera ya Maendeleo Vijijini na Mkakati wake. Ofisi yangu imekamilisha sera hiyo ili iweze kutekelezwa ikiwa ni nyenzo muhimu katika vita dhidi ya umaskini. Katika mwaka 2003/2004, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itahakikisha kuwa inasimamia utekelezaji wa sera hiyo kwa ushirikiana na Wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, uandaaji wa mwongozo unaotoa fursa kwa jamii kumiliki shughuli za kupanga, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za maendeleo umekamilika. Aidha, vimeandalowi vitini vya aina 4 ambavyo ni Kiongozi cha Mkufunzi, Mchakato wa Kijijini, Mchakato wa Mjini na Kitabu cha Rejea. Mafunzo ya matumizi ya mfumo wa upangaji mipango shirikishi jamii wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (*O and OD*), yalianza kutolewa katika Halmashauri ya Bagamoyo, Kibaha, Manyoni, Kisarawe na Halmashauri ya Mji wa Singida, baada ya majoribio ya mfumo huu yaliyofanyika katika Halmashauri ya Hai kufanikiwa. Mfumo huu umeanza kuenezwa katika Halmashauri za Makete, Mbarali, Kilosa, Magu, Musoma, Ngara, Kibondo, Masasi, Mtwara, Songea, Mufindi na Manispaa ya Temeke. Lengo ni kuendeleza mfumo huu katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, baada kuanzishwa kwa Wilaya mpya za Kiutawala za Kilindi, Kilolo, Namtumbo, Kishapu, Mvomero, Uyui, Nyamagana na Ilemela mwezi Julai, 2002, Serikali ilieleza bayana kuwa mamlaka za Serikali za Mitaa hazitaanzishwa mara moja. Wilaya za Nyamagana na Ilemela zitaendelea kuwa chini ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Hivyo, hazitahusika katika kuunda Halmashauri mpya. Ofisi yangu ilikwisha kutoa mwongozo rasmi kwamba, Halmashauri za sasa za Handeni, Iringa, Songea, Shinyanga, Morogoro na Tabora zinaendelea kuwepo. Kwa sasa zimeundwa Kamati za Madiwani za Maandalizi ya Uanzishaji wa Halmashauri mpya kwa kila Wilaya. Kamati hizo zimepewa jukumu la kuratibu shughuli zote za Halmashauri ndani ya eneo la Wilaya isipokuwa kwa yale majukumu ambayo hayaruhusiwi kukasimiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzoefu uliopatikana tangu mwongozo utolewe imedhihirika kuwa utaratibu wa sasa wa Kamati haukidhi matakwa ya kuunda Halmashauri mpya ifikapo mwaka 2005. Ili kuondoa upungufu huu, ninakusudia kuunda Tume ya Utendaji badala ya Kamati za sasa. Tume hizo zitakuwa na jukumi la kusimamia maandalizi ya kuunda Halmashauri katika Wilaya hizo ifikapo mwaka 2005. Vilevile zitasimamia matumizi ya fedha za maendeleo na matumizi ya kawaida ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wilaya hizo mpya. Aidha, Serikali ilikwishatangaza kuanzishwa kwa Halmashauri za Miji kwa iliyokuwa Miji Midogo ya Kibaha na Korogowe na Kijiji cha Babati. Hati na nyaraka za uanzishwaji wa Miji hiyo zitawasilishwa kwenye Bunge hili linaloendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeendelea kushughulikia migogoro ya mipaka katika maeneo mbalimbali. Aidha, Ofisi yangu imekamilisha pendekezo la marekebisho ya Tangazo la Serikali Na.65 la mwaka 1961, linalolezea mipaka kati ya Mikoa ya Dodoma na Arusha katika Wilaya ya Kondoa na Wilaya ya zamani ya Masai iliyojumuisha Wilaya za sasa za Kiteto, Simanjiro, Monduli na Ngorongoro. Wananchi wa maeneo hayo wanatakiwa kuzingatia maelezo na maelekezo ya Serikali yaliyotolewa na kuheshimu mipaka iliyowekwa. Migogoro ya mipaka inayohusisha Wilaya ya Kahama na Bukombe na kati ya Bukombe na Biharamulo imetatuliwa kwa kuandaa maelezo ya mipaka kati ya Mikoa ya Kagera na Shinyanga kama liliyvo Tangazo la Serikali Na.27 la mwaka 1961 lililoweka mipaka hiyo. Mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Manyoni na Sikonge umetatuliwa kwa kuhakiki maelezo ya mipaka na kubaini kuwa hapakuwepo na tatizo la mipaka. Hivyo, Kijiji cha Kalangali kilichodaiwa kuwa kipo katika Wilaya ya Manyoni kitaendelea kuwa katika Wilaya ya Sikonge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, hali ya watumishi katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri inaonyesha kwamba, bado kuna uhaba mkubwa wa watumishi. Watumishi wanaohitajika katika Sekretarieti za Mikoa ni 1,743 ikilinganishwa na 1,262 waliopo. Ofisi yangu inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi na Wizara za Kisekta kuangalia uwezekano wa kujaza nafasi wazi katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri. Aidha, taratibu za kuunda cheo kipycha Katibu Tawala Msaidizi zimekamilika. Zoezi la kujaza nafasi hizi linaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 nililifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikishirikiana na Wizara ya Fedha inaendelea kutafiti njia za kuboresha mapato ya Halmashauri. Ili kuondoa kero zinazotokana na kodi mbalimbali zinazotozwa na Halmashauri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeandaa Mwongozo Maalum kufafanua Tamko la Serikali lililotolewa mwezi Desemba, 2002 juu ya kufutwa kwa kodi zenye kero kwa wananchi na Wawekezaji. Halmashauri zilipewa muda wa miezi 6 kuainisha na kufuta vyanzo hivyo na kuandaa bajeti upya kwa kuzingatia mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kufuta kodi zenye kero ikiwepo Kodi ya Maendeleo, nimekwishatoa Agizo linalozielekeza Halmashauri kuitisha Vikao vya Mabaraza ya Madiwani kufuta Sheria Ndogo zilizotumika kutoza Kodi ya Maendeleo na kodi zenye kero kama zilivyoordheshwa katika Agizo hilo la Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha. Hatua za kufuta kodi zilizoainishwa kama kero zinatakiwa ziwe zimekamilika kabla ya tarehe 30 Juni, 2003. Halmashauri zitakazokiuka Agizo hili na kuendelea kutoza kodi zilizofutwa zitakuwa zinakiuka maagizo halali ya Serikali na zitachukuliwa hatua kali. Ni dhahiri kwamba, hatua ya kufuta kodi mbalimbali zinazotozwa na Halmashauri itazipunguzia Halmashauri mapato kwa kiasi kikubwa. Hivyo, pamoa na fidia itakayotolewa na Serikali kwa Halmashauri ambayo haitoshelezi, suala la wananchi kushiriki kikamilifu

katika kujiletea maendeleo yao haliwezi kuepukika. Hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitatakiwa kuweka mipango mizuri ya kuwashirikisha wananchi katika maeneo yao kubuni na kutekeleza mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003 mapato yatokanayo na vyanzo vya Halmashauri, yanatarajiwa kupungua sana kutokana na hali ya hewa kuwa mbaya pamoja na kufutwa kwa kodi zenye kero. Mwaka 2002, Halmashauri zilipanga kukusanya Sh.66,291,571,612/= kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato na kiasi cha Sh.55,187,451,655/= zilikusanywa. Mwaka 2003 Halmashauri zilitarajia kukusanya kiasi cha Sh. 73,938,339,965/= kutokana na vyanzo hivyo (kabla ya Serikali kufuta Kodi ya Maendeleo na kodi zenye kero).

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2002/2003, nilieleza kwamba, Halmashauri 114 zilifunga vitabu na kuwasilisha hesabu kwa wakati kwa Ukaguzi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa ujumla Halmashauri zimeendelea kufunga vitabu kwa wakati na kuwasilisha hesabu hizo kwa Ukaguzi. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imekwishapokea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Halmashauri zinazoishia Desemba, 2001. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kati ya Halmashauri 117, Halmashauri 68 zilipata Hati Safi za Ukaguzi (*Clean Certificate*), ikilinganishwa na Halmashauri 3 zilizopata Hati Safi kwa mwaka 2000. Aidha, Halmashauri 40 zilipata Hati Chafu (*Adverse Opinion*), ikilinganishwa na Halmashauri 76 zilizopata Hati za aina hiyo kwa mwaka 2000. Nachukua nafasi hii kuzipongeza Halmashauri zote zilizopata Hati Safi za Ukaguzi na kuhimiza Halmashauri zilizopata Hati Chafu kuchukua hatua za dhati kuweka hesabu zao katika hali nzuri na kuwawezesha kupata Hati Safi za Ukaguzi mwakani.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanya uchambuzi wa hali ya madeni ya Halmashauri. Kwa takwimu za madeni zilizopokelewa hadi Mei, 2003, Halmashauri nchini zinadaiwa jumla ya Shilingi 36,106,266,623.48. Madeni makubwa kati ya hayo ni ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Shilingi 3,927,609,006/=, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa Shilingi 1,127,290,094/=, TALGWU Shilingi 234,151,992/=, Bima Shilingi 201,053,187/=, Vyama vya Kuweka na Kukopa Shilingi 24,516,081/= na WADU Shilingi 11,708,652. Madeni mengine ya Shilingi 30,579,937,611.48 ambayo Halmashauri ziliikuwa zimelimbikiza hadi Desemba, 2001 yалиhusu malimbikizo ya mishahara, posho za kujikimu, likizo na madeni ya Wazabuni. Ofisi yangu inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha kuangalia uwezekano wa kulipa madeni hayo kurudisha imani za Wazabuni na Watumishi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa utoaji wa leseni mbalimbali katika Halmashauri una mlolongo mrefu ambao unaleta usumbu kwa wafanyakishara. Kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais ya kuondoa usumbu huo wa utoaji leseni, Halmashauri zote zimeelekezwa kuanzisha kituo kimoja cha kutolea leseni (*One Stop Licensing Centre*). Kwa utaratibu huu mpya, mfanyakishara hatahusika tena kutembeza nyaraka mbalimbali za leseni na badala yake kazi hiyo itafanywa na watumishi wa Halmashauri. Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Mapato na Wizara ya Viwanda na Biashara, imekwishaandaa mwongozo kuhusu suala hili na kuutuma kwenye Halmashauri zote na utaanza kutekelezwa kuanzia mwezi Julai, 2003. Utaratibu huo utakapoanza kutumika, utaondoa kero kwa wafanyakishara na kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kufuata Tangazo la Serikali Na. 137 la mwaka 1990, iliyatangaza maeneo ya Vijiji vya Njombe, Kahama, Masasi, Kondoa, Kibaha, Sengerema, Mpanda na Korogwe kuwa Miji Midogo. Mwaka huu inakusudia kuyatangaza maeneo mengi ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya kuwa na Hadhi ya Miji Midogo na kuyaondolea Hadhi ya Vijiji. Jumla ya Mamlaka za Miji midogo inayohusika na uamuhi huu ni 88. Orodha ya majina na maeneo ya Miji Midogo inayokusudiwa kuanzishwa imepelekwa kwa Wakuu wa Mikoa waweze kuifanya uhariri kabla ya tangazo rasmi kutolewa katika Gazeti la Serikali. Mamlaka hizo za Miji Midogo zitaanza Januari, 2004.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Serikali za Mitaa imepewa jukumu la kusimamia, kuimarisha na kuendesha Utumishi wa Serikali za Mitaa. Katika mwaka wa fedha 2002/2003, TUMITAA imeshughulikia masuala yafuatayo:-

- (a) Kuandaa na kuhuisha aina 50 za Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya Serikali za Mitaa. Baraza la Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa limekwishapitisha Miundo hii na itanza kutumika katika mwaka wa fedha ujao;
- (b) Kuandaa na kukamilisha Ikama za Watumishi wa Halmashauri 117;
- (c) Kufanya usaili wa kujaza nafasi wazi 13 za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara 38;
- (d) Kuandaa kumbukumu za Watumishi wa ngazi ya LGGS5 na kuendelea kwa kutumia Kompyuta;
- (e) Kupandisha vyeo watumishi 1,126 wa Kada mbalimbali katika Halmashauri;
- (f) Vibali vya kuajiri watumishi 12,611 wa Kada mbalimbali;
- (g) Masuala ya nidhamu 29;
- (h) Kuhamia Dodoma na kuboresha Ofisi zake kwa kununua samani mpya pamoja na vitendea kazi; na
- (i) Kuwapatia watumishi 21 mafunzo ya kompyuta, ukarani, Uhaisibu, Biashara, mafunzo ya uzamili katika fani ya Utawala, Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, TUMITAA imojiwekea malengo yafuatayo:-

- (a) Kuandaa kanuni na miundo ya utumishi kulingana na mabadiliko yanayoendelea katika Utumishi wa Serikali za Mitaa;
- (b) Kuangalia na kutathmini utekelezaji wa masuala ya Utumishi katika Halmashauri kulingana na Kanuni na Taratibu za Utumishi katika Serikali za Mitaa;
- (c) Kuhakikisha mashauri ya nidhamu yanakamilika katika wakati muafaka kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Serikali za Mitaa;
- (d) Kuhakikisha nafasi zote wazi za ajira zinajazwa kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira; na
- (e) Kuimarisha Ofisi kwa kununua Vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kutungwa kwa Sheria Na. 6 ya mwaka 2000, shughuli za Mfuko zimeimarishwa kimundo na kiutendaji. Chini ya Sheria hiyo, majukumu makuu ya Mfuko yameainishwa kuwa ni:-

- (a) Kubuni sera na kusimamia ulipaji wa mafao kwa wanachama waliopo na wale watakaojiunga na Mfuko baadaye; na
- (b) Kubuni na kutekeleza mikakati endelevu ya kuboresha mafao na maisha ya baadaye ya izeeni kwa wanachama.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2002/2003, Mfuko ulitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuandikisha upya Wanachama 2,584 katika Halmashauri za Mkoa wa Dodoma ili kurahisisha ukusanyaji wa michango na ulipaji wa mafao;
- (b) Kukusanya michango toka kwa wanachama. Kiasi cha Sh.19,298,387,556/= kilipatikana kati ya Sh.21,313,164,500/= zilizokusudiwa ikiwemo riba na marejesho ya fedha zilizowekwa katika dhamana za Serikali na Mabenki;
- (c) Kulipa mafao ya Sh.445,302,242/= kwa wanachama waliostaifu au kuacha kazi; na
- (d) Kuwapelekea Wanachama taarifa za michango yao hadi mwaka 1999/2000.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 wakati nikiwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiil nilisema kwamba, Mfuko ulikuwa unafanyiwa uchambuzi wa kina kwa lengo la kuubadili na kuwa wa malipo ya pensheni tofauti na malipo yanayotolewa sasa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji wa zoezi hilo sasa umekamilika na taarifa ya mradi huo yaani *Final Project Report*, imekwishawasilishwa kwenye Bodi ya Wadhamini wa Mfuko kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Mfuko wa *LAPF* katika miaka ya hivi karibuni umeweza kupata maendeleo ya kuridhisha kwani kwa mujibu wa hesabu zake za 2002 Mfuko uliongezeka kwa asilimia 25.51 kutoka Sh.40,457,906,830/= mwaka 2001 hadi Sh.50,759,697,244/. Katika jitihada zake za kuboresha mafao, Mfuko uliwapa wanachama riba ya asilimia 10 kwa hesabu zake za 2000/2001. Kiwango hiki cha riba bado ni cha juu ikilinganishwa na riba zinazotolewa na Asasi nyingine za fedha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba michango yote ya Wanachama inakusanywa kwa wakati, kuanzia mwezi Septemba, 2002 Hazina ilianza kupeleka fedha zote za makato ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa moja kwa moja kwenye Mfuko wa *LAPF* badala ya kuitisha fedha hizo kwenye Halmashauri kama ilivyokuwa ikifanyika miaka ya nyuma. Utaratibu huu umepunguza tatizo sugu la malimbikizo ya michango kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, bado lipo tatizo la malimbikizo ya michango ya miaka ya nyuma ambapo ilipofika mwezi Aprili, 2003 jumla ya Sh.3,927,609,006/= zilikuwa hazijalipwa *LAPF*. Kuendelea kuwepo kwa malimbikizo ya miaka ya nyuma ni baadhi ya kasoro zinazowasababishia usumbufu Wanachama wa Mfuko pale wanapodai mafao yao. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeingia mikataba na Halmashauri zote zinazodaiwa. Kwa mujibu wa mikataba hiyo, madeni yote yanatakiwa yawe yamelipwa ifikapo Desemba 31, 2003 na Halmashauri zitakazoshindwa kutekeleza makubaliano hayo zitachukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria. Ninapenda kuzikumbukusha Halmashauri zinazodaiwa kutekeleza makubaliano hayo kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Mfuko utaendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kisheria ikiwa ni pamoja na kuandikisha Wanachama, kukusanya na kutunza michango ya fedha za Mfuko, kuwekeza katika vitega uchumi mbalimbali na kulipa mafao. Aidha, pendekezo la kubadili mpango wa sasa wa malipo ya akiba kuwa wa malipo ya pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa litawasilishwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa iliundwa kwa Sheria Na. 9 ya 1982, ikiwa na madhumuni ya kutoa mikopo kwenye Halmashauri kwa ajili ya kuanzisha na kuendesha miradi ya kiuchumi na huduma nyingine kwa lengo la kuongeza mapato ya Halmashauri. Aidha, chombo hiki kina jukumu la kutoa ushauri wa kitaalam kwenye Halmashauri kuhusu vitegauchumi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Bodi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuelekeza nguvu zaidi katika kukusanya michango na marejesho ya mikopo kama njia mojawapo ya kuongeza uwezo wa Bodi kifedha. Hadi kufikia 30 Aprili, 2003, Bodi imefanikiwa kukusanya michango kiasi cha Sh.259,978,315/= ikilinganishwa na Sh.253,382,600/= zilizokusudiwa kukusanywa. Kwa upande wa marejesho ya mikopo, kiasi cha Sh.169,547,975/= kilirejeshwa. Riba iliyolipa kutookana na mikopo ilikuwa ni Sh.49,089,457/. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Bodi ya mikopo ya Serikali za

Mitaa itaendelea kukusanya michango na kufuutilia marejesho ya mikopo kama hatua ya kuongeza mtaji wa kufanya kazi (*Working Capital*).

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuifanya marekebisho Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kuiwezesha kutoa huduma zake kwa ufanisi. Moja ya hatua hizo ni kufanya uchambuzi wa Bodi hiyo kwa lengo la kubaini upungufu katika muundo, uendeshaji, masuala ya fedha na sheria. Kufuatia uchambuzi huo, Wataalam Washauri walitoa mapendekezo yafuatayo ya jinsi ya kuimarishe Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa:-

- (a) Mfuko wa Rasilimali wa Serikali za Mitaa (*The Local Government Investment Fund*);
- (b) Benki ya Rasilimali ya Serikali za Mitaa (*The Local Government Investment Bank*); na
- (c) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa katika muundo wa sasa ulioboreshw (*A Modified Local Government Loans Board*).

Mapendekezo haya yatawasilishwa Serikalini yapate kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Viongozi na Watendaji wa Halmashauri wakitumie chombo hiki kikamilifu kwa uwekezaji kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya Halmashauri na wananchi kwa jumla. Aidha, napenda kusisitiza kwa mara nyingine tena umuhimu wa Halmashauri kuhakikisha kuwa katika kipindi cha mwaka huu wa 2003/2004, zinachangia Bodi kikamilifu na kurejesha mikopo kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Elimu Kibaha lina jukumu la kupambana na maadui wa maendeleo ambaa ni ujinga, maradhi na umaskini kwa kutumia elimu. Shirika limejiwekea malengo ya miaka mitano kuanzia 2003 - 2008, kutekeleza malengo na majukumu yake ya kuondoa ujinga, maradhi na umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Shirika limetekeleza majukumu yafuatayo:-

- (a) Adui Maradhi:
 - (i) Kutoa elimu ya afya, matibabu na mafunzo ya Maafisa Tabibu. Jumla ya wanafunzi 42 wamehitimu mafunzo haya;
 - (ii) Kutoa elimu kwa akinamama juu ya lishe bora ambapo jumla ya watoto 110 walipata huduma za lishe bora; na
 - (iii) Wagonjwa 48,745 wa nje walihudumiwa, wagonjwa 12,202 walilazwa na kutibiwa na majeruhi 1,022 wa ajali za barabarani walipokelewa na kuhudumiwa.
- (b) Adui Ujinga:
 - (i) Kutoa elimu ya msingi na sekondari kwa wanafunzi 2,019;
 - (ii) Wanafunzi 134 wa Kidato cha Nne na wanafunzi 168 wa Darasa la Saba walimaliza masomo yao; na
 - (iii) Kuanza ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana.
- (c) Adui Umaskini:
 - (i) Wanafunzi 221 wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi walipatiwa mafunzo;

(ii) Shirika liliendelea na kazi ya utotoaji na uuzaaji vifaranga kwa wafugaji mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2003, vifaranga wa nyama 454,110, vifaranga wa mayai 21,769 na vifaranga vijogoo 20,558 waliuzwa kwa wafugaji mbalimbali hapa nchini;

- (iii) Lita 76,695 za maziwa zilizalishwa; na
- (iv) Shirika liliendelea kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi kutoka Vyuo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Shirika limejiwekea malengo yafuatayo:-

- (a) Kutoa mafunzo kwa wataalam wa Afya ngazi ya stashahada;
- (b) Kuendelea kutoa huduma na kupanua huduma za kinga katika hospitali na katika viji vilivymomo katika eneo maalum la kilomita 15 linalolizunguka Shirika;
- (c) Kukarabati miundo mbinu ikiwa ni pamoja na vifaa vya uganga;
- (d) Kununua dawa muhimu na vifaa vya kisasa vya uganga;
- (e) Kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi;
- (f) Kuanza ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana;
- (g) Kufundisha stadi ya kompyuta kwa wanafunzi na watumishi; na
- (h) Kuendelea na ujenzi wa maabara.

Mheshimiwa Spika, madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, kama yalivyoainishwa kwenye Sheria Na.26 ya mwaka 1994 ni:-

- (a) Kutoa mafunzo ya uendeshaji wa Serikali za Mitaa kwa Viongozi wa Watumishi walio katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa nchini;
- (b) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya taaluma ya Serikali za Mitaa;
- (c) Kutoa mafunzo juu ya mabadiliko yanayohusu Serikali za Mitaa katika mchakato wa programu ya maboresho;
- (d) Kutoa ushauri kwa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na watu binafsi kuhusu masuala yote yanayohusu Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2003 shughuli zifuatazo zimefanyika kwa viwango tofauti:-

- (a) Mafunzo yametolewa kwa Maafisa Watendaji wa Kata 152 kutoka Halmashauri 23 za Mikoa 11 nchini;
 - (b) Mafunzo ya Madiwani 146 kutoka Halmashauri 4 za Mkoa wa Dodoma; na
 - (c) Kuboresha mazingira na mandhari ya Chuo.
- Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Chuo kinatarajiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-
- (a) Kuhuisha mitaala ya masomo;

- (b) Kuajiri wakufunzi;
- (c) Kuimarisha chanzo cha maji safi na ya uhakika;
- (d) Marekebisho na ukarabati wa majengo ya Chuo hasa ukumbi wa mikutano, madarasa, mabweni, bwalo la chakula na ujenzi wa Maktaba;
- (e) Kujenga uzio kuzunguka majengo ya chuo;
- (f) Kufukiza dawa ya kuua wadudu na panya (*Fumigation*);
- (g) Kujenga na kutengeneza viwanja vyta michezo na burudani na kununua vifaa vyake; na
- (h) Kununua vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vyombo vyta usafiri.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Masoko Kariakoo lilianzishwa kwa madhumuni yafuatayo:-

- (a) Kusimamia na kuendesha Soko Kuu la Kariakoo pamoja na masoko mengine yatakayowekwa chini ya usimamizi wa Shirika; na
- (b) Kujenga masoko mengine mapya katika Jiji la Dar es Salaam na kusimamia utekelezaji wa shughuli za masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Shirika la Masoko Kariakoo lilitkeleza shughuli zifuatazo:-

- (a) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa kusimamia kwa karibu Kamati za mapato na kuweka usimamizi thabiti;
- (b) Kutengeneza maumbo 1,119 ya biashara ndogo ndogo;
- (c) Kuboresha mazingira ya soko kwa kuweka maturubai, kuchimba kisima cha maji, kununua pampu ya maji taka na kupulizia dawa majengo;
- (d) Kufanya ukarabati wa majengo;
- (e) Kulipa malimbikizo ya madeni (Sh.128 milioni kati ya Sh.161 milioni); na
- (f) Ununuzi wa vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi.

Hadi kufikia Machi, 2003 Shirika lilikusanya na kutumia Sh.555,124, 628.50 kati ya Sh.804,923,433/= zilizopangwa kukusanya kwa mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa kipindi cha 2003/2004 ni pamoja na:-

- (a) Kutengeneza maumbo 200 ya biashara ndogo ndogo;
- (b) Kuboresha mazingira ya soko la kufanya biashara kwa kuendelea kuweka maturubai, kununua pampu za maji safi, kufunga kipooza hewa na kukarabati mfumo wa umeme katika soko la jumla (shimoni);
- (c) Kukarabati paa la jengo;
- (d) Kununua vitendea kazi;

- (e) Kuendesha mafunzo kwa watumishi katika fani za biashara na Uhasibu; na
- (f) Kuendelea kutoa elimu ya biashara na afya kwa wafanyabiashara sokoni kwa lengo la kuwajengea uwezo kuendesha biashara na pia kuzingatia kanuni za usafi.

Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Shirika linatarajia kukusanya jumla ya Sh milioni 918 ikiwa ni ongezeko la Sh. milioni 112.8 ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, changamoto inayolikabili Shirika ni pamoja na yafuatayo:-

- (a) Viwango vidogo vya kodi ikilinganishwa na gharama halisi za uendeshaji;
- (b) Kupanda kwa gharama za uendeshaji; na
- (c) Uhaba wa fedha kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Mpango huu ni kuinua ubora wa huduma zinazotolewa kwa wananchi kwa lengo la kupunguza umaskini. Utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa unazingatia Sera ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi (*Decentralization by Devolution*).

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2002/2003, shughuli zilizotekelawa chini ya Mpango huu ni pamoja na:-

- (a) Kuendelea kujenga na kujembelea hali ya Utawala Bora katika ngazi za Halmashauri. Halmashauri zote zimefanyiwa uchambuzi kwa nia ya kubainisha kiwango cha utawala wa sheria, demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi, uwazi na uwajibikaji wa Halmashauri kwa wananchi;
- (b) Kuandaa vigezo vya kupima uwezo wa umakini wa Halmashauri katika kusimamia fedha zake. Vigezo hivyo sasa vinatumika katika kuchambua na kupendekeza Halmashauri zitakazopewa uhuru zaidi wa kupanga na kuamua jinsi zitakavyotumia fedha kutoka vyanzo vya mapato na ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa kufuata vigezo vinavyokubalika;
- (c) Kuandaa mapendekezo ya utoaji wa ruzuku kwa Serikali za mitaa kulingana na vigezo ambavyo viko wazi na rahisi kuelewaka;
- (d) Kuzifanyia uchambuzi Halmashauri zote kwa ajili ya kutathmini hali ya usimamizi wa fedha (*Financial Benchmarking*) na kuandaa mkakati wa kuziwezesha kuondokana na matumizi mabaya ya fedha;
- (e) Kuziwezesha Halmashauri 38 za Awamu ya Kwanza ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa kuandaa Mipango Mikakati (*Strategic Plans*) na kutayarisha miundo inayofaa kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma katika Halmashauri zao;
- (f) Kuendelea kuzichambua sheria za Kisekta kwa nia ya kuziwianisha na azma ya Serikali ya kupeleka Madaraka kwa Wananchi;
- (g) Kufanya maandalizi ya kuboresha miundo ya Halmashauri 45 za awamu ya pili ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa takwimu muhimu kuhusu utoaji wa huduma mbalimbali katika Halmashauri hizo;
- (h) Kuchapisha na kusambaza Rejesta za Vijiji na Mitaa katika Halmashauri zote za Tanzania Bara kwa mujibu wa sheria ya nchi ambayo inaagiza kuwepo kwa Rejesta za kuhifadhi takwimu za wakazi wa Vijiji na Mitaa. Matumizi bora ya Rejesta yatawezesha kujua idadi halisi ya wakazi wa vijiji na mitaa na kutambua uraia wao. Takwimu hizi zinatumika kama nyenzo kwa wananchi wa ngazi hizi wakishirikiana na wataalam wao kutoka kwenye Kata kuweza kupanga, kutekeleza na kutathmini

utekelezaji wa mipango ya maendeleo na utoaji wa huduma muhimu katika maeneo yao, ikizingatiwa kwamba sensa hufanyika mara moja katika kila kipindi cha miaka 10. Rejesta za wakazi wa vijiji na mitaa ndicho chombo kitakachotegemewa katika kutoa takwimu sahihi za idadi ya wakazi nchini wakati wowote;

(i) Kutoa mafunzo kwa viongozi na watumishi wa Serikali za Mitaa na kuwapatia vitendea kazi; na

(j) Kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inafanya zoezi la kuhuish Sheria za Serikali za Mitaa Namba 7, 8 na 9 za mwaka 1982, kwa madhumuni ya kuondoa tofauti za sasa za miaka ya fedha baina ya Serikali Kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mwaka wa fedha wa Serikali za Mitaa kuanzia mwaka ujao utakuwa sawa na ule wa Serikali Kuu yaani utsanza tarehe Mosi Julai na kuishia tarehe 30 Juni ya kila mwaka. Utekelezaji wa uamuzi huu utsanza mara baada ya Bunge lako Tukufu kuitisha mabadiliko yanayokusudiwa katika zoezi nililotaja.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo kadhaa ambayo yamekuwa yakipunguza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa. Mambo hayo ambayo ni changamoto kwa kipindi kijacho ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Dhana ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi bado haijaleweka na kukubalika kwa baadhi ya Viongozi na Watendaji Waandamizi katika ngazi mbalimbali Serikalini;

(b) Kuwepo na tafsiri tofauti na maelezo yenyе kipingana kuhusu azma ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi, kwa mfano Wizara za kisekta kuendelea kuunda Bodi mbalimbali za utoaji huduma ngazi za Mikoa na Wilaya ambazo zinawajibika moja kwa moja Wizarani;

(c) Kusita kwa baadhi ya Halmashauri katika kuendelea na hatua za uboreshaji wa miundo yao kwa kuhofia kwamba zoezi hilo linaweza kuambatana na upunguzaji wa watumishi;

(d) Kuwepo kwa idadi kubwa ya vianzio vya mapato ambavyo vinafanya ukusanyaji wa mapato haya kuwa na tija ndogo;

(e) Kuwepo kwa matukio ya wizi na ubadhirifu wa fedha za Halmashauri kutohana ukosefu wa uadilifu kwa upande wa Madiwani na Watendaji kama ilivyojitekeza katika Halmashauri za Arumeru, Arusha, Korogwe, Musoma Mjini na Tanga;

(f) Uwezo mdogo wa Watumishi katika Idara za Uhasibu kumudu utunzaji na matumizi ya fedha zinazopelekwa kwa ajili ya huduma mbalimbali;

(g) Kuendelea kuwepo kwa sheria ambazo zinakwamisha uamuzi wa Serikali kukasimu madaraka kwa Halmashauri wa kusimamia watumishi wake; na

(h) Kuangalia upya muundo na majukumu ya Kamati za Kudumu katika Halmashauri kwa shabaha ya kuondoa migongano inayojitekeza katika baadhi ya Halmashauri. Kamati za Kudumu hususan Kamati ya Fedha na Uongozi/Fedha, Mipango na Utawala katika baadhi ya Halmashauri zimechukua Mamlaka ya Baraza la Madiwani kama chombo chenye Mamlaka ya kufanya maamuzi ya kisera katika Halmashauri. Jukumu kubwa la Kamati ya Kudumu ni kuchambua masuala yanayoletwa kwenye Kamati hizi na kushauri Baraza la Madiwani kuhusu uamuzi wa kuchukuliwa katika hoja iliyojadiliwa na Kamati. Baraza la Madiwani ndilo lenye mamlaka ya kutoa uamuzi/maamuzi ambayo yanapaswa kutekelezwa na Watendaji katika Halmashauri husika. Migongano inayotokana na kupokonywa mamlaka Baraza la Madiwani na Kamati za Kudumu kwa kiwango kikubwa imezorotesha na kuvuruga jitihada za kuimarissha nidhamu, utekelezaji wa maadili ya Viongozi na Watendaji na hata kusababisha maamuzi yenyе kuathiri maslahi ya wananchi katika Halmashauri husika kufanyika kinyume cha Sheria za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

- (a) Kuendelea na juhudzi za kupeleka madaraka ya usimamizi wa fedha kwenye Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kuzipatia ruzuku kufuatana na vigezo maalum (*Formula Based*) vitakavyokubaliwa;
- (b) Kushughulikia masuala yatakayoziwesha Halmashauri kuwasimamia watumishi wao;
- (c) Kuendeleza jitihada za kuwianisha sheria za kisekta ziendane na azma ya kupeleka madaraka ya kufanya maamuzi kwenye Halmashauri; na
- (d) Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa na uboreshaji unaotekelizwa na Wizara za kisekta katika maeneo ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ni wa miaka 5 ambao umelenga katika maeneo makuu 4 kama ifuatavyo: Kuongeza uandikishaji watoto wenyewe umri wa kwenda shule, kuinua ubora wa elimu ya msingi, kujenga uwezo wa Asasi mbalimbali zinazojihusisha na elimu na kuboresha mifumo ya Taasisi.

Uzinduzi rasmi wa madarasa mapya ya MMEM ulifanywa tarehe 20 Septemba, 2002 na Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa katika Kijiji cha Mtopwa, Wilaya ya Newala, Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2002/2003, ulikuwa kama ifuatavyo:-

- (a) Watoto 1,453,483 walikuwa wameandikishwa darasa la kwanza kati ya watoto 1,600,000 waliokusudiwa. Hii imetokana na Halmashauri kutoendelea kuwaandikisha watoto wenyewe umri zaidi ya miaka 10 na uandikishaji wa kishindo wa mwaka wa kwanza.
- (b) Ujenzi wa nyumba za walimu 155 umekamilika na 325 ujenzi unaendelea;
- (c) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 9,820 umekamilika na 2,075 unaendelea;
- (d) Ujenzi wa matundu ya vyoo 10,469 umekamilika;
- (e) Utengenezaji wa madawati 110,000;
- (f) Ununuzi wa visanduku vya vifaa vya sayansi (*Science Kits*) 6,364;
- (g) Ununuzi wa vitabu mbalimbali;
- (h) Mafunzo ya Kamati ya Shule; na
- (i) Kutoa ruzuku ya *capitation* kiasi cha shilingi 14.0 bilioni.

Hadi sasa fedha zilizokwishapokelewa na kupelekwa kwa Halmashauri ni shilingi 22.5 bilioni. Kiasi cha shilingi 70 bilioni kutoka Benki ya Dunia hazijapokelewa. Kuchelewa kutolewa kwa fedha hizi kumesababisha malengo ya mwaka 2002/2003 kutofikiwa kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, mafanikio yaliyofikiwa katika mpango huu yameifanya Tanzania kupata heshima kubwa Kimatafia kwa kuhamasisha wananchi katika ujenzi wa majengo, uandikishaji wa watoto na kusimamia matumizi ya fedha zilizopelekwa hadi ngazi ya shule.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004 mpango umelenga kuendelea kutekeleza yafuatayo: Kujenga vyumba vya madarasa 14,203, kuajiri walimu 10,563, kujenga nyumba za walimu 8,000, kutoa ruzuku ya *capitation* kwa watoto milioni saba kwa kiwango cha dola kumi kwa kila mwanafunzi anayetarajiwa kuwepo darasani na kuendelea kutoa mafunzo ya kuongeza uwezo wa kusimamia utekelezaji wa mpango kwa Kamati za Shule.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pamoja wa Afya (*Health Sector Common Basket Fund*) ulianzishwa mwaka 2000/2001, kwa madhumuni ya kuboresha huduma zinazotolewa na sekta ya afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hivi sasa Halmashauri zote zinatekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Spika, maeneo makuu ya mpango huu ni yafuatayo: Utoaji wa huduma ya afya ya mama na mtoto, utoaji elimu ya afya na tiba ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza, uboreshaji wa mazingira na huduma za maji safi na salama na uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya huduma za afya kama vile mfumo wa maji safi na maji taka.

Mheshimiwa Spika, hadi Mei, 2003 mradi umeweza kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Kufanya ukarabati mdogo wa majengo ya hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati;
- (b) Kusambaza dawa katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati zilizomo katika Halmashauri 116;
- (c) Kutoa huduma za chanjo;
- (d) Kutoa mafunzo kwa Madaktari, Wauguzi na Wakunga;
- (e) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza;
- (f) Kuimarisha mfumo wa mawasiliano kwa njia ya redio na
- (g) Kununua vifaa vya Hospitali kama vile vitanda vya kujifungulia, mipira ya kuvaan mikononi (*gloves*) na mashine za kupima mgandamizo wa damu.

Hadi kufikia Machi, 2003 shilingi 10,637,916,594.85/= zilitolewa na kutumika katika Halmashauri zote nchini. Kwa mwaka 2003/2004, jumla ya shilingi 17,600,068,600/= zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango. Aidha, kazi kubwa zitakazofanywa ni kutoa elimu kwa wataalam, kuelimisha umma juu ya magonjwa mbalimbali, kununua vifaa vya kutolea tiba muhimu, uboreshaji wa mazingira na ukarabati wa majengo.

Mheshimiwa Spika, mradi unahu ukarabati wa majengo na kusambaza vifaa vya kitaalam vya hospitali. Katika mwaka 2002/2003 yafuatayo yalitekelezwa: Kuwapata Wataalam Washauri (*Consultants*) wa kufanya tathmini ya mahitaji ya ukarabati, kukamilisha mwongozo kuhusu taratibu za manunuvi na zabuni, mafunzo yamefanyika kwa Wakurugenzi, Wahandisi, Waweka Hazina na Madaktari kuhusu taratibu za zabuni, utunzaji wa majengo, vifaa na ulinzi wa mali katika vituo vya huduma za afya na watumishi wanne wa mradi wameweza kupata mafunzo katika fani zao yaani, Uhaisibu, Uhandisi na Manunuvi ya Vifaa. Mafunzo haya yameimarisha utendaji na kuinua ubora wa huduma.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka 2003/2004 ni yafuatayo: Kuzihusha Halmashauri katika kuhakiki tathmini ya mahitaji ya ukarabati na ukarabati wenywewa na kutengeneza michoro (*Standard Drawings*) ya majengo na kuandaa mwongozo kuhusu ujenzi wa majengo ya zahanati na vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, mradi huu uliana kutekelezwa mwaka 1996 na unatarajiwa kumalizika mwezi Juni, 2004. Madhumuni ya Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Mijini ni kukarabati na kufanya upanuvi wa huduma muhimu, kuijengea Miji uwezo wa utoaji huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2002/2003, mradi umeendesha mafunzo ya uongozi na utumishi, stadi za kiufundi kwa wafanyakazi wa Halmashauri na bodi za maji safi na maji taka katika Miji ya mradi. Pia mradi umetoa mafunzo kwa Madiwani na Maafisa Watendaji wa Kata kutoka Halmsahauri za Miji ya Mradi pamoja na Wakurugenzi wa Bodi za Maji Safi na Maji Taka katika Miji hiyo. Mradi umetoa mafunzo kwa walengwa 1,044 kwa kipindi cha mwaka huu kuhusu mbinu za kuboresha ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004, mradi utaendelea na mikakati ya kuboresha huduma kwa wananchi na kuzijengea uwezo Halmashauri za Miji na Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka kuziwesha kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na kuwapunguzia umaskini. Serikali inasisitiza Halmashauri kutunza miundombinu iliyojengwa kuitia mradi huu uweze kuwa kichocheo cha maendeleo ya wananchi katika hali endelevu. Aidha, Halmashauri na Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka zinashauriwa kujijengea uwezo wa ndani wa kuendeleza ujenzi wa miundombinu inayohitajika kwa maendeleo endelevu ya Miji.

Mheshimiwa Spika, programu hii inatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Muheza, Mbozi, Rufiji, Morogoro, Masasi, Iramba na Iringa. Programu inafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Norway katika Halmashauri za Wilaya za Muheza na Mbozi, Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*) katika Halmashauri za Wilaya za Rufiji na Iringa, Shirika la Maendeleo ya Uswisi (*SDC*) katika Halmashauri za Wilaya ya Morogoro, Shirika la Maendeleo la Finland (*FINNIDA*) katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na Benki ya Dunia katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Malengo ya programu hii ni pamoja na kuboresha hali ya usafiri na usafirishaji Vijijini, kupunguza muda na nguvu zinazotumiwa na wanavijiji katika shughuli za usafiri Vijijini na kuzijengea jamii uwezo wa kuendeleza na kuhudumia miundombinu ya usafiri kama vile barabara za Vijijini na zinazounganisha barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, programu inakusudia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- (a) Kutoa mafunzo kwa baadhi ya Watendaji wa Halmashauri za Wilaya kuwawezesha kutekeleza mipango yao ya barabara;
- (b) Kupanua programu hii kufikia Halmashauri za Wilaya zipatazo 35;
- (c) Kuimarisha kitengo cha uratibu kiweze kutoa ushauri kwa Halmashauri za Wilaya zinazotekeleza programu hii; na
- (d) Kuendeleza mawasiliano na programu nyingine zinazotekeleza miradi ya aina hii, kwa mfano, *TASAF* na *Rural Integrated Program Support (RIPS)*.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2002/2003, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 19,175,000,000/= kwa ajili ya Mfuko wa Barabara za Halmashauri. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Mei, 2003 kiasi cha shilingi 17,299,047,157.33/= kilikuwa kimepokelewa na kutolewa kwa Halmashauri na Asasi mbalimbali zinazohusika na utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Halmashauri zimefanyiwa ukaguzi wa matengenezo na matumizi ya fedha za barabara. Ukaguzi huu, pamoja na taarifa za utekelezaji zinazoandaliwa na Halmashauri kila robo mwaka vimeonyesha kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha katika baadhi ya Halmashauri, uhamishaji wa fedha hizo kwenda katika kazi ambazo hazikukusudiwa, kiwango kidogo cha utekelezaji wa malengo na uwezo mdogo wa baadhi ya Halmashauri kutumia fedha zilizotolewa. Aidha, kumekuwepo na tatizo la kuchelewesha taarifa za utekelezaji. Kwa mfano, katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2002/2003, Halmashauri 15 zilifungiwa kupewa fedha kwa kutowasilisha taarifa za utekelezaji na matumizi ya fedha iliyokuwa imetolewa.

Halmashauri hizi ni Kiteto, Babati, Mbulu, Rufiji, Kigoma, Kilwa, Kilombero, Morogoro, Tandahimba, Mpanda, Nkasi, Meatu, Shinyanga, Newala na Halmashauri ya Mji wa Mtwara/Mikindani. Vile vile Halmashauri za Bagamoyo, Kibaha na Ruangwa zilifungiwa kwa kutumia vibaya fedha za Mfuko huu. Halmashauri ya Kibaha imeweza kurudisha fedha hizo na hivyo kuruhusiwa kuendelea kupata fedha za Mfuko. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, washirikiane na Halmashauri zao kuongeza kasi ya utekelezaji wa mpango wa barabara na matumizi ya fedha hizo kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa ili kuwaondolea wananchi kero za miundombinu duni inayokwamisha usafiri wao wenyewe, usafirishaji na uchukuzi wa mazao yao kupelekwa kwenye masoko mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2002/2003, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikail za Mitaa, iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Sekta ya Kilimo, Huduma za Jamii, Ardhi na Makazi, Ushirika na Maliasili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 nililieze Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilishirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Ushirika na Masoko (zikijulikana kwa ujumla *Agricultural Sector Lead Ministries*) na wadau wengine, kuanda programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ya miaka mitano ambayo utekelezaji wake unaanza mwaka 2003/2004. Programu iliyoandaliwa ina sehemu tatu, moja ikiwa ni ya uwekezaji katika kilimo kwenye ngazi ya Wilaya na ngazi ya Kijiji. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inalo jukumu la kuratibu sehemu hii. Semina za kuwaelewesha watendaji katika ngazi za Mikoa na Wilaya zimefanyika na zitaendelea katika mwaka 2003/2004, kwa kujumuisha viongozi na watendaji katika Mikoa na Halmashauri kuhakikisha kwamba programu hii inafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inalo jukumu la kuhakikisha kuwa suala la kutunza na kuendeleza mazingira (*Conservation and Management of Environment*), linapewa msukumo unaostahili. Kazi hii inatekelezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Ujenzi na Wizara za kisekta nydingine na Asasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inashiriki katika maandalizi ya utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa *Management of Natural Resources* unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark na Benki ya Dunia. Mradi huu utatekelezwa kwa miaka minne kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004. Utekelezaji wake utatumia mbinu shirikishi (*Participatory Forest Management*) na utakuwa katika Mikoa minne ya Mbeya, Iringa, Morogoro na Lindi. Ofisi yangu vile vile inashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kwamba, masuala ya mazingira yanafungamanishwa (*mainstreamed*) katika utekelezaji wa mkakati wa Kupunguza Umaskini na kwamba katika viashiria vya umaskini, vimo pia vinavyohusu mazingira. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na *NEMC*, mwongozo wa jinsi ya kuzingatia masuala ya mazingira katika uendelezaji barabara unaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaendelea na juhudzi za kututua vikwazo katika maendeleo ya elimu ya msingi, huduma za afya na maji safi na salama kwa kushirikiana na Wizara husika pamoja na wadau wengine katika Sekta ya Huduma za Jamii. Aidha, tutahakikisha kuwa huduma hizo zinaboreshwu ili zichangie katika juhudzi za kuondoa umaskini kwa kuwashirikisha wananchi wakati wa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya jamii. Utaratibu huu utasaidia kuipunguzia Serikali gharama za kutekeleza miradi ya maendeleo, kuongeza uwezo wa Serikali kutoa huduma na wananchi kupata ujuzi zaidi na kumiliki miradi hiyo. Kwa kushirikiana na Wizara husika taratibu zitaandaliwa kufanikisha utekelezaji wa malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kutaka kudhibiti ukuaji holela wa Viji, maelekezo yatatolewa kuhusu masharti mapya ya uanzishaji na usajili mpya wa Viji. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitatakiwa kuzuia uanzishaji ovyo wa Viji visivyo kuwa na shughuli rasmi au idadi ya kutosha ya wakazi wake na pia kuzuia ujenzi holela wa nyumba katika maeneo yenye hatari na karibu sana na barabara. Aidha, Halmashauri zitahimizwa kuongeza kasi ya upimaji viwanja na kusimamia uendelezaji kwa kufuata kanuni za ujenzi Mijini.

Mheshimiwa Spika, ushirika wa wakulima, wafugaji na wavuvi na hata wafanyakazi na wafanyabiashara katika maeneo yao ni mojawapo ya mikakati ya kupambana na umaskini. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itashirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko katika kutoa elimu juu ya umuhimu wa ushirika katika ujenzi wa uchumi imara. Aidha, itafuatilia kwa karibu kuhakikisha kuwa ushirika wa vikundi vya kiuchumi na vyama vya kuweka na kukopa unaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliidhinishiwa jumla ya Sh. 24,446,054,700/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo, Mfuko wa Barabara na Ruzuku kwa ajili ya Shirika la Elimu Kibaha. Hadi kufikia mwezi Mei,

2003 jumla ya Sh. 21,520,988,803.33 zimepokelewa na zimetumika. Kati ya fedha hizo Sh. 315,626,336/= ziligharamia mishahara na Sh. 2,746,519,800/= ziligharamia matumizi mengineyo ya Ofisi Kuu. Shirika la Elimu Kibaha lilitumia Sh. 1,159,795,510/= kugharamia mishahara na Sh. 690,770,985/= kugharamia matumizi mengineyo. Aidha, Sh. 17,299,047,157.33 zilitumika katika Mfuko wa Barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, TUMITAA iliidhinishiwa jumla ya Sh. 624,819,800/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 jumla ya Sh. 613,137,722/= zimetumika kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziliidhinishiwa jumla ya Sh. 25,447,966,700/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi Sh. 12,271,422,400/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 13,176,544,300/= ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 Mikoa imepokea jumla ya Sh. 24,218,910,733/= kwa ajili ya kugharamia mishahara na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizi Sh. 11,537,480,164/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 12,681,430,569/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ziliidhinishiwa jumla ya Sh. 247,027,347,900/. Kati ya fedha hizi Sh. 190,643,068,900/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 56,384,279,000/= ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 Halmashauri zimepokea jumla ya Sh. 257,113,886,592/= kugharamia matumizi ya kawaida zikiwemo Sh. 200,711,509,492/= kugharamia mishahara na Sh. 56,402,377,100/= kugharamia matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ushirika wa wakulima, wafugaji na wavuvi na hata wafanyakazi na wafanyabiashara katika maeneo yao ni mojawapo ya mikakati ya kupambana na umaskini. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itashirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko katika kutoa elimu juu ya umuhimu wa ushirika katika ujenzi wa uchumi imara. Aidha, itafuatilia kwa karibu kuhanikisha kuwa ushirika wa vikundi vya kiuchumi na vyama vya kuweka na kukopa unaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliidhinishiwa jumla ya Sh. 24,446,054,700/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo, Mfuko wa Barabara na Ruzuku kwa ajili ya Shirika la Elimu Kibaha. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 jumla ya Sh. 21,520,988,803.33 zimepokelewa na zimetumika. Kati ya fedha hizo Sh. 315,626,336/= ziligharamia mishahara na Sh. 2,746,519,800/= ziligharamia matumizi mengineyo ya Ofisi Kuu. Shirika la Elimu Kibaha lilitumia Sh. 1,159,795,510/= kugharamia mishahara na Sh. 690,770,985/= kugharamia matumizi mengineyo. Aidha, Sh. 17,299,047,157.33 zilitumika katika Mfuko wa Barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, TUMITAA iliidhinishiwa jumla ya Sh. 624,819,800/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 jumla ya Sh. 613,137,722/= zimetumika kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziliidhinishiwa jumla ya Sh. 25,447,966,700/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi Sh. 12,271,422,400/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 13,176,544,300/= ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 Mikoa imepokea jumla ya Sh. 24,218,910,733/= kwa ajili ya kugharamia mishahara na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizi Sh. 11,537,480,164/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 12,681,430,569/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ziliidhinishiwa jumla ya Sh. 247,027,347,900/. Kati ya fedha hizi Sh. 190,643,068,900/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 56,384,279,000/= ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 Halmashauri zimepokea jumla ya Sh. 257,113,886,592/= kugharamia matumizi ya kawaida zikiwemo Sh. 200,711,509,492/= kugharamia mishahara na Sh. 56,402,377,100/= kugharamia matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2002/2003, Bunge lako Tukufu iliidhinisha jumla ya Sh. 64,033,575,700/= kugharamia utekelezaji wa miradi na programu chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizi Sh. 270,000,000/= ni

fedha za ndani na Sh. 63,763,575,700/= ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 jumla ya Sh. 270,000,000/= fedha za ndani na Sh. 45,753,793,930.91 fedha za nje, zimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Mikoa pamoja na Halmashauri zilitengewa jumla ya Sh. 35,652,500,400/= kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizi Sh. 7,163,746,100/= ni fedha za ndani na Sh. 28,488,754,300/= ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Mei, 2003 jumla ya Sh. 7,168,499,500/= fedha za ndani na Sh. 1,650,216,006/= fedha za nje zimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu napenda kuyashukuru Mashirika yasiyo ya Kiserikali, makundi mbalimbali na watu binafsi kwa michango yao ya hali na mali waliyotoa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, natoa shukrani kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mabenki na wahisani mbalimbali, waliochangia jitihada za Watanzania za kujiletea maendeleo. Mashirika ya Umoja wa Mataifa ni pamoja na Shirika la Kimataifa la Japan (*JICA*), Marekani (*USAID*), *DANIDA*, *DFID*, Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*), Serikali za Austria, Finland, Ireland, Sweden, Uhlanzi, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ujeruman, Uswisi, Canada, Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Bajeti inayowasilishwa leo imeandaliwa kwa ushirikiano wa watumishi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretariet za Mikoa na Halmashauri. Napenda niwashukuru Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, Katibu Mkuu Bwana Deotrephe Mmari, Naibu Katibu Mkuu Bwana Damian Foka, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Asasi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wafanyakazi wote wa Ofisi yangu. Napenda pia kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwasilishwa makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2003/2004 ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TUMITAA, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zake inaombewa jumla ya Sh. 32,292,811,800/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo Sh. 443,807,600/= ni kwa ajili ya kulipia mishahara na Sh. 31,849,004,200/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kadhalika, jumla ya Sh. 134,116,701,400/= zinaombwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Sh. 270,000,000/= ni fedha za hapa na Sh. 133,846,701,400/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, TUMITAA inaombewa jumla ya Sh. 681,486,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo Sh. 66,358,500/= ni kwa ajili ya kulipia mishahara na Sh. 615,127,500/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaombewa jumla ya Sh. 28,999,826,500/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo Sh. 14,255,244,600/= ni kwa ajili ya kulipia mishahara na Sh. 14,744,581,900/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Vile vile Mikoa inaombewa jumla ya Sh. 30,264,103,900/= kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo zikiwemo Sh. 4,630,892,800/= fedha za ndani na Sh. 25,633,211,100/= fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Halmashauri za Wilaya zinaombewa ruzuku ya jumla ya Sh. 236,886,196,400/= zikiwemo Sh. 188,705,437,300/= kwa ajili ya mishahara na Sh. 48,180,759,100/= kwa ajili ya matumi zi mengineyo. Halmashauri za Wilaya zinaombewa jumla ya Sh. 4,227,280,900/= fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Halmashauri za Miji zinaombewa jumla ya Sh. 54,087,604,600/= ikiwa ni ruzuku ya Serikali zikiwemo Sh. 41,319,087,300/= kwa ajili ya mishahara na Sh. 12,768,517,300/= za matumizi mengineyo. Kadhalika, Halmashauri za Miji zinaombewa Sh. 999,572,400/= fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, majedwali mbalimbali yamegawiwa pamoja na hotuba hii kutoa ufanuzi zaidi wa masuala yaliyoelezwa na kutoa mchanganuo wa makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, nawasilisha makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2003/2004, kama ifuatavyo:-

| | | |
|--------------------------|------------|--------------------------|
| Ofisi ya Rais - TAMISEMI | Sh. | 166,409,513,200/= |
| TUMITAA | Sh. | 681,486,000/= |
| Ofisi za Wakuu wa Mikoa | Sh. | 59,263,930,400/= |
| Halmashauri za Wilaya | Sh. | 241,113,477,300/= |
| Halmashauri za Miji | Sh. | 55,087,177,000/= |
| JUMLA | Sh. | 522,555,583,900/= |

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio haya ya matumizi ya fedha za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TUMITAA, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naafiki

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa namwita Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua matumizi haya atoe maoni ya Kamati.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (k.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1) ya Kanuni za Bunge 2003 naomba sasa kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Ofisi ya Rais - TAMISEMI na kuomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala walioshiriki katika kazi hii ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Ramadhani Khalfan, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Zahor Khamis, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Ruth Msafiri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipitia kwa makini Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya TAMISEMI tarehe 5 Juni, 2003 kama ilivyowasilishwa kwetu na Mheshimiwa Brigadia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mafungu yanayohusika na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ni kama ifuatavyo: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Serikali za Mitaa (TUMITAA) na Mikoa 21 ya Tanzania Bara na Halmashauri zake.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa mwaka 2002/2003, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo katika maeneo kadhaa. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeyafanya kazi karibu maeneo yote na hatua kadhaa za kiutekelezaji zimeonekana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji huo bado Kamati yangu iliona kuna maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi zaidi na iliagiza yaendelee kufanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2002/2003, Kamati ilifahamishwa kuwa kwa mwaka wa fedha uliopita Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilikadiria kukusanya kiasi cha Sh. 66,391,002,612.00/= na hadi mwezi Mei, 2003 Sh. 53,357,135,672.59/= zilikuwa tayari zimekusanywa.

Kwa upande wa matumizi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka 2002/2003 iliidhinishiwa Sh. 88,479,630,400.00/= ikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (Sh. 124,446,054,700.00/=) na maendeleo Sh. 64,033,575,700.00/= Hadi mwezi Mei, 2003 Sh. 21,706,879,446.00/= zilikwisha tolewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijulishwa kwamba, katika mwaka wa fedha uliopita mafanikio yaliyopatikana ni mengi na mionganoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na kuendesha mafunzo ya Wakurugenzi wa Halmashauri, Makatibu Tarafa, Madiwani, Watendaji wa Vijiji na Kata, Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa, Serikali kukubali kulipa mishahara ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa na Tume ya Utumishi wa Serikali za Mitaa (TUMITAA), kuhamishia rasmi Ofisi zake Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana Kamati yangu pia ilielezwa matatizo yaliyojitokeza ikiwa ni pamoja na kucheleva kutolewa kwa fedha za miradi kutoka kwa wahisani, hali ambayo imesababisha kucheleva kuanza kwa utekelezaji wa miradi iliyokuwa inategemea fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka ujao wa fedha Kamati yangu imeelezwa kwamba, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kugharamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Ofisi ya Rais, TAMISEMI, TUMITAA, Mikoa na Halmashauri na pia kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati, baada ya Majadiliano Kamati yangu imetoa ushauri na maoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri ufanyike utaratibu wa kupunguza kodi nyingi wanazotozwa wananchi na ambazo zimekuwa kero, mfano kodi ya baiskeli, kodi ya mikokoteni, kodi ya biashara ndogo ndogo na kadhalika. Hata hivyo, kwa niaba ya Kamati yangu napenda niipongeze Serikali kwa kutekeleza pendekezo hilo la Kamati la kufuta Kodi ya Maendeleo. (*Makofi*)

Aidha, kutokana na usumbufu mkubwa huo ambaou unaawaletea wananchi kwa hiyo kodi zimefuta na hata jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alitangaza kufutwa kwa kodi za mifugo. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa unaotumika kusimamia Mfuko wa Pembejeo unawapa gharama kubwa wakulima hadi kufikia hatua ya kukata tamaa ya kuendelea na kilimo. Hivyo, Kamati yangu inashauri Halmashauri za Wilaya zipewe uwezo wa kusimamia Mfuko wa Pembejeo kwani wao ndio walio karibu na wakulima hivyo wanaelewa matatizo yao na namna ya kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa ajira kwa makundi mbalimbali ya jamii yetu sasa limekuwa sugu na kuwa chanzo cha vitendo viovu. Hivyo, Kamati yangu inashauri Wizara hii ishirikiane na Wizara nyingine katika kutafuta namna ya kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa watumishi wenye sifa katika Idara ya Uhasibu ni kubwa katika ngazi za Mikoa na Halmashauri za Wilaya. Hata hivyo, Kamati yangu inapongeza hatua zinazochukuliwa kukabiliana na upungufu huo. Hivyo tunashauri Wizara iandae orodha ya Mikoa inayokabiliwa na upungufu huo, hatua zinazochukuliwa na jinsi upungufu huo unavyoathiri mahesabu ya Mikoa/Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri kuwa Sheria Na. 6 ya mwaka 1999 ifanyiwe marekebisho ili nafasi na majukumu ya Makatibu Tarafa yawekwe wazi na wapewe vikao vya maamuzi ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri kwamba, Wizara iandae utaratibu maalum na kusimamia ajira ya Watendaji wa Vijiji, Kata na Mitaa. Pia wapewe elimu juu ya majukumu yao katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au vyuo vingine.

Mheshimiwa Spika, agizo la Kamati yangu kwa mwaka 2002/2003 kuwa Wabunge wa Kuteuliwa, Viti Maalum na Majimbo wapatiwe Ofisi katika maeneo yao bado halijatekelezwa katika mikoa mingi. Hivyo, Kamati yangu inashauri kuwa juhudzi ziendelee ili utekelezaji huo ufanyike katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri ianzishwe Programu Maalum ya kuwapatia elimu watumishi wa ngazi mbalimbali kuhusu jinsi ya kukabiliana na janga la moto pale linapojoitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri Serikali za Mitaa zipatiwe mwongozo wa kutunga na kuandika Sheria Ndogo ili uwe unafanyiwa rejea mara kwa mara. Aidha, Sheria Ndogo zilizokwisha pitishwa zichapishwe kwa wingi na zisambazwe Wilayani na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mpango wa maboresho ya Serikali za Mitaa. Kamati yangu inapongeza hatua zilizokwishachukuliwa katika mpango huu. Hata hivyo, tunashauri kwamba mpango huo ufikie Halmashauri zote na uhusishe pia kuboresha huduma zinazotolewa kama vile huduma za afya na upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imegundua kuwa sehemu ya Miradi ya Maendeleo kwa upande wa Mikoa ni ukarabati nyumba **z** Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Hivyo, tungependa tupatiwe ufanuzi kama nyumba hizo hazihusiki katika zoezi la kuuzwa nyumba za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inapendekeza Mipango ya Maendeleo ilenge katika kupunguza hali ya umaskini inayowakibili Watanzania wengi. Kwani kwa sasa Bajeti inaonyesha fedha zinazolenga kupunguza umaskini ni asilimia ndogo sana (10% - 20%) ya Bajeti yote na katika baadhi ya Wilaya hakuna kabisa Bajeti ya maendeleo ya kilimo wakati huo huo masuala mengine kama gharama za simu na safari ndiyo zinatengewa fedha nyiningi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia inashauri kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005, mikoa yote iwe na mfumo mmoja wa uandishi wa taarifa zao zinazowasilishwa mbele ya Kamati kama zinavyoelekezwa na HAZINA na kuonyesha ufananisho wa miaka mitatu, Mwaka uliopita, uliopo na mwaka ujao. Vile vile maagizo yanayotolewa na Kamati yangu yazingatiwe katika uandaaji wa Bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliombwa iidhinishe Sh. 522,555,583,900.00/=, ambapo Sh. 352,947,925,300.00/= ni za matumizi ya kawaida na Sh. 169,607,658,600.00/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maeleo hayo naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, pia niwashukuru Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mheshimiwa Mizengo Pinda, Naibu Waziri, Wakuu wa Mikoa na wataalam wote, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati yangu. (*Makofi*)

Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa michango yao iliyowezesha kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, pia kwa namna ya kipekee kabisa napenda niishukuru Ofisi yako hususan Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa na bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ernest Zulu, kwa ushirikiano mkubwa waliouonyesha katika kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa. Mbona anasita sita. (*Makofi*)

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA - MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii kutoa, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kutoa maoni ya Kambi kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004, kwa mujibu wa Kifungu cha 43(5)(c) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2003.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Brig. Jen. Mstaafu Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Msaidizi wake Mheshimiwa Mizengo Pinda, Naibu Waziri, Wakuu wa Mikoa wote, Bwana D. Mmari, Katibu Mkuu na timu ya wataalam waliosaidiana nao katika kuandaa Hotuba na Bajeti hii ambayo kwa kiwango kikubwa inaridhisha kama itatekelezeka. Pamoja na pongezi hizo, Kambi ya Upinzani inadhani kuna maeneo ambayo yanahitaji ufanuzi wa kina kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu na Wananchi kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kurejea kwa kina Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa Mwaka wa Fedha 2002/2003 na kutafakari ni kwa kiasi gani yaliyosemwa na Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake iliyokuwa nzuri na ya kutia matumaini yametekelezwa. Kambi ya Upinzani inadhani bila kuanzisha utamaduni huu, tutakuwa na utamaduni wa kusifia hotuba, lakini hatimaye hakuna tathmini ya kuangalia ni kwa kiasi gani hotuba hiyo nzuri imetekelezwa. Kwa kutekeleza azma hiyo, tumependa kutazama maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Waziri, mwaka 2002 katika Hotuba yake kifungu 33 kuhusu Mfuko wa Barabara, alitoa taarifa kuwa Ofisi yake kwa kushirikiana na Mfuko wa Barabara na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya ukaguzi wa matumizi ya Fedha za Mfuko huo katika Halmashauri zote. Waziri alitoa taarifa kuwa Taarifa ya tathmini hiyo imeshatoka na inafanyiwa kazi kuona kama fedha hizo zimetumika vizuri. Mheshimiwa Waziri alimalizia kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kufuatilia matumizi ya fedha hizo kwenye Halmashauri zao ili barabara husika ziweze kutengenezwa kwa ubora zaidi. Kambi ya Upinzani ilitegemea kuwa Mwaka huu, Mheshimiwa Waziri atatoa matokeo ya tathmini hiyo ili Waheshimiwa Wabunge, kupitia vikao vyao waweze kufuatilia na kusimamia vizuri zaidi matumizi ya fedha za Mfuko huo.

Mwaka 2002/2003, Mfuko huo ulitoa takriban Shilingi 14 bilioni kwa Halmashauri kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizo chini ya Halmashauri. Mwaka huu wa Fedha imetengwa Shilingi 20.4 bilioni, hivyo, ni jambo la muhimu kabisa kuona jinsi Fedha za Mfuko zilivyotumika ili kufanya marekebisho pale panapohitajika. Tunaitaka Wizara itoe taarifa rasmi ni Halmashauri ngapi hazikutumia fedha hizo na kwa sababu zipi? Pia, fedha hizo zipo wapi ili zitumike kama ilivyopangwa? Wahusika katika suala hilo wamechukuliwa hatua gani na wako wapi sasa? Tunapigana vita na umaskini, lakini haiwezekani kuwavumilia watu ambao wanatumia vibaya fedha zinazopatikana au wanachelewesha matumizi yake kwa sababu zisizoleweka. (*Makofi*)

Isitoshe, kwa desturi wanaotumia vibaya (wabadhirifu), mara nyingi ni Viongozi au Madiwani na Watendaji kwa pamoja au Watendaji pekee yao. Hivyo, hatuoni busara ya kuwaadhibu Wananchi kwa ujumla wao kwa ajili ya makundi au watu wachache ambao Wizara inaweza kuwawajibisha au kuwachukulia hatua za kisheria.

Tunapenda kufahamu hasa ni hatua gani za kinidhamu na kisheria zimechukuliwa dhidi ya wahusika, kwa lengo la kukomesha ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha za umma au kuelekeza fedha za umma mahali ambapo haikupangiwa kwa hulka ya wahusika. Ni vema Basi, Waheshimiwa Wabunge wakapata nakala ya tathmini hizo, ili wawe na uwezo wa kusimamia vizuri kama Mheshimiwa Waziri alivyowaomba katika Hotuba yake ya mwaka 2002. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake ya 2002/2003, alizungumzia kwa kirefu juu ya mafanikio tuliyopata katika utekelezaji wa Mpango wa MMEM. Kambi ya Upinzani haina tazizo na mafanikio hayo na Waziri ameelleza vizuri tena katika hotuba yake ya mwaka huu. Napenda

kuipongeza Serikali na Wananchi kwa ujumla kufanikisha na hasa kuvuka lengo la uandikishaji wa watoto kwa Darasa la Kwanza, ujenzi wa madarasa, nyumba za Walimu na vyoo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa tahadhari ifuatayo hasa kwa vile Mpango huo ni mkubwa na wenye kutumia fedha nyingi sana: -

(a) Mpango wa MMEM siyo mpango wa Tanzania peke yake bali ni mpango wa Dunia, uliobuniwa katika Mkutano wa Elimu wa Dunia uliofanyika huko Jomtien, Thailand, mwaka 1990. Mkutano huo haukuzungumzia tu Mpango wa Elimu ya Msingi, bali Mpango wa Elimu kwa Wote, yaani *Education for All (EFA)*, ifikapo mwaka 2000. Mwaka 2000 Mkutano kama huo ulipofanyika tena Dakar, ulibaini kuwa lengo hilo halitaweza kufikiwa na kuweka tena mwaka 2015. Hivyo basi, si vema Tanzania tukabweteka na kuridhika na mafanikio tuliyopata katika MMEM, ambayo ni sehemu ndogo sana ya malengo ya *EFA* kama yalivyowekwa Jomtien...

(Hapa microphone aliyokuwa anatumia msemaji ilidondoka chini)

WABUNGE FULANI: Aaah!

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA - MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Kuna mchawi hapa! (*Kicheko*)

Hatimaye katika mkutano wa Durban 1998 na Dakar mwaka 2000. Mkutano wa Mawaziri wa Elimu wa Nchi za Afrika (*MINEDAF VIII*), ambao kwa bahati nzuri Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Pius Ng'wandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, uliofanyika Dar es Salaam, ulipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Mpango wa *EFA* na kudhihirisha kuwa tunahitaji kufanya kazi ya ziada iwapo tunahitaji kufikia malengo ya *EFA*. Ndiyo maana tunapoisukuma Serikali, wengi wasiopenda kutafakari ukweli wanafikiria Kambi ya Upinzani tunapinga tu, lakini ieleteweke tunasukuma sana kwa lengo la kupata mafanikio ya kweli kufuatana na ahadi tulizojiwekea kama sehemu ya Jumuia ya Mataifa. Bado tuna safari ndefu kufikia malengo hayo.

(b) Taarifa iliyotolewa katika Mkutano wa Mawaziri wa Elimu wa Afrika (*MINEDAF VIII*), niliousema hapo juu na Mkutano wa Kuanzisha Umoja wa Wabunge wa Afrika (*FAPED*), uliofanyika pia Dar es Salaam tarehe 26 Novemba hadi tarehe 2 Desemba 2003, ambao kwa bahati nzuri niliwakilisha Bunge letu, wakati mmoja na Mkutano wa Mawaziri wa Elimu ulipewa taarifa ya vigezo mbalimbali vya *EFA* na mafanikio au mapungufu ya kila nchi.

Taarifa ya *UNESCO* inaonyesha kuwa, Tanzania tumefikia hatua nzuri katika kuandikisha watoto wa kike na wa kiume kwa uwiano wa 1:1. Lakini kadri ngazi ya elimu inavyopanda, Tanzania ni mionganii mwa nchi 43 ambazo kama hatua madhubuti haitachukuliwa, haitafikia lengo la kufikisha uwiano huo kwa Elimu ya Juu na hasa Vyuo Vikuu ifikapo 2015. Aidha, Tanzania inaongoza kuwa na idadi kubwa ya watoto wanaorudia madarasa na hasa katika ngazi ya darasa la 3 na la 4, mambo ambayo siyo tu yanachukua kiwango kikubwa da bajeti, lakini pia kurudia kunachukua nafasi nyingi za watoto ambao vinginevyo wangeweza kupata nafasi ya kusoma. Aidha, Tanzania imepitwa na nchi kama Somalia, Niger, Mali, Msumbiji na Angola, kwa Elimu ya Sekondari, Elimu ya Walemaru na Elimu ya Watu Wazima, jambo ambalo linasikitisha, kwani Tanzania ambayo ina amani, utulivu na mshikamano inapitwa na nchi hizo ambazo historia zake zinajulikana. Hizi si taarifa nzuri, lakini ndio ukweli na ni lazima tufanye kila jitihada na ikiwezekana tukimbiwe wakati wenzetu wanatembea, kama Mwalimu alivyotuasa huko nyuma na wakati huo huo, badala ya kuimba kwa mdomo tugeuze mshikamano, amani na utulivu wetu kuwa mtaji wa kujivunia. (*Makofi*)

(c) Ni kwa msingi huo basi, Kambi ya Upinzani imetafakari kwa kina Hotuba ya Waziri ya Mwaka 2002/2003 na hasa ya mwaka huu wa 2003/2004, Hotuba ambayo Wabunge wote wa CCM walisema ni nzuri na wakaiunga mkono kwa asilimia 100. Kwa bahati mbaya Hotuba hiyo haikugusia chochote kuhusu Mpango wa *EFA* na hatua zinazochukuliwa na Tanzania, ikizingatiwa kuwa Wizara yake ndiyo hasa inayosimamia na kutekeleza mipango ya Elimu, katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ufundji. Vivyo hivyo, Wizara haina mpango wowote wa kutekeleza mpango wa *EFA* katika

Bajeti ya Mwaka 2003/2004 na wala Wizara ya Elimu nayo pia haikutenga mafungu kwa ajili hiyo. Hii tunaona kama ni upungufu mkubwa na unahitaji kurekebishiwa mara moja ili angalau tukaribie hata kama hatutafikia malengo ya *EFA* kwa mwaka 2015. Tuanze kuchukua hatua, vinginevyo 2015 itatukuta hatujapiga hatua, kama 2000 ilivyotukuta baada ya Azimio la Jomtien. (*Makofi*)

(d) Mheshimiwa Waziri, anazungumzia kwa kina juu ya idadi ya madarasa yaliyojengwa, nyumba za Walimu, vyoo, vitabu na mafunzo kwa Kamati za Shule. Ni vema, Wizara ikafanya sasa tathmini ya kina kuhusu ubora wa madarasa, nyumba za Walimu na vyoo vilivyojengwa. Tunatoa hoja hiyo, ikizingatiwa kuwa Mkataba kati ya Serikali na Benki ya Dunia ulizungumzia kutoa kiwango cha Dola 4 kwa darasa, jambo ambalo kwa kukosa mwongozo katika sehemu nyingi haikutekelezwa hivyo, hasa kutokana na Wananchi kujenga madarasa mengi zaidi kuliko yaliyotakiwa na hivyo fedha hizo kutawanywa kwa madarasa na nyumba nyingi zaidi kuliko iliyotakiwa. Hali hii imesababisha nyumba na madarasa mengi kuwa chini ya kiwango cha ubora unaotakiwa.

Kwa vile fedha zinazotumika kwa ujenzi huo sehemu kubwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, mathalan mwaka huu tunategemea kutumia Shilingi 104.3 bilioni ambapo kati ya hizo fedha za ndani ni Shilingi 30 milioni tu ambazo ni asilimia 0.029 na zilizobaki zote yaani Sh.104,337,638,900/= ni mkopo kutoka Benki ya Dunia kupitia *IDA*, ambazo ni asilimia 99.97 na kati ya hizo Shilingi 63.9 bilioni ni kwa ajili ya ujenzi uliotajwa hapo juu. Hizi fedha ni nyingi na watakaolipa ni wajukuu na vitukuu vyetu. Hivyo, ni budi waelewe wazi kwamba, mikopo watakayolipa wakati ujao ni dhahiri ilifanya kazi ambayo matunda yake yataonekana. Hivyo, ni lazima yawe majengo ya kudumu na ya kufaa kwa muda mrefu. Kutokufanya yaliyoelezwa hapo juu, yanaweza kuleta matatizo baadaye, hasa kwetu sisi viongozi wa leo kama inavyotokea katika nchi mbalimbali duniani. (*Makofi*)

(e) Tuna taarifa kuwa fedha zaidi ya Shilingi 1.38 bilioni zilizotolewa kwa ajili ya kujenga uwezo wa Kamati ya Shule, yaani kwa mafunzo ya wajumbe wa Kamati za Shule, katika Shule nyingi na katika Halmashauri nyingi hazijaanza kutumika, japo fedha hizo zilitumwa katika mwaka wa fedha 2001/2002. Kutokufanya kwa mafunzo hayo kumeathiri kwa kiasi kikubwa utendaji kwa kukosekana mwongozo maalum kutoka Taifa kwa Kamati hizo. Aidha, kuna taarifa kuwa ndani ya muda wa mwaka mmoja, kumetolewa nyaraka 14 (*circulars*), wastani wa waraka mmoja kila mwezi, kuhusu namna ya kuchagua Kamati za Shule. Hali hii imewachanganya Wananchi kwa kiwango kikubwa na sehemu nyingine uchaguzi umepaswa kufanya kazi ya mara tatu kutokana na mabadiliko yaliyotokana na nyaraka hizo. Ni vema siku zijazo, maandalizi yakafanya mapema kabla ya kuanzisha mpango mkubwa kama huu na hii ni kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI. Tusipende kufanya majoribio katika mambo yanayowahusu Wananchi kwani athari zake ni kubwa na huchochea Wananchi kukosa imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ni wakati muafaka Waziri akaeleza bayana mbele ya Bunge lako Tukufu, jinsi na taratibu zifaazo kupata hawa Wajumbe wa Kamati za Shule. Kambi ya Upinzani inaanmini kabisa kwamba, mkanganyiko uliopo kwa sasa waweza kuondolewa tu iwapo suala hili litawekwa wazi kwani linalenga Wananchi moja kwa moja.

(f) Katika mwaka wa fedha 2001/2002, Serikali iliahidi kutoa Dola 10 kwa ajili ya kichwa cha kila mtoto aliyeo darasani kwa mwaka. Katika fedha hizo, dola 4 zinatakiwa kupelekwa na kutumika moja kwa moja na Kamati za Shule na Dola 6 zinatakiwa kutumika na Halmashauri katika kununua vitabu kwa uwiano wa kitabu 1:3 pamoa na matunzo ya majengo, ambayo zitatolewa baada ya Kamati za Shule kupeleka mpango. Waziri ameleeza katika kitabu chake kuwa, kwa mwaka 2001/2002, zilipelekwa Sh.11 bilioni kwenye Halmashauri. Lakini taarifa tulionayo ni kuwa, kiasi kilichopokelewa hadi sasa ni chini ya Dola 6 na nimshukuru Waziri wa Elimu na Utamaduni, leo asubuhi amethibitisha hivyo, kwa mwaka 2001 hadi 2003 katika Akaunti za Shule katika sehemu mbalimbali nchin i, badala ya Dola 12 kwa miaka 3 kwa maana ya Dola 4 kwa mwaka zinazotakiwa kwenda kwenye Kamati ya Shule moja kwa moja.

Hali hii imeziweka shule nyingi katika hali ngumu, kwani Wakuu wa Shule hawaruhuswi tena kuanzisha mchango wa aina ye yeyote ile. Kamb i ya Upinzani inauliza ni kwa nini fedha hizo hazitolewi kama ilivyoainishwa katika Bajeti zilizopita na baada ya kutangazwa sana? (*Makofi*)

Tunaitaka Serikali itoe kiwango chote kinachotakiwa kwa wakati ili Kamati za Shule ziweze kutekeleza majukumu yao. Isitoshe, Dola 2 kwa mwaka, yaani kiasi cha Dola 6 kwa kila kichwa cha mtoto kwa miaka 3 iliyopangwa kutumika kwa ajili ya majengo bado haijatumika, kwani Kamati za Shule na walimu inasemakana hawajui namna ya kuandaa mpango wa miaka 3 kama ulivyo kubaliwa kwenye Mkataba wa Mkopo na *IDA* kama tulivyo taja hapo awali. Nayo taarifa ya Dola 4 kwa kila mtoto kwa kila mwaka nayo imebaki kitendawili kwa sehemu nyingi kwani Walimu Wakuu hawapewi taarifa bali hupelekewa vitabu bila kuainisha ni kiwango gani wanapaswa kupokea kufuatana na idadi ya watoto katika Shule zao. Kama tulivyoomba hapo awali, sehemu kubwa ya fedha hizi ni mkopo toka Benki ya Dunia na mwaka huu tumepanga kutumia katika mkopo huo toka Benki ya Dunia Shilingi 104.3 bilioni, kama inavyoonekana kwenye Kitabu cha Nne cha Bajeti na mkopo lazima hatimaye ulipwe. Tunasisitiza basi kuwe na uwazi katika matumizi ya fedha hizi na kila mhusika apate taarifa kamili ya kiwango au vifaa anavyotakiwa kuvipata, ili hatimaye wajukuu zetu na vitukuu wanapolipa na watakapolipa wasituite sisi babu zao tulikuwa vichwa vya Mwendawazimu, kuwalipisha mkopo ambao Taifa wala wao hawa jaufaidi. (*Makofi*)

Tumeyasema haya yote, kwa vile Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake ya 2002/2003, aliiwaomba Wabunge na ninanukuu: "Waisaidie Serikali kusimamia matumizi ya fedha hizi na kuhakikisha kuwa Halmashauri na Shule zinafuata miongozo inayotolewa na kutoa taarifa sahihi ya matumizi ya fedha". Kambi ya Upinzani tuna hakika kabisa Waheshimiwa Wabunge wako tayari kufanya kazi hiyo, lakini watamsaidia na nini iwapo hawana taarifa kamili. Ni kichekesho kuombwa kusaidia kusimamia wakati unayetakiwa kusimamia unamtegemea huyo huyo unayemsimamia kupata taarifa zako! Tuna tatizo la mfumo au huwa tunapenda kuwa na maneno matamu kwenye hotuba lakini yasiyotekelze. Wakati huo huo tunaona mambo hayaendi sawa na Wananchi sehemu mbalimbali wanapiga kelele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya, tunamtaka Mheshimiwa Waziri, aweke mazingira ya kutoa taarifa kila mara inapohitajika na tunaamini kwamba, kama taarifa zitatolewa kwa usahihi, Wabunge wote kwa pamoja watafanya kazi ya kumsaidia kwa haraka na wepesi zaidi kuliko ilivyo sasa. (*Makofi*)

Tunaishauri Serikali kwamba, iwapo kwa dhati kabisa inapenda kuwatumia Wabunge kama jicho la Serikali na ili waweze kutekeleza majukumu yao ya Kikatiba ya kuisimamia Serikali, wawezeshwe kwa kupewa taarifa zote muhimu, siyo tu ya fedha iliyopangwa kutumika, lakini hasa wajue ni kiasi gani kimetolewa, lini na kwa ajili ya nini. Tuwe na uwazi tunaozungumzia kila siku katika matendo na sio kinadharia. Pamoja na kwamba taarifa hizo huwa zinawekwa kwenye magazeti, lakini siyo za kina.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya *Public Finance Act, 2001* na *Public Procurement Act, 2002*. Wakati huo Bunge lako liliahidiwa kuwa Serikali iko kwenye mpango wa kuleta Bungeni Muswada wa *Local Authority Procurement Act*, ili kuhuisha utaratibu wa manunuza katika nchi yetu, kama hatua muhimu ya kuzuia ubadhirifu, rushwa, manunuza hewa na kuweka nidhamu ya hali ya juu ya matumizi ya fedha kwa vyombo vyote vya Serikali. Kwa Bahati mbaya, jambo hilo halijatendeka hadi leo na katika hotuba yake ya 2002/2003, Mheshimiwa Waziri, alizungumzia tu *Local Authority Procurement Manual*. Hotuba ya leo haikugusia chochote!

Kama tunavyofahamu, *manual* inatumika vizuri zaidi palipo na Sheria bayana. Lakini hata hivyo, hiyo *manual* hajulikani kama imetengenezwa ama vipi na wala Mheshimiwa Waziri hazungumzii tena juu ya *manual* hiyo katika Bajeti ya 2003/2004, kumetokea nini? Wakati kila siku kila kona ya nchi kuna kelele za ubadhirifu, wizi wa mali ya umma, manunuza hewa, lakini Serikali inashindwa kuchukua hatua ya haraka katika jambo zito kama hilo! Ulaguzi wa kila mwaka wa *CAG* unaonyesha jinsi mabilioni ya fedha yanavyotumika kwa njia hizo, fedha ambazo zingegelekezwa katika matumizi muhimu zingetusaidia sana, mathalan Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, ambako Daktari wa Wilaya alitoa tenda yenye thamani ya Sh.4,824,177/= kwa Kampuni ya *Stationary* na hata hivyo kazi ya ukarabati haikufanyika kama ilivyopangwa na wala hakuna hatua ya makusudi iliyochukuliwa kumdhhibitit mtu kama huyo, huu ni mfano tu. Wananchi wanajua hali hiyo, wamelalamika na kilio chao kimeangukia kwenye masikio yaliyoziba. Tenda za aina hiyo kwa Kyela tu zilikuwa Sh.21,223,593/= (Tazama taarifa ya *CAG*). (*Makofi*)

Kanuni zilizotolewa hivi karibuni katika *GN 49* ya 2003, imetoa maelekezo yanayopingana na azma nzima ya Serikali ya Uwazi. Marekebisho ya kifungu cha 75(1) kwa mfano, yanamtaka sasa Diwani

kutoa taarifa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kabla ya kutembelea mradi ulioko katika eneo lake, akieleza sababu ya kutaka kutembelea mradi huo. Kambi ya Upinzani tunaona hii inapingana kabisa na dhana nzima ya Wananchi kusimamia maendeleo katika maeneo yao kupitia Wawakilishi wao, pia na dhana ya Maboresho ya Serikali za Mitaa yanayoendeshwa nchi nzima kwa gharama kubwa sana.

Kanuni hizo zimewafanya Madiwani wasiwe tena Wajumbe wa *Tender Board*, tunaipongeza hatua hiyo, lakini tungependa mambo kama hayo yajulikane yasifanyike kimya kimya na ni vema Waziri akalieleza Bunge lako Tukufu, kuhusu nia na malengo ya utaratibu huu na kuwa sasa udhibiti utafanyika vipi na kuna *Check and Balance* gani zimewekwa ili kuondokana na matatizo yanayoendelea kujitokeza, kama hayo tuliyyotaja ya kifedha, kwani Watendaji peke yao wakiwa kwenye *Tender Board* hawawezi kudhibitiwa na Baraza la Madiwani. Hivyo basi, ni budi kuwepo na taarifa ili uwezo kamili wa kuwadhibiti ueleweke. Tulitegemea Kanuni zitaainisha kuwa badala ya Watendaji tu kuwa Wajumbe wa *Tender Board*, basi wangekuwepo Wajumbe wengine kutoka nje ya Halmashauri kwa ajili ya *Check and Balance*. Bila mfumo kamili tusitegemee kuwa na badiliko la aina ye yote ile. Ni imani yetu kuwa, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake atatoa ufafanuzi wa kina wa jambo hili na kurekebisha dosari zinazoweza kusababishwa na Kanuni hii na kuondoa hisia zilizokwishajengeka kuwa Serikali inawalinda Watendaji wabadhirifu.

Mheshimiwa Spika, sasa ninapenda kwa kifupi n'igusie suala la TUMITAA. Siku za hivi karibuni kumekuwa na malamiko mengi kutoka kwa Madiwani wa Halmashauri mbalimbali, kuhusu Watendaji na jinsi malalamiko yao yanavyoshughulikiwa. Malalamiko hayo yametokea kwenye Halmashauri tofauti zikiwemo Manispaa kama Morogoro, Korogwe, Arumeru, Karatu, Songea na kadha wa kadha. Mgogoro mara nyangi unatokana na Madiwani kulalamikia utendaji kazi mbovu, matumizi mabaya ya fedha za Halmashauri, ubadhirifu na kadhalika.

Kambi ya Upinzani inadhani malalamiko hayo yatazidi kuongezeka jinsi Madiwani wenye kujuwa wajibu wao watakavyoongezeka. Hivyo, ni muhimu Serikali ikachukua hatua za haraka kutafuta msingi wa matatizo hayo na isitoe majibu ya haraka haraka kama vile kusema: "Madiwani wasiingie jikoni", "Madiwani wawaachie Watendaji kufanya kazi zao" na kadhalika. Sisi tunaamini kuwa, inawezekana kabisa panapofuka moshi pana moto. Haiwezekani Madiwani wapige kelele kama hakuna dalili za matatizo. Tunavyofahamu sisi kazi ya Madiwani ni kusimamia Utendaji wa Watendaji na siyo Kusimamia Watendaji. Mtu asipoelewa tofauti kati ya hayo mawili ataendelea kusema kuwa Madiwani wanaingilia.

Kazi ya kusimamia utendaji, tunaamini inakwenda ndani kuona jinsi Watendaji hao wanavyotekeleza mipango iliyopangwa, kutumia fedha zilivyokubaliwa kwenye vikao, kutekeleza maazimio ya vikao na kadhalika. Lakini kuwasimamia Watendaji ni pamoja na kupanga ratiba zao za kazi, wajibu ambaa ni wa Mkurugenzi na wala si wa Madiwani. Ni muhimu basi, majukumu ya Watendaji yaainishwe bayana na vivyo hivyo kwa majukumu ya Madiwani katika kusimamia shughuli za Halmashauri. Vingenevyo kuna hatari kuwa hatua kubwa tuliypiga kwa kutunga Sheria ya Manunuzi ya 2001 na ya Fedha 2001, zitapoteza maana katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya, Manispa na Miji, jambo ambalo ni hatari kuwa na *Double Standards* katika Vyombo nya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, ni njia moja ya uhakika ya kuzisaidia Serikali za Mitaa kuondokana na ukosefu wa mitaji. Mwaka 2001/2002, Mheshimiwa Waziri alieleza kwa kirefu hatua anazozichukua kuimarisha Mfuko huu. Mheshimiwa Waziri, alibainisha matatizo makubwa ya Mfuko kuwa ni mtaji mdogo, mwamko mdogo wa Viongozi na Watendaji katika ngazi ya Wilaya kuutumia Mfuko huo, ikiwa ni pamoja na kuwataka Watendaji wahakikishe mikopo inarudishwa kwa wakati. Tunaungana na Mheshimiwa Waziri katika wito huo.

Hata hivyo, Kambi ya Upinzani imesikitishwa kuwa pamoja na kutumia fedha nyangi kupitia msaada wa Serikali ya Denmark kuainisha matatizo ya Mfuko huo, Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004, imetenga kiasi cha Sh. 400 milioni tu kwa ajili ya Mfuko huo, wakati katika Fungu 56 Wizara kwa mfano, imetenga kiasi cha Sh. 300 milioni kwa ajili ya viburudisho/takrima ya Serikali, samani, mambo ambayo karibu kila mwaka yanajirudia rudia na malipo ya masaa ya ziada. Ni dhahiri kuwa vipaumbele vyetu haviko kwenye maeneo yenye tija au kama kuna tija basi ni ndogo sana. Tunaitaka Serikali kuuwezesha Mfuko huo na kuupatia mtaji wa kutosha ili uwe ukombozi kwa Halmashauri, kama

Mheshimiwa Waziri alivyosema, unafikiriwa kubadilishwa kuwa ama Benki au utaratibu mwingine, basi uandaliwe mapema. (*Makofii*)

Tukumbuke kuwa kitu unachokitolea jasho utakijali zaidi kuliko cha kupewa, hivyo, ruzuku haijengi uwajibikaji bali utegemezi na tunaitaka Serikali iwe na mipango ya kuziwezesha Halmashauri kuwa na uwajibikaji mkubwa katika mipango na miradi yake. Mfuko huu ni njia moja ya uhakika ya kuhimiza uwajibikaji huo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa uliundwa kwa lengo la kuwalipa mafao Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa pale utumishi wao unapokoma. Mapato ya Mfuko yanatokana na michango ya Wanachama pamoja na fedha iliyowekezwa kwenye vitega uchumi mbalimbali. Mwaka 2002 Mfuko ulikusanya jumla ya Sh.31.7 bilioni, sawa na asilimia 93.3. Hiki ni kiwango kikubwa na cha kuridhisha. Katika kipindi hicho kiasi cha Shilingi 26.2 bilioni zilitumika kwa kuwekeza katika vitega uchumi mbalimbali, ikiwemo amana za Serikali, amana za mabenki, ununuzi wa hisa za Makampuni, ujenzi na ukarabati wa nyumba. Lakini katika kipindi hicho hicho ni kiasi cha Sh.222,187,249.10 tu ndizo zilizotumika kulipa mafao kwa Wanachama 1,205. Kwa bahati mbaya, bado kuna malalamiko kutoka kwa baadhi ya Wanachama kuwa wanapata usumbufu mkubwa katika kufuatilia mafao yao na isitoshe yanachelewa sana.

Lakini vile vile, tunaamini kuwa Mfuko huu ni lazima uende na wakati katika kuboresha mafao yake mara kwa mara na uweke vivutio vipyta ikiwa ni pamoja na kuhudumia wagonjwa, *maternity*, mazishi, pamoja na matatizo mbalimbali kama ilivyo kwa Mifuko mingine kama vile *NSSF*. Ikiwa ni lazima Sheria zilizounda Mfuko zipitiwe upya ili kuruhusu mfuko kuangalia aina nyingine ya mafao kwa Wanachama wake. Mfuko usilenge kupata faida kubwa tu kwa kuwekeza katika vitega uchumi vinavyochukua muda mrefu kupevuka na badala yake kadri Mfuko unavyokua uwekeze zaidi katika maslahi ya Wanachama wake. (*Makofii*)

Mwaka 2002/2003, Waziri alikiri kuwa taarifa kamili ya Hesabu yaani *Statements* za mwaka 1997/98, zilipelekwa katika Halmashauri 66 tu. Ni imani yetu kuwa mwaka huu Mfuko utapeleka taarifa kamili kwa Halmashauri zote na kwa wakati muafaka na atatolea taarifa jambo hilo, ili Wanachama wote wawe na haki ya kujua mahesabu yao kwa wakati na hivyo kupanga maisha yao pale inapohitajika. (*Makofii*)

Aidha, wakati Mfuko ulikuwa unatoa riba ya asilimia 12 mwaka 2000/2001, ulipanga kutoa riba ya Asilimia 10 tu 2002/2003, kutokana na kushuka kwa riba katika vitega uchumi. Tunataka Mfuko uwe na riba *fixed*, inayojulikana ili Mwanachama awe na maisha ya uhakika kuliko kubahatisha kutokana na kupanda au kushuka kwa riba katika soko. Mfuko unaweza kabisa kwa kiasi hicho cha mapato kuweka kiwango maalum ili kisibadilike badilike ghafla na hivyo kuathiri maisha ya Wastaafu wetu. Pamoja na hayo, kama riba itakuwa *fixed* watendaji wake watakuwa wabunifu, waangalifu, wachambuzi kwani uzembe ndio unawalazimisha kushusha riba, badala ya kufikiria namna ya kumnufaisha Mwananchama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili Sheria Na. 6 ya mwaka 1999, Waziri wa TAMISEMI wa wakati ule, alisema kuwa: "Utaratibu wa kuwa na Katibu Tarafa chini ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya utakuwa wa muda tu." Ni imani ya Kambi ya Upinzani kuwa miaka mitano inatosha kabisa kupata uzoefu na hivyo hadi sasa tumeshaona manufaa na matatizo ya kuwa na Makatibu Tarafa chini ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya. Makatibu Tarafa wako zaidi ya 500 katika nchi yetu na wanalipwa mshahara wa ngazi ya juu Wilayani. Lakini kwa bahati mbaya, Makatibu Tarafa hawana vikao vya kisheria katika maeneo yao yanayowawezesha kufanya maamuzi ya kisheria na wala hawana Vyombo vinavyoweza kuwapa ushauri wa kisheria kama ilivyo kwa *WDC*.

Kambi ya Upinzani kwa mara nyingine inashauri tena kuwa, Serikali ilete mara moja Bungeni marekebisho ya Sheria Na. 6 ya mwaka 1999 ili Makatibu Tarafa wawe Wasaidizi Wakuu wa Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya katika ngazi ya Tarafa na wawe na majukumu ya kuratibu shughuli za maendeleo katika ngazi ya Tarafa. Kwa utaratibu huo Makatibu Tarafa watatumika vizuri zaidi na tutakuwa tumepeleka uratibu wa shughuli za maendeleo karibu zaidi na Wananchi hasa katika kipindi hiki ambapo

tunapaswa kuelekeza nguvu zetu zote katika kupiga vita adui umaskini. Kuwataka Makatibu Tarafa washiriki kwenye vikao nya Ha l mashauri kwa njia ya *Circular* au Waraka haina tija, kwani kwa sasa hivi Makatibu Tarafa hawawajibiki kwa Mkurugenzi Mtendaji na wala kisheria hawatoi taarifa zao kwa Mkurugenzi Mtendaji. Tunatumaini kuwa Mheshimiwa Waziri, ataleta Bungeni mapema iwezekanavyo, marekebisho ya Sheria hiyo, ikiwa ni pamoja na majukumu, uwajibikaji na taratibu za kazi katika ngazi ya Tarafa na hivyo kuondoa utata ulioko sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusikiliza kilio cha Waheshimiwa Wabunge, kilichotolewa mwaka wa 2001, kuhusu Ajira ya Watendaji wa Vijiji. Hata hivyo, tunaitaka TAMISEMI iandae utaratibu mzuri wa ajira kwa Watendaji hao. Tunasisitiza kuwa Waziri alete Bungeni Sheria au Marekebisho ya Sheria ya 1982 ya Serikali za Mitaa itakayotumiwa na Watendaji hao muhimu na ambao kwa kweli ndio sura halisi ya Serikali, ili tuondokane na tatizo la kuwa na Miungu Watu na majukumu na mipaka ya kazi yao ioanishwe kabisa ndani ya Sheria kama ilivyo kwa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji, ikiwa ni pamoja na wajibu wao kama Walinzi wa Amani, ambao kwa miaka nenda rudi wameutekeleza bila kuwa na Sheria wala mwongozo mahsus. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kila Mtanzania amefurahishwa na ahadi za Serikali kupitia Bajeti ya mwaka huu has a kuhusu Mfuko wa Pembejeo, mpango wa Zao la Biashara na Chakula kwa kila Wilaya, ikiwa ni pamoja na kufuta kodi mbali mbali ambazo ni kero kwa Wananchi. Pamoja na hali hiyo, Kambi ya Upinzani imestushwa kuwa mipango hiyo mizuri inaelekeha haikufanyiwa maandalizi ya kina, ila imechomekwa dakika za mwisho katika hotuba ya Waziri wa Fedha kama inavyoonekana kwenye Hotuba ya Waziri wa Fedha, ukurasa wa 68 ambapo kipengele cha kufuta Kodi ya Maendeleo kimechomekwa kwa kubandika kijikaratasi juu ya maandishi yaliyokuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na dosari hiyo, tumestushwa kwa vile baada ya kupitia kasma zote za TAMISEMI na Mikoa, haionekani mahali popote Serikali imeweka utaratibu gani mahsus kufidia pengo hilo. Ni wazi sababu inaeleweka kwani ilitumbukizwa dakika ya mwisho. Tunamtaka Waziri wakati wa ufanuzi alihakikishie Bunge lako Tukufu, ni kasma ipi itatutumika kutoa ruzuku hiyo na kwa vigezo gani kwa Halmashauri mbalimbali za Manispa, Jiji, Wilaya na Vijiji, hasa ikizingatiwa kuwa jambo hilo halikuwepo katika maelekezo ya awali ya Wizara yaliyopelekwa kwenye Halmashauri katika kuanda bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, tumeptia vipengele vyote nya ruzuku nya Fungu 56, ambayo ndiyo inayotumika kupeleka ruzuku katika Halmashauri na hatukuona mahali popote panapotoa au kuonyesha mafungu kwa ajili ya Mfuko wa wafugaji wadogo, wavuvi wadogo, wenye viwanda wadogo na wafanyabiashara wadogo, tutaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie katika ufanuzi wakati wa majibu yake. Vivyo hivyo, kwa ruzuku ya Zao la Biashara na Chakula, hatukuona mahali popote isipokuwa kwenye Wizara ya Kilimo *Subvote 1003* nayo pia hazikuanishwa isipokuwa zimetengwa Shilingi 4 bilioni tu ambazo tunafikiri ndipo zilipowekwa, tunadhani kwa malengo yaliyokusudiwa ni fedha kidogo sana, ambazo ukigawa kwa Wilaya zilizoko ni wastani wa Shilingi 33 milioni tu kwa kila Wilaya. Tungependa Waziri atupe ufanuzi kama fedha hizo zinapitia kwake au kwa Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ukurasa wa 7 alieleza kuwa mwaka 2002/2003, Mikoa pamoja na Halmashauri zilitengewa jumla ya Shilingi 35.6 bilioni kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Lakini, hadi kufikia Mei, 2003 zilipatikana tu jumla ya Shilingi 8.8 bilioni sawa na asilimia 24.7 ya fedha zote zilizotengwa na kati ya hizo, fedha za ndani ni Shilingi 7.1 bilioni sawa na asilimia 20.10 na fedha za nje ni Shilingi 1.6 bilioni sawa na asilimia 4.63 tu. Mwelekeo huu ni wa hatari sana kwa maendeleo ya nchi. Kambi ya Upinzani inatoa tahadhari, isije hata mwaka huu, ambapo pia tumetenga Shilingi 35.4 bilioni na kati ya hizo Shilingi 25.6 bilioni fedha ya nje, furaha yote ya Watanzania ikaishia kwenye Hotuba nzuri, lakini utekelezaji ukawa kitu kingine kabisa kama zilivyoonyesha Hotuba zote kwenye *Hansard* toka mwaka 1966 hadi 2002/2003, hasa ikizingatiwa kuwa Bajeti yetu ni tegemezi kwa asilimia 45. Ni wakati muafaka sasa Waheshimiwa Wabunge, tukaacha kushangilia uzuri wa Hotuba, badala ya uzuri wa Bajeti yenye. (*Makofii*)

Tathmini inaonyesha kwamba, kuanzia mwaka 1966 ...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA - MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, hatutaunga mkono hoja mpaka tutakapopata majibu. (*Makofii*)

SPIKA: Kwa kuwa muda wa kusema unajulikana na uko kwenye kanuni, nawashauri Wasemadi wa Upinzani watakaofuata, wapange hotuba zao ziishie katika dakika zilizowekwa, si vizuri kukatis hwa namna hii.

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutoa shukrani zangu kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu wake, Katibu Mkuu na Wataalam wao wote kwa kuweza kutengeneza Bajeti nzuri, ambayo inavutia sana na imejaribu kutatua matatizo mengi ambayo yanatukabili katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijachangia, nina mambo kama matatu ambayo ningependa kuyatilia mkazo. Kwanza, ni suala la kusamehewa Kodi ya Maendeleo, pamoja na kodi nyingine. Suala hili wengi tumelizungumzia na tunaliafiki. Halmashauri nyingi zilikuwa zinategemea kodi hizo, kwa hiyo, naomba sana kama kuna fungu ambalo limetolewa liweze kuharakishwa ili liende katika Wilaya na ziweze kufanya mambo ya maendeleo. Kwa sababu sasa hivi hakuna mtu ambaye anaweza kulipa kodi na wala hawesi tena kwenda porini kujificha baada ya kusikia kwamba amesamehewa kodi. Vile vile, napendekeza kwamba, wakati wa kutuma fungu hilo (fedha ambazo zinatokana na makisio ya kodi) ni lazima Wizara izitolee maelekezo, la sivyo fedha hizo zitakwenda kwenye Mfuko mmoja ambao ni wa kinyama kabisa unaoitwa *GIF*. *GIF* ni matumizi ya kawaida kabisa na wala si ya maendeleo, kwa hiyo, kama hamtaelekeza kwa kikamilifu kabisa kwamba asilimia fulani iwe ni ya kimaendeleo, watafanya fedha zote za kodi *ziwe* ni za matumizi ya kawaida tu. Kwa hiyo, naomba watenge sehemu ya maendeleo na sehemu ya matumizi ya kawaida katika fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji. Ninaishukuru sana Serikali Kuu kwa kuchukua tena mzigo huo mzito, ila naomba tu kabla hamjachukua huo mzigo, kuna madeni mengi sana ambayo wale Watumishi walikuwa wanaidai Halmashauri, mtoe maelekezo, la sivyo kuchukuliwa kwa Serikali Kuu, basi itazika yale madai yao. Kwa hiyo, muwe wazi kabisa katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo napenda kuliongelea na ambalo ni zito ni kwamba, tarehe 28 Julai, 2002 katika jumba hili (Ukumbi wa Bunge) kulikuwa maelezo binafsi ya mwenzetu Mheshimiwa Paschal Degera, kuhusu mgogoro uliotokea kati ya Kijiji cha Itolwa na Kijiji cha Katikati. Kijiji cha Itolwa kiko Kondoa na Katikati kiko Kiteto. Mwenzetu alielezea sana kwamba, Kondoa wamenyanyaswa na nilimsikiliza na ni karibu mwaka mzima sasa, maana ilikuwa ni mwezi wa saba mwaka 2002. Alielezea mgogoro huo kwa uchungu mkubwa sana, lakini nilinyamaza. Uvamizi huo uliotokea tarehe 5 na 6 Novemba, 2002 uliotokea katika Kijiji cha Itolwa Kondoa, ni siku ambayo wafugaji wote wa siku hiyo wanapeleka mifugo yao kwenda kunywesha pale. Ng'ombe wengi sana karibu 1,789 siku hiyo walikuwa wanakunywa maji, wakavamiwa na watu wa Vijiji viwili vyia Itolwa pamoja na Mlongia. Walivamiwa na watu karibu 3,000 na jamii ya kifugaji haikuwa na hisia kwamba siku hiyo watavamiwa wakiwa na mbuzi wao pamoja na kondoo.

Mheshimiwa Spika, siku hiyo walipovamiwa Wanawake walibakwa, wakawekewa michanga katika sehemu zao za siri na wengine walifariki. Siku hiyo ng'ombe walitoroka wote wakasambaa, ng'ombe 1,700, mbuzi zaidi ya 2,000, kondoo, punda na kadhalika na watu wakaona kabisa mambo hayo. Wale ng'ombe baadaye walirudi, japo wachache, walibaki ng'ombe karibu mia tisa na kitu. Kesho yake Serikali ikaingilia suala hilo. Serikali ilishughulikia tatizo hili kwa kina kabisa na katika jambo ambalo Serikali imeunda Vyombo na imefanya kazi kwa makini ni katika suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu tunaposema kwamba mafahali wawili wakipigana ziumiazo ni nyasi, ni ukweli. Hii fidia tunayoizungumzia ni kifuta jasho tu, ni suala la ng'ombe tu maana kulikuwa kuna upotevu wa mali, mazao pamoja na fedha taslim karibu Sh.6,000,000/= na maboma 25 yalichomwa moto yote. Sasa, siku ile Mheshimiwa Degera, alipokuwa anatoa hii hoja watu walishangilia sana, wakifikiri kwamba ni Serikali ilisema toa hii kitu kidogo. Leo wale wa Kijiji cha Katikati wanatembea na vikombe kuomba maziwa baada ya kupotelewa na mali zao zote. Kamati za Ulinzi na Usalama kwa Mikoa ya Arusha na Dodoma wamekaa, wakajiuliza tutafanya nini kwa wale walionyanyaswa? Sasa, tangu wakati ule wametoa Shilingi 20 milioni, bado Shilingi 48.6 milioni. Kwa vile mafahali walikuwa wanapigana, wameacha sasa majani yanaungua mwaka mzima. Watu wanatembea na vikombe tu wanasubiri Serikali.

Napenda kusema kwamba, nawaombeni sana, katika suala hili kama Kondoa wameshindwa kutoa hicho kifuta machozi na Serikali Kuu imeshindwa kutoa hiki kifuta machozi, waambieni wale tumeshindwa, siyo hiyo tu wamerudia mwaka jana, mwaka huu tena wamepiga wameua kijana mmoja, wakachoma tena maboma, uzikumbuke katika zile shilingi milioni 20 kuna kijana aliuawa, ilibidi tutenge hela kidogo. Kuuawa kwake ilikuwa katika zile purukushani, ni risasi zilizomuua. Kama polisi wamefyatua au zimefyatuka lakini ni risasi.

Kwa hiyo, naomba sana Serikali isiwfanye watu wakagombanishwa halafu baadaye wakasema hii jamii ni korofi. Naishukuru sana Serikali kwa kujibu ile kauli yake. Lakini kuna masuala ambayo Serikali imeamua hivyo.

La mwisho kwa dakika tatu ni suala la mpaka. Mimi sitaki kugusia suala la mpaka. Lakini ukuraswa wa 11 katika hotuba ya Waziri imegusia suala la mpaka. Nataka niseme wazi Serikali isiwe mbabaishaji kuweka mipaka 4, 5 katika eneo moja. Leo mpaka uko hapa, kesho mpaka uko pale, keshokutwa mpaka pale. Lakini tumegundua kwamba Serikali imebadilisha *GN* ya mwaka 1961, ambayo ndiyo ilikuwa imebadilisha na imesema hapa tunarekebisha. Hivi unaporekebisha *GN* bila ridhaa ya wananchi, bila ridhaa ya viongozi na huendi kuwaelezea kwamba nimebadilisha ni haki hii? Wanajua wao kabisa kwamba *GN* wanayofuata ni tangu ile ya wakoloni, leo unakaa unabadilisha unakwenda kupima, unatarajia nini? Unafikiri wale wananchi ni wajinga pamoja na viongozi wao? Hebu kama umerekebisha utuite basi tuambie hiyo *notes* ya Serikali ya 65 umeefanya na nani? Au siku hizi mna mamlaka Serikali na Rais anajua kabisa kwamba mna mamlaka basi Rais wetu atutangazie nimefanya mabadiliko atuambie kwamba, wananchi nachukua vijiji fulani nya Mwitikira, Oboloti, Kiperisa, Mashiga, Kondoa, watangazieni wananchi wazi wazi kuwa mabadiliko hayo mmeefanya, kwamba *GN* Kondoa tumeshatengeneza. Jamani kama ninyi ni mafahali huko Kondoa mnafanya hivyo sisi ni nyasi! Kama mnafanya hivyo kwa matakwa ya Kondoa, tunafuata *GN* mliyotengeneza mtuambie sisi hatuna ugomvi na Kiteto, lakini muwe wazi na Rais aelewé hayo, halafu nendeni mkawatangazie watu kwamba mmebadilisha. Leo wanasubiri mipaka mnachora kumbe mnabadilisha *GN* hamuwezi kuwaeleza mna kigugumizi? Mnasema tu *GN* 1961 kumbe mmebadilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana kama ikiwezekana mwende mkawaambie wananchi. Hii Serikali ni yao na hii nchi ni yao. Sasa kama unataka kufanya dhuluma fanya tu na utaonekana. Nimesema haya niweze ku -register na niweke iwe katika *Hansard* ili na vizazi vijavyo viweze kusoma hayo na kauli zingine zote ambazo zimetolewa katika vikao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru basi imeisha. (*Makofi*)

MHE. ESHA H. STIMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mapema kwa siku ya leo. Pili, nimpongeze Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni, ambayo ina mwelekeo mzuri katika maendeleo ya wananchi. Pia mimi nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kutoa idhini ya mabadiliko na kufuta Kodi ya Maendeleo kwa wananchi. Kwa uhakika wananchi wamefurahia sana mabadiliko aliyoyafanya na hasa wanawake. Tumefurahi sana kwa sababu hapo mwanzo tulikuwa tunafanya kazi za maendeleo peke yetu, waume zetu walikuwa wanaogopa kama wakienda kule wanaweza wakakamatwa. (*Makofi*)

Vile vile kwenye shughuli za mbio za mwenge tulikuwa tunaonekana wanawake peke yetu na watoto, wanaume wote wanajificha kwa kuhofu hilo hilo. Hali kadhalika, wanawake tulipokuwa tunapata matatizo ya kuugua waume zetu hawakuwa tayari kutusindikiza hospitali au *clinic* kwa kuhofia suala hilo hilo la kukamatwa na badala yake tulikuwa tunasindikizwa na ndugu zetu na wifi zetu. Lakini kwa sasa hivi tumeanza kupata raha ya kuhudumiwa vizuri na waume zetu tunashukuru sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwapongeza watendaji wa Wizara hii, kwa kuiwezesha hotuba hii kuwa nzuri kwa maandalizi ambayo wamempa Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie suala zima linalohusu mabadiliko ya Madiwani kutokuwepo katika Bodi ya Zabuni. Madiwani wenzetu bado wanapata kigugumizi kulikoni haya mabadiliko? Mwanzo tulikuwa wote na watendaji katika zabuni hizo. Sasa nani amepeleka malalamiko kwa Waziri kwamba wanaomba wafanyiwe mabadiliko hayo? Kwa misingi hiyo, namwomba Waziri tena kwa upendo kabisa katika suala hili atuwasilishie maelezo hapa Bungeni ili na sisi kama Wabunge, tutakapokwenda wenzetu tuwape elimu ya kuridhisha na mabadiliko haya kuliko ilivyokuwa sasa hivi imekuwa ghafla mno hakuna maelezo yaliyotangulia kabla ya maagizo yake aliyoleta kwenye Halmashauri na Manispaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa naomba kuchangia ni kuhusu maslahi ya Waheshimiwa Madiwani. Waheshimiwa Madiwani wenzetu kwa sababu na sisi tunaingia katika vikao kama Madiwani. Sasa maslahi yao yamekuwa ni finyu sana na hivyo wanalamika maeneo mengi tu kwa sababu maagizo ya posho zao inategemea jinsi zilivyo Halmashauri na uwezo wao. Sasa kwa vile kuna mabadiliko ambayo yamejitokeza na Serikali kutoa ruzuku baada ya kufuta Kodi ya Maendeleo, mimi nilikuwa naomba kama kutakuwa na uvezekano hata kama siyo katika Bajeti hii, Bajeti ijayo posho za Waheshimiwa Madiwani, ziwe na kima kimoja kwa nchi nzima. Kwa sababu gani naomba iwe hivyo? Ikiwa itakuwa kima ni kimoja Waheshimiwa Madiwani wataweza kupata maslahi ya mikopo kama wanavyopata Waheshimiwa Wabunge. Kwa sasa hivi hawawezi kupata kwa sababu hawana nyenzo za kudhibitiwa zile posho zao. Inakuwa vigumu akipata kwenye kikao basi anatumia matumizi mengine. Lakini kama itatolewa na Serikali kuititia Halmashauri zetu, basi watakuwa na uhakika wa kuweza kukopa angalau pikipiki au kwa wale ambao wana uwezo tangu mwanzo wanaweza wakakopa hata magari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili nalizungumzia kwa sababu mara nyingi kwenye vikao vyetu Madiwani hawa wametuomba tuwasemee huku na kwa kweli haawamini kama sisi tunajali shughuli zao wanazozifanya. Kwa sababu Waheshimiwa Madiwani ndiyo wanaoandaa utulivu katika Uchaguzi wa Rais na Wabunge. Kama hawatakuwa imara, hawataridhika katika maslahi yao, wanaweza wakaacha hizo shughuli zisiende vizuri na tukajikuta chaguzi zetu zinakwenda kwa migogoro na mvutano. Kwa misingi hiyo, kitu kikubwa ambacho mimi nimeona nikizungumzie ni hicho ili wakipata walau na wao mikopo ya magari, pikipiki na uhakika wa posho, basi watakuwa na utulivu mzuri na hakutakuwa na malumbano wakati wa uchaguzi, huyu kumfanyia kejeli huyu na huyu kuwa na mvutano na mtu mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliona niseme haya. Masuala mengine ambayo yametokea kwenye hotuba ya Waziri, mimi nayaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, kwa kweli safari hii masuala yote ameyaweka katika maelekezo mazuri. Ukitosha tu hiki kitabu hakika unajua kwamba, maendeleo katika Halmashauri zetu safari hii yatakewenda vizuri na hakuna mgogoro wa aina yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile kanuni zetu zinakataza kurudiarudia yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzako, basi mimi nilikuwa na makubwa hayo mawili ambayo yanahusu maslahi ya Waheshimiwa Madiwani kuongezeka na vile vile tupate maelezo ya kutosha kuhusu mabadiliko ya kuwatoa Waheshimiwa Madiwani katika Bodi ya Zabuni katika Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Nianze kwa kukushukuru sana wewe mwenyewe

Mheshimiwa Spika, kwa umahiri wako mkubwa wa kuliongoza Bunge hili. Naomba nikwambie kwamba, mambo mengi tunajifunza kutoka kwako hasa sisi Wabunge wapya kupitia vitabu vyako unavyoviandika na makala mbalimbali, mimi huwa nasoma sana. Hata ile ya juzi nimeisoma mara nne bado nai-*admire, remembering Shakespears much do about nothing*. Napendekeza kuwa uendelee kuwa unaandika kwa sababu ni kweli Watanzania wengi na hata baadhi ya sisi Wabunge bado masuala ya *Parliamentary Procedures* yanatupa tabu na haitatusaidia sisi tu, bali yatasaidia na wengine watakaofuata baada yetu. (*Makofi*)

Pili, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanyika, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ametueleza na hotuba ambazo zimetangulia kabla yake na maendeleo makubwa ambayo yamejitokeza katika eneo la uchumi kukua, Pato la Taifa kukua, ukuzaji raslimali kuongezeka, kasi ya upandaji bei kushuka, kufuta Kodi ya Maendeleo, kufuta kodi ya mifugo na maendeleo mengi katika Wilaya yangu ambayo yanaendelea kutokea kama kujenga zahanati nyingi tumesaidiwa na Serikali na sisi wenyewe tumeshirikiana nayo, hospitali yetu ya Wilaya inazidi kubadilika kila kukicha, barabara zetu, miradi ya maji. Kwa kweli maendeleo ni makubwa na wananchi wanaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika sekta zilizokua kwa kiwango kikubwa sana iliyoongoza ni sekta ya madini na uchimbaji mawe. Hii sekta mwaka 2002 ilikua kwa asilimia 15, mwaka 2001 ilikua kwa asilimia 13.5. Lakini ukiangalia mchango wa sekta katika Pato la Taifa ni mdogo sana, ni asilimia 2.6. Sekta imekua kwa haraka sana lakini mchango wake kwenye Pato la Taifa ni kidogo sana. Sasa sababu nyingi zimekwishaelezwa na mimi sina nia ya kurudia ila ni kuendelea kusisitiza kwa Serikali kuangalia kwa undani zaidi katika sekta hii, kuona namna ambavyo ukuaji wa haraka unaweza ukachangia na kuwa na nafasi maalum katika Pato la Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Naomba nimpongeze Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza Wizara hii kubwa sana wakitoea hapa Dodoma pamoja na wasaidizi wao wote. Wanadhirisha kwamba inawezekana kufanya kazi ukiwa hapa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia na kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nitachangia mambo mawili tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni lile agizo la Serikali kwamba kila Wilaya ichague mazao mawili ya kuyawekea kipaumbele zaidi kuliko mazao mengine. Sisi wa Kanda ya Kati ni kanda yenye ukame. Kutokana na ukame huo tumekuwa na wakulima wetu ambao wengi wao ni maskini wanaotegemea kilimo cha jembe la mkono. Sasa wakulima tajiri huwa wana-*practise monoculture*, wanalima kilimo kikubwa cha *plantations*, iwe ni kahawa, chai, katani, pamba na mazao mengine. Mashamba makubwa zao moja katika mashamba yale. Lakini wakulima maskini huwa wana sifa mbili kubwa kama hawa wa kwetu wanaolima kwa jembe la mkono. Kwa lugha ya wenzetu wanasema hawa wakulima maskini ni *risky a verse* na huwa wana-*diversify* mazao. Kwa sababu ya *risk* ya kulima katika maeneo kame, mkulima anabahatisha kwa sababu anabahatisha katika eka zake mbili hana hakika mwaka huu hali ya hewa itakuwaje, anachofanya ni kwamba katika shamba hilo la eka mbili anapanda mahindi, mtama, uwele kidogo, maboga, matikiti, matango kunakuwa na bamia, alizeti, karanga, njugumawe, kunde, choroko na kadhalika. Anafanya hivyo kwa makusudi kwa sababu anajua kutokana na *experience* ya miaka mingi kwamba ukipanda zao moja mfano mahindi tu mvua isiponyesha itakuwaje? (*Makofi*)

Kwa hiyo, ndiyo huko ku-*diversify* anapanda mazao mengi kidogo kidogo ili aweze kubahatisha. Kwa hiyo, agizo lile la kusema zao moja moja sisi wananchi wa Kanda ya Kati inabidi litazamwe vizuri, ni agizo kidogo linakwenda tofauti na hali halisi ya hewa ambayo wanadamu bado hatujaweza kupambana nayo. Hata Wazungu walioendelea, wameendeleza mengine yote, lakini hali ya hewa hawajaweza kuibadilisha, wahamishe *winter* iwe ni kitu kingine. Sis i hali ya hewa ni hiyo ya ukame wa mara kwa mara lazima tu-*diversify*. Kitu muhimu tunachoiomba Serikali ni kubadilisha nyenzo wanazotumia wakulima katika kufanyia kazi ili watumie zaidi plau na matrektta. Wakianza kulima ekari nyingi zaidi watapunguza hii habari ya kuchanganyachanganya mazao mengi zaidi. Lakini kadri ambavyo watakavyoendelea kutumia jembe la mkono, kuwaambia wachague zao moja haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni suala la Makao Makuu ya Serikali, Mahakama na Bunge kuhamia Dodoma. Kuhamisha watu huwa si jambo rahisi, hata humu Bungeni, Mheshimiwa Spika ukiagiza mtani wangu Mheshimiwa Hadija Kusaga ahamie hapa nilipo na mimi nihamie pale alipo, utapata barua za malalamiko japo uhamisho huo haugharimu chochote kwa maana ya fedha na kadhalika. Hata shuleni kuwahamisha wanafunzi wa bweni moja uwapeleke bweni lingine na wale wa kule uwalete bweni lingine huwa ni ngumu. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa suala la kuhamia Dodoma ni gumu vile vile, pamoja na sababu za kiuchumi na nyininge. Kuna ile hali ya mwanadamu akiwa mahali fulani anajisikia *comfortable* kuwa pale. *Change* ni kitu ambacho huwa hakipokewi kiurahisi. Ni kweli ziko sababu hizi za gharama kubwa kuendesha Bunge Dodoma na Serikali kule Dar es Salaam, ni kweli kuwa gharama ambayo imetumika *so far* tumeambowiwa hapa jana ni shilingi bilioni 21.9 tu, hela ambayo ni chini ya barabara moja inayojangwa mahali ambapo sina haja ya kutaja. Ni kweli kuwa kuendelea kujenga nyumba za Mawaziri na nyumba za Serikali Dar es Salaam ni kwenda kinyume na *spirit* nzima ya kuhamia Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana na Taasisi yako ya Bunge kwa kuonyesha kwa vitendo kwamba, inaweza kufanya kazi Dodoma. Pia nawapongeza TAMISEMI na Wizara nyininge ambazo zimekwishahamia hadi leo. Ninachojiliza hawa wengine wanaendelea kuwa huko kwa sababu zipi hasa za msingi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi tulioitangaza ili tuweze kuja hapa Dodoma Bungeni, ukurasa wa 112 fungu 106 kuhusu kuhamia Makao Makuu Dodoma, nanukuu inasema: "Sera ya CCM ni Dodoma ndiyo Makao Makuu ya Chama na Serikali." (*Makofi*)

Sasa ni kitu cha ajabu sana kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi aliyeinadi sera hii na akachaguliwa kwenda Dodoma anakuja kulaani Dodoma, wewe umeomba kura kwa wananchi niwawakilishe Dodoma Bungeni, tunakuja hapa tunataka tuhame, hapana! Tumechaguliwa tuje tuwe Wabunge tuwawakilishe wananchi Dodoma. Kwa kuwa ni Ilani yetu na ni Sera yetu, wajibu wetu Wabunge Kikatiba ni kuisimamia Serikali na kuishauri ili itekeleze Ilani yake. Tunatakiwa kuisimamia na kuishauri Serikali ihamie Dodoma na si vinginevyo. Kama tunataka jambo lingine zaidi ya hapa si katika uwanja huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu mkubwa, nasikitishwa sana na wale wanaonyanya mara kwa mara kwa ajili ya jambo hili ambalo liko wazi na zuri. Tukibadili uamuzi huu ambao kwenye Ilani yetu lipo ni jambo gani lingine ambalo tutaaminiwa na wananchi tuliowaahidi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa maeleo mazuri sana hasa kukataa ile hoja wa Wapinzani kwamba, kuwe na tathmini ya sera yetu wenyewe kwa sababu kufanya hivyo ni sawa sawa na ule mfano alioutoa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wa kuanza kufunga magoli kwenye goli lako mwenyewe. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa jinsi hiyo, nashauri mambo mawili, la kwanza Serikali itoe *time frame*, Wizara ipi, ni lini itahamia Dodoma? Napendekeza tuanzie na Waziri wa Fedha na Hazina watafuata wengine. Ushauri wa pili, Serikali ya Awamu ya Tatu isikubali kuingia kabisa katika vitabu vya historia kwamba, yenyewe ndiyo iliyofuta uamuzi huu muhimu wa kihistoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Julius K. Nyerere katika hotuba zake nyingi aliwahi kusema wakati fulani akinukuu maneno ya Bibili ya Mpanzi kwamba, kazi aliyoifanya yeye katika miaka mingi alikuwa kama Mpanzi tu, anapanda mbegu, mbegu nyingine zinaanguka kwenye mwamba, nyingine zinaanguka kwenye miiba, nyingine zinaanguka kwenye udongo mzuri, akahitimisha kazi yake namna hiyo. Moja ya mambo mazito na maamuzi aliyoifanya katika uongozi wa Awamu wa Kwanza ni uamuzi wa kuhamisha Makao Makuu Dar es Salaam kuja Dodoma. Sasa mimi naamini mbegu hiyo ilianguka kwenye udongo wenye rutuba haikuanguka kwenye jiwe au kwenye miiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema tuna utaratibu sasa Serikali kuwa na awamu. Tulikuwa na Awamu ya Kwanza, tukawa na Awamu ya Pili na tunayo Awamu ya Tatu. Tukianza utaratibu wa kuwa tunafuta maamuzi muhimu ya awamu zilizopita, tujuue awamu zinazokua nazo zitafuta maamuzi muhimu ya awamu zilizopo leo. Kwa hiyo, tulinde maamuzi muhimu, tuyafanyie kazi yatusaidie ili tusonge mbele. Kuendelea kutumia zaidi ya nusu ya *Recurrent* Bajeti Dar es Salaam kwenye eneo lisilozidi *square* kilometra 30 pembezoni ya nchi unatumia fedha nyingi kiasi hicho, sidhani kama itatusaidia sana kimaendeleo, tusogee katikati ya nchi, nchi hii ni kubwa, uamuzi huu ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ninaomba Mheshimiwa Waziri, tumuidhinishie fedha zake aende akafanye kazi nzuri. Ahsante. (*Makofii*)

MHE. PHILIP A. MAGANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia mjadala wa leo. Awali ya yote ningependa kumpongeza Waziri mtoa hoja, Mheshimiwa Brigadia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Katibu Mkuu, Ndugu Deo Mmari, pamoja na watendaji wote katika Wizara hii, kwa kutuletea hotuba ambayo ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu mimi nitakuwa na mambo mawili ya kuzungumza, ya kwanza itakuwa ni programu ya uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa, ya pili huko mwisho nitagusia juu ya Mfuko wa *TASAF* ingawa moja kwa moja haukutajwa hapa ndani, lakini mnufaikaji mkubwa wa Mfuko huo ni wananchi ambaao wanaongozwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, amezungumzia juu ya programu ya uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa. Mradi huu unakwenda kwa awamu. Tulikuwa na awamu ya kwanza ilikuwa na Wilaya nadhani 38 na awamu ya pili nasikia ni Wilaya 45. Sasa hizo zingine zilizobaki zitafikiwa lini na awamu moja sijui inachukua miaka mingapi.

Mheshimiwa Spika, programu hii ni nzuri sana hasa kwa muundo wa Serikali za Mitaa ulivyo sasa hivi. Utaona katika hotuba ambayo Mheshimiwa Waziri ametoa hapa, amesema kuna Wilaya ambazo zimepata ripoti safi kutoka kwa mkaguzi wa vitabu na sehemu kubwa ya Wilaya zile ambazo ziko kwenye programu hii. Kwa hiyo, ninachopenda kusisitiza ni kwamba, Waziri achukue hatua za haraka za kuweza kueneza Mradi huu katika Wilaya zote ambazo zimebakii. Wilaya hizo ambazo haziko kwenye programu sasa hivi kwa kweli zinapata uzito fulani katika utendaji wa kazi. Wafanyakazi wake hawana uelewa wa undani wa shughuli zao, Madiwani nao wana matatizo hasa ukizingatia kwamba, sheria inayohusu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Ninaamini kabisa Madiwani wengi hawana ujuzi wa ndani wa lugha ya Kiingereza. Kwa maana hiyo basi, programu ya kutoa mafunzo kwa watu hawa, pamoja na haya aliyosema Waziri kwamba wanatafsiri ile sheria iwe kwa Kiswahili ili waelewe watu wote, mimi nadhani kitu cha kupongezwa, ni kitu ambacho kingefanywa haraka ili na wao waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi kama iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, ningechukua nafasi hii kumpongeza Waziri na kuipongeza Serikali kwa ujumla wake, kwa kuamua kuwalipa mshahara Maafisa Watendaji vijiji. Naamini kabisa kwamba, hii itawapa motisha ya kufanya kazi kwa bidii na vile vile itapunguza minong'ono ya rushwa ambayo labda baadhi ya maafisa walikuwa wanadai kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao kwa sababu hawana mshahara. Kwa hiyo, kitendo cha kuamua kutoa mshahara kwa wafanyakazi hao ni kitu cha kupongezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuongelea juu ya Mfuko wa *TASAF*. *TASAF* ni Mfuko ambaao umebuniwa ili iwe kichocheo cha kuleta maendeleo katika Wilaya mbalimbali, hasa Wilaya ambazo zimeamua wananchi wake kujitolea na kufanya kazi zake kungoja fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama ule Mfuko wa Programu ya Kwanza, *TASAF* nayo inakwenda kwa awamu, Wabunge wengi wame shazungumzia hapa jinsi gani ambavyo hawaelewi sawasawa utaratibu na vigezo ambavyo vimetumika katika kuchagua Wilaya ipi iingizwe katika programu hii. Ni ukweli ulio wazi kabisa kwamba, Wilaya zimeingizwa katika programu hii zimefaidika katika kutekeleza mipango yao ya maendeleo kwa wananchi hasa yale yanayohusu maendeleo ya jamii kwa mfano, upatikanaji wa maji kwa kuchimba visima vipyta, ujenzi wa madarasa ya shule, ujenzi wa *dispensaries* na shughuli zingine nyingi ambazo wanafanya wananchi huko.

Mfuko hu umechangia sana nguvu za wananchi. Mwanzoni tuliona kwamba uchaguzi wa Wilaya hii ije chini ya usaidizi wa fedha za Serikali na fedha za wahisani ambapo ulizingatia katika sekta hii kwamba Wilaya ambazo zimepewa kipaumbele, zipewe kipaumbele katika kuendelea na shughuli zake na pia zitapewa kipaumbele hata kupata msaada huu. Haya yalisemwa na Mheshimiwa Rais, alipokuwa anazindua Bunge lako Tukufu mwezi Desemba, 2000. Lakini katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais, alitoa mifano ya baadhi ya Wilaya ambazo zimejitoa muhanga katika kuleta maendeleo ya Wilaya zao na moja ambayo aliizungumzia sana ilikuwa ni Wilaya ya Ruangwa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ruangwa ni Wilaya ambayo wananchi wenyewe waliomba toka Serikalini iundwe, ikaundwa. Mara baada ya kuwa Wilaya imeundwa, wananchi wa Ruangwa hawakungoja Serikali iwape fedha kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao. Mara moja wazee wa Ruangwa waliamua kukaa chini na kutafuta njia za kuweza kujenga Wilaya yao bila kutegemea sana msaada wa Serikali maana walijua wakitegemea msaada wa Serikali, basi hakutakuwa na maendeleo yoyote.

Kwa hiyo, waliamua kuwa na mfuko wao wenyewe wa kuchangia fedha kidogo zilizotokana na mauzo ya ufuta na korosho na kwa njia nyingine wao wenyewe wameweza kujenga boma ambalo ndio sasa hivi anatumia *DC*, pamoja na jengo la Halmashauri ya Wilaya pamoja na majumba wanayokaa wafanyakazi wa sehemu hizo nilizozitaja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri mwenyewe alijionea alipotembelea Wilaya hiyo mwaka 2002. Ninachoshangaa ni kwamba, Wilaya hii mpaka leo haijawekwa katika utaratibu wa *TASAF*. Mimi ninaamini kabisa kama Wilaya hii ingewekwa katika mfuko wa utaratibu wa *TASAF* ungekuwa kichocheo kikubwa kabisa ukichanganya na nguvu za wananchi wenyewe katika kujiletea maendeleo ya Wilaya ile. Ile Wilaya nadhani ingefaa. Ni Wilaya ambayo haina *resources* nyingi zaidi ya kilimo na ninaamini tatizo linatokana na moyo ambaa wananchi wenyewe wamejjjengea, wakipata nguvu za msaada wa Serikali, maendeleo yatakuwa makubwa sana. (*Makofii*)

Kwa hiyo, naomba sana Serikali ipitie Wilaya hii katika awamu inayofuata ya Mfuko wa *TASAF* kwamba iwekwe kwenye programu ya Mfuko wa *TASAF* kusudi na wao waweze kuongeza nguvu zao ambazo zimeshakua kwa sasa hivi katika kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, nilisema nitakuwa na mambo mawili ya kuzungumza na nisingependa kugongewa kengele ya pili. Lakini kabla sijamaliza napenda kuchukua nafasi hii, kuiomba Serikali kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia kwamba, ifikirie utaratibu wa kuweza kuwa lipa Madiwani wetu posho. Ukweli Madiwani hawa katika hali ya sasa hivi wanakuwa wanyonge sana na mtu unapokuwa mnyonge hupati nguvu, hupati hamasa ya kuweza kutoa mchango wako kwa nguvu zako zote. Mtu asiyeshiba hawezi kufanya kazi au mwenye njaa hawezi kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kumalizia napenda kuunga rai ambayo imetolewa na Mbunge aliyetangulia kwamba, Serikali ifikirie sana kutoa malipo ya posho kwa Madiwani wetu ili na wao wajisikie kwamba kweli Serikali inawajali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kumalizia kwa kusema kwamba, naiunga mkono hoja ilio mbele yetu kwa asilimia mia. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na mimi naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo uliofanyika katika siku za karibuni. Nawapongeza sana. (*Makofii*)

Lakini pamoja na kuwapongeza Wabunge wenzangu labda nilikuwa na machache tu kwamba, nilikuwa nawaasa hawa Wabunge ambaa wamechaguliwa siku za karibuni kwamba, wakifika kwenye Mji,

basi wajifunze kuishi kama wale wa liowakuta kwa maana kwamba watahitaji kupata muda waweze kujua taratibu na Kanuni za Bunge na namna ambavyo wanastahili kuzungumza ndani ya Bunge. Pamoja na yote hayo, pia wajifunze kuheshimu Viongozi wa Kitaifa kwamba watakapokuwa wanawatamka Viongozi wa Kitaifa watamke kwa heshima inayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri sana na niseme tu wazi kwamba, mimi nina imani kubwa na utendaji kazi wa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa TAMISEMI. (*Makofi*)

Niseme kwamba wanajitahidi kufanya kazi kwa kadri wanavyoweza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Ilani hiyo ndio imetupa madaraka tuliyonayo na nina uhakika kama Wizara hii ikitekeleza majukumu yake kama ilivyoyaleta katika Bajeti hii, basi tutakuwa tumetekeleza kwa kiasi kikubwa sana Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa uamuzi wa kuanzisha hii nafasi ya Mtendaji wa Mtaa na uamuzi wa Serikali wa kuamua kuwalipa hawa Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Mitaa. Mimi niseme kwamba, hii itatuwezesha kuhakikisha kwamba, tunamfikishia huduma mwananchi wetu kwa urahisi zaidi, kwa sababu tukishakuwa na hawa Watendaji wa Mitaa, nina uhakika hata masuala ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Kiserikali na shughuli mbalimbali za kimaendeleo yanaweza kufanikiwa zaidi kwa kuwatumia hawa Watendaji wa Mitaa. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba, kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hii kwa mba kuanzia Januari, 2004 Watendaji hawa watakuwa wameajiriwa na kuanza kazi. Niombe tu kwamba suala hili ikifika hiyo Januari, liweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nijikite kwenye maeneo machache kwa sababu maeneo mengine yamekwishazungumzwa. Lakini nilikuwa napenda nizungumzie ukurasa wa 27 kifungu cha 59. Pale Mheshimiwa Waziri anaposema, yapo mambo kadhaa ambayo yamekuwa yakipunguza kasi ya utekelezaji wa mpango wa uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa na mambo hayo ambayo ni changamoto kwa kipindi kijacho ni pamoja na haya yafuatayo ambayo ameyataja. Katika kifungu cha nne amesema: "Kuwepo kwa matukio ya wizi na ubadhirifu wa fedha za Halmashauri kutopteka na ukosefu wa uadilifu kwa upande wa Madiwani na upande wa Watendaji kama ilivyojitekeza katika Halmashauri za Arumeru, Arusha, Korogwe, Musoma Mjini na Tanga."

Mheshimiwa Spika, kama kuna eneo ambalo lina migogoro, ni eneo la Halmashauri zetu za Jiji, Manispaa na Miji. Niseme kwamba ni eneo lenye mgogoro mkubwa kwa sababu aidha, kuna Watendaji wachache amba hawana sifa kwa nafasi au nafasi hizo za uongozi walizopewa au ni Watendaji amba wanalindwa hata kwa kutotimiza majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimesikitishwa kuona Halmashauri ya Mji wa Musoma imetajwa hapa kwamba ni mionganoni mwa Halmashauri ambazo zimehusika na ubadhirifu. Niseme tu kitu kimoja kwamba, tulikuwa na mgogoro kwenye Halmashauri ya Mji wa Musoma. Tulikuwa na Mkurugenzi ambaye tulimtuhumu kwamba amehusika na ubadhirifu wa fedha za umma na ushahidi tukauweka wazi, Tume ikaundwa na baada ya Tume kuundwa hatujapata matokeo ya Tume hiyo. Lakini Mkurugenzi huyo katika siku mbili, tatu, ameitwa kwenda kuhudhuria kwenye semina ya Wakurugenzi pamoja na kwamba amesimamishwa kazi.

Mheshimiwa Spika, taarifa niliyonayo leo ni kwamba, Mkurugenzi huyu amerejeshwa kazini. Lakini tunasema kwamba huu ndio Utawala Bora au ni bora utawala?! Maana kazi ya Madiwani wa Halmashauri zetu ni kusimamia makusanyo ya mapato na kudhibiti matumizi ya mapato yanayotokana na mapato yanayokusanywa. Sasa kama Madiwani wanaweza kumtuhumu Mkurugenzi na ushahidi ukawepo wa wazi kwamba amehusika na ubadhirifu fulani na hii sio kesi ya Musoma tu, hii ni kesi kwenye Halmashauri nyingi na nadhani hata tukipiga kura hapa Waheshimiwa Wabunge wenzangu watanianiwa mkono. Lakini inakuwaje basi tunafika mahali ambapo hata Serikali haionyeshi kwamba inachukua hatua kwa wale watu wanaoonekana kwamba wanafanya ubadhirifu kwa fedha za umma na bado watu hao wanahamishwa? Si tu kwamba wanachukuliwa hatua, lakini bado hawachukuliwi hatua na pale ambapo

bado wanaonekana kwamba ni vipenzi vya viongozi wa Wizara au Tume inayohusika na Ajira, basi wanaondolewa kutoka Kituo kimoja kwenda Kituo kingine. (*Makofii*)

Ningependa nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwanza yeye ni Kamanda wa Jeshi na Jeshi lina amri. Hakuna suala la kubembelezana kwenye ubadhirifu wa mali za umma. Achukue hatua, pale ambapo ushahidi unaonekana upo wazi kwamba Kiongozi Mtendaji wa Halmashauri amehusika na ubadhirifu wa fedha za Serikali, afukuzwe kazi au achukuliwe hatua za kinidhamu na watu waone kwamba Serikali inafanya maamuzi ya dhati kukabiliana na uzembe wa namna hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nimwombe tu Mheshimiwa Waziri kwamba, hata mahusiano ya kazi hayawezi kujengwa kwa misingi hii kwamba pale ambapo tunamtuhumu mtu na tunajua kabisa kwamba ushahidi tuliouweka ulikuwa wa dhahiri halafu anarejeshwa tena kwenye Kituo hicho hicho. Mimi sina tatizo na Mheshimiwa Waziri, lakini nimwombe tu kwamba hatutakuwa tayari kuharibiwa sifa nzuri ya Halmashauri yetu ya Wilaya ya Musoma Mjini, kwa sababu ya aidha tulichukua hatua za kumtuhumu huyu Mkurugenzi ambaye anaonekana labda ni kipenzi sana cha Viongozi wa TAMISEMI ama TUMITAA. Sasa wako viongozi wa namna hiyo wengi ambao wanafanya makosa lakini wanalindwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, rushwa iko katika sura mbalimbali. Kuna rushwa ya ngono, kuna rushwa ya fedha, kuna rushwa ya madaraka na kadhalika. Sasa hizi rushwa ndio zinatufikisha mahali ambapo wakati mwingine watu wanalelewa, wanalindwa hawachukuliwi hatua. Nilikuwa naomba kwamba, basi Waziri atusaidie kwa kuchukua hatua madhubuti pale matatizo yanapokuwa yamejitokeza kwenye Halmashauri. Maana badala ya kuzungumzia mambo ya maendeleo, tutakaa kujadili tu matatizo, migogoro na Viongozi wa Halmashauri hizi. Kwa hiyo, atusaidie ili sisi Wabunge na Waheshimiwa Madiwani tusimamie masuala ya maendeleo, tusikalie migogoro na hii migogoro inatuchelewesha. Sasa kama sisi tumemwona Mkurugenzi wetu hatufai, atuondolee tu wampeleke kule ambako nadhani atakwenda kufanya huo ubadhirifu wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa pia naomba nzungumzie machache kuhusu huu Mradi wa *TASAF*. Huu mradi unafanya kazi yake nzuri lakini niseme tu kitu kimoja kwamba, unaweza ukachukua sura ya kibaguzi. Watanzania maeneo mengi ni maskini na sidhani kwamba vigezo ambavyo vinatumika vinawenza visiwe ni *appropriate* kwa maeneo mengine kwamba mfuko huu uende kuchangia nguvu za wananchi. Nakumbuka kama si mwaka 2002 basi ni mwaka 2001, Serikali iliahidi kwamba mfuko huu ungetembea au ungetawanyishwa ukawafikia wananchi wengi zaidi kwa maana ya kufika kwenye Wilaya zote za nchi yetu. Nasema hivi kwa sababu kuna maeneo unakuta Jimbo moja la Uchaguzi *TASAF* inajenga zaidi ya Shule kumi au zaidi ya Shule tano wakati kuna sehemu nyininge haijapelekwa hata shule moja. Kwa hiyo, nasema Wizara isambaze Mradi huu wa *TASAF* kwenye maeneo mengineyo katika nchi hii ili kila Mtanzania aweze kunufaika na mradi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba, Mheshimiwa Waziri atalifanyia kazi hili maana alishawahi kuahidi kwamba litashughulikiwa kwamba angalau mradi huu sasa uweze kutawanyika kwenda sehemu kubwa zaidi ya nchi yetu.

Mwisho kabla sijamalizia, nilikuwa napenda kusema machache kuhusu mahusiano tuliyonayo kule kati ya Halmashauri, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Wakuu wa Mikoa walikuwa ndio wahimili wa Halmashauri zetu kipindi cha nyuma lakini baadaye utaratibu huu ukabertilishwa wakaondolewa kwenye ile nafasi ya kuwa wahimili wa Halmashauri zetu. Lakini nadhani kutokana na matatizo mengi ambayo tunayapata kwenye Halmashauri zetu, kulikuwa na umuhimu sasa wa kuliangalia upya au kuangalia upya uamuza huu wa kuondoa uhimili waliokuwa nao *RCs* kwenye Hamashauri zetu kwa sababu matatizo mengi yanatokea na muda wa kuchukua hatua unakuwa mrefu sana kiasi kwamba unakatisha tamaa kwamba wakati mwingine watu wanajiliza hivi, mbona kuna matatizo na hatua hazichukuliwi?

Kwa hiyo nilikuwa namshauri Mheshimiwa Waziri, labda aliangalie hili kwamba tuwape nguvu Wakuu wetu wa Mikoa waweze kuchukua hatua za kinidhamu kwa Watendaji ambao wataonekana hawatekelezi majukumu yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mwisho niseme tu kwamba, kama Bajeti yetu hii ya TAMISEMI itatekelezwa, nina hakika tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana ya kufikisha huduma za msingi kwa wananchi wetu. Lakini pia tuseme kwamba wakati umefika kwa Wizara kuhakikisha kwamba inaondoa tatizo la kutokuwa na wafanyakazi au wataalam wasio na sifa. Bado taarifa zetu za hesabu sio nzuri kwa sababu hatuna Wahasibu wa kutosha na tatizo ni kwamba uhasibu sasa ni moja ya fani ambayo ni *too demanding* kiasi kwamba, labda mishahara yetu ni midogo na haiwavutii kuweza kufanya kazi kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, nashauri hilo liangaliwe ili tuweze kuwa na wataalam wa kutosha.

Lakini vile vile kwa upande wa Wakurugenzi, sasa hivi Serikali inapeleka fedha nyingi sana za maendeleo kwenye Halmashauri zetu. Ni wakati muafaka kuhakikisha kwamba tunakuwa na Wakurugenzi ambao wana sifa za kuweza kusimamia shughuli za maendeleo kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii. Naomba kwanza nimpongeze mtoa hoja na wataalam wake wote ambao wameshiriki katika kuandaa na kuleta hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe salamu za pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika chaguzi ndogo na hatimaye kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na leo tuko pamoja. Naamini kwamba tutashirikiana vyema kuhakikisha kwamba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Sera za Chama Tawala zinaheshimika na zinatekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo ningeliomba kabla sijaendelea nitoe pia pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa jinsi alivyowasilisha vizuri hotuba yake na kwa jinsi ambavyo hotuba ile kama msingi wa hotuba nyininge zinazofuata, imekuwa ni Bajeti nzuri ambayo imesifika na kila Mtanzania. Kwa msingi huo, nami ningependa isipite walau bila kulizungumza neno moja ambalo lilinigusa, likanifurahisha na likapongezwa sana na wananchi wangu wa Jimbo la Muleba Kaskazini, nalo ni hili la kumwondolea mwananchi kero namba moja, ambayo ilikuwa ni kero ya Kodi ya Maendeleo au kodi ya kichwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kimsingi Watanzania hawakuwa wanaichukia Kodi ya Maendeleo na kwa kweli walikuwa wanaiunga mkono. Tatizo liligeuka kuwa ni kodi ya kichwa. Haikuwa inaleta maendeleo badala yake ilikuwa inaleta kero. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuona jambo hili kwa kweli lilifikia hatua mbaya badala ya kuleta sifa likawa ni kero.

Mheshimiwa Spika, ninapochangia Hotuba ya TAMISEMI ninaomba kusema yafuatayo tu kwa ufupi: Napenda kusema kwamba, kulingana na msingi wa Bajeti ambayo nimesema ni Hotuba ya Wizara ya Fedha, Bajeti imekusudia kuboresha maisha ya Mtanzania kwa kipindi cha fedha kijacho kwa mambo mengi ambayo yamelengwa, yanaendelea kuboresha huduma za jamii na mengi sana yatakelezwa na hii Wizara ya TAMISEMI ambayo ni Wizara inayofanya kazi na mwananchi wa kwanza kabisa katika mazingira ya mwanzo. Kwa hiyo, Bajeti imekusudia kumwondolea kero na kumwekea mazingira bora ya kuweza kuchangia uchumi wake. Kwa hiyo, mimi ninachopenda kukiomba ni kuweka pia hatua madhubuti katika kusimamia utekelezaji wake na kuangalia zile kero nyininge ndogo ndogo ambazo zimebaki ambazo zinakwamisha wale Watendaji kuweza kufanya kazi zao ipasavyo. Kwa msingi huo, nitaendelea kuchangia kwa kuyataja maeneo kwa maeneo.

Mheshimiwa Spika, nitapenda kulitaja eneo la elimu. Ni juhudu sasa hivi za Serikali yetu kuona kwa mba elimu inaboreshwu katika ngazi ya Msingi kuanzia Chekechea kwenda Sekondari, kwenda Vyuo mbalimbali mpaka Chuo Kikuu. Lakini juhudu hii kubwa ambayo inalenga kumwezesha Mtanzania kumwondolea ujinga na kumpa ujuzi ili aweze kupata nyenzo mojawapo muhimu katika kuchangia uchumi wa nchi hii, kumekuwepo na kero mbalimbali zinazowakera wale wataalam wa elimu hasa walimu.

Mheshimiwa Spika, utakuta walimu wetu hasa hawa wa Shule za Msingi wamekuwa na malalamiko yao ya muda mrefu, ambayo mara nyingi yamekuwa hayashughulikiwi. Kwa mfano, utakuta Mwalimu anapopanda daraja inamchukua muda mrefu sana kupata malipo yake tangu daraja alilokuwa nalo la zamani kwenda daraja jipya. Anapoletewa mshahara, yale mapunjo yake hayapati. Anapopata uhamisho halipwi, ikiwa ni bahati mbaya sasa anatakiwa kupata mafao, basi mafao yale hatapata. Akistaifu atakaa kipindi kirefu kama walivyo watumishi wengine na mwisho anaweza hata akaishia kufariki dunia hajaweza kupata mafao yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nayo ni mionganoni mwa kero ambazo ni kero sugu ambazo nilikuwa nashauri Wizara ya TAMISEMI izisimamie kwa karibu sana kuhakikisha kwamba, Walimu wanapata haki yao. Hatuwezi tukategemea kwamba Walimu watakuwa bega kwa bega na Tawala za Mikoa kuona kwamba elimu inaboreka wakati wao wana malalamiko mengi ambayo hawaoni majibu yake. Lakini wakati huo huo wanapoteza muda mwingi sana katika kufuatilia haki zao ambazo hawapewi majibu. Kwa hiyo, nashauri Idara za Elimu katika kila Halmashauri ya Wilaya ziangaliwe kwa karibu. Zisigeuke kuwa ni kero na mwiba kwa Walimu badala ya kuwa ni msaada na kuwaondolea matatizo hawa wenzetu ili waweweze kupata nafasi nzuri ya kuweza kushirikiana na Serikali katika kuboresha elimu kwa kutoa utaalam wao ipasavyo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nizungumzie suala la pili linalohusu kero. Napenda kuwashukuru wale wenzangu amba wamechangia hili suala linalohusu posho za Madiwani, kwani nayo ni mionganoni mwa kero ambayo inaendelea kulikabili Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wameelezea kero lakini mimi naomba kutoa pendekemo ambalo nadhani Serikali ingeliweza ikaliangalia. Kwa mara nyingi tumekuwa tukizungumza tunaambishiwa kwamba, Madiwani si watumishi, wanategemewa wawe na kazi zao, kwa hiyo hata wakikopeshwa vyombo vyaya usafiri hakuna namna ya kuweza wao kurudisha mikopo. Mimi ningeshauri, ili kuondoa hali hiyo basi, wawe na kiwango fulani cha posho ambacho kitawawezesha kulipa mikopo ya vyombo vyaya usafiri mathalan pikipiki. Madiwani wote nchini hawataweza kufanya kazi ipasavyo kama hawatakuwa na vyombo vyaya usafiri, kwa sababu tunapolenga kutekeleza uzuri wa Bajeti hii lazima wawepo wanaosimamia.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Madiwani wanatusaidia sana katika kusimamia masuala yote ya utekelezaji wa shughuli zetu za Kiserikali. Kwa msingi huo, ninapendekeza kiasi kitakachokuwa kimefaa wapewe, badala ya kuachiwa kila Halmashauri ziangalile, basi kisiwe chini ya kima cha chini cha mfanyakazi wa kawaida aliyeajiriwa katika Taifa letu. Kiwango hicho kama kitazidi kidogo kitamwezesha Diwani kuweza kupata pesa za kukatwa katika miaka mitano kuweza kulpia walau pikipiki moja ya kawaida ya C.C. 100, nafikiri itakayomwezesha kufanya kazi zake katika eneo lake la uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Madiwani wamekuwa wakilalamika kwamba, Wabunge tunapoingia Bungeni tunawasahau, lakini tunapokuwa na kazi tunahitaji watusaidie. Nami naamini kwamba tunashirikiana nao vizuri katika utekelezaji wa sera na hasa ukizingatia kwamba wengi wa Madiwani zaidi ya asilimia 80 ni Madiwani wa Serikali iliyoko madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitapenda pia nizungumzie suala la kero ya Watendaji wa Kata na Vijiji. Naipongeza Serikali kwa kuamua kuwalipa mishahara tangu kipindi cha mwaka ujao, lakini pia imeanzishwa ngazi nyingine ya Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sisi tulio na Majimbo ya Vijijini hatuna Mitaa, tunavyo Vitongoji. Ningependa kufahamu kama utaratibu huu unaosema Watendaji wa Mitaa unahuishwa na Vitongoji kwa sababu katika maeneo yetu ya Vijijini tunayo maeneo mapana sana ambayo yamepeewa sifa za Vitongoji na ingekuwa ni vizuri kama nayo yatawekwa katika Bajeti ili hawa Watendaji waweweze kusaidiana na Watendaji wa Vijiji na wa Kata. Kwa sababu Mitaa inasimamiwa na wale wa Mijini tu na sijaona mahali popote ambapo Vitongoji imetamkwa.

Lakini baada ya zoezi zuri hili ningeomba liambatane na maneno mazuri aliyyoyazungumza Mheshimiwa Mto Hoja katika ukurasa wa tano ibara ya 11, ametamka kwamba vitendea kazi ni nyenzo muhimu sana katika kuleta ufanisi katika utendaji kazi. Ametamka *computer* na vyombo vyaya usafiri. Mimi

sitaki kusemea *computer*. Mtendaji wa Kijiji, Kata, Mtaa na Kitongoji kwa karne hii kwa nchi ya Tanzania ninaomba asaidiwe vyombo vyaya usafiri. Kipindi kilichopita, Watendaji wa Kata walikuwa na pikipiki lakini kipindi hiki hawana chombo chochote.

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu hii itakuwa na mapungufu kama tutaendelea kuona Watendaji wanaendelea kufanya kazi kwa kutembea kwa miguu. Ninapozungumza, mimi siendi Dar es Salaam. Dar es Salaam kuna daladala nyingi. Ninakwenda Muleba ambapo hakuna gari la kuaminika linalokwenda nje ya barabara kuu kwa sababu kijiji changu ama Jimbo langu limetawanyika katika maeneo ambayo magari ya abiria hayafiki na huko ndiko anakotakiwa huyu Mtendaji wa Kata, wa Kijiji na Kitongoji aende akafanye kazi wakati huo hana usafiri.

Mheshimiwa Spika, hawezi kufanya kazi ipasavyo. Kwa sababu inampasa atembee kwa muda mrefu bila kuwa na chombo cha usafiri. Ninaomba hawa Watendaji wapewe pikipiki ili waweze kufanya kazi hii ipasavyo na Sera zetu zitakuwa zimeendelea kuungwa mkono na zitatekelezeka na Wapinzani watapata maneno mazuri ya kusema katika Bajeti ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia katika ajira mpya inayokuja uaminifu na uadilifu viangaliwe kwa makini sana kwa hawa Watendaji wapya wa Kata na Vijiji na Vitongoji na Mitaa watakaoajiriwa. Kwa sababu wanapokwenda kufanya kinyume na hayo ambayo wametakiwa kuyafanya na ikawepo tabia ya kupenda kuwalinda, Serikali yetu inapakwa matope na Sera zetu zinaonekana kwamba si za msingi. Kwa hiyo, katika ajira hii uaminifu na uadilifu wao viangaliwe sana sana na VEO ni moja ya nguzo na katika ajira yao.

Mheshimiwa Spika, ninapokwenda kumalizia zipo kodi nyingine ambazo naomba ziangaliwe na zenyewe ni kero. Kwa mfano, iko kodi ya ardhi na jengo. Unapokwenda kuchukua kiwanja unalipia kodi. Unapokwenda kujenga nyumba jengo nalo unatakiwa lilipiwe. Sasa unalipa mara ngapi juu ya ardhi ile ile, jengo unalilipia, hapo hapo unalipia kiwanja hivi inakuwa ni kwa namna gani? Lakini ukienda kuangalia kodi ile unayolipa nenda katazame, hakuna barabara, hakuna huduma za taka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja ya Hotuba ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulingana na Kanuni mimi sitaki kurudia rudia maana Wabunge wapya wamekwishapongezwa sana. Kwa hiyo, nadhani pongezi zilizokwishatolewa zinatosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali na kuipongeza kwa kuondoa kodi mbalimbali ikiwemo Kodi ya Maendeleo, baiskeli, ng'ombe na nyinginezo ambazo kwa kweli zilikuwa ni kero kwa wananchi na hii imeipa sifa kubwa Serikali ya CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kuzungumzia kuhusu ruzuku ambayo ilikuwa imebuniwa kwa ajili ya kusaidia Vyama vyaya Siasa katika utendaji wake wa kila siku katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya na Miji. Lakini ruzuku hii haikudumu muda mrefu. Waziri aliifuta, lakini sababu za kuifuta hazikueleweka.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tufahamu kwa nini ilifutwa hii ruzuku. Lakini mimi nilikuwa napenda kumfahamisha Waziri na Bunge lako Tukufu kwamba, lengo la ruzuku hii ilikuwa ni kusaidia vyama hasa Chama Tawala kuweza kufanya kazi zake za kuandaa watu. Kazi za chama cha siasa hasa Chama Tawala ni kuwaandaa watu ili waweze kupokea mipango ya Serikali na kuweza kujiletea maendeleo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, chama kinahitaji kupata nguvu, kupata uwezo wa kuweza kufanya kazi hiyo na mara nyingi tumekuta mipango mingi ya Serikali inakwama kwa sababu chama hakikuweza kufanya kazi yake vizuri ya kuwaandaa watu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, kupertia kwako namwomba Mheshimiwa Waziri, atafakari upya, akae chini na wataalam wake na kuweza kurejesha hii ruzuku ili vyama hasa Chama Cha Mapinduzi ambacho kinaandaa watu, vyama vingine vinakwenda kuwaambia watu wagome kulipa kodi, ndiyo maana hata Kodi ya Maendeleo ikaonekana ifutwe, kwa sababu baadhi ya vyama vilikuwa kazi yao ni kuhubiri watu wasilipe kodi. Kwa hiyo, kuweza kupata hii ruzuku na kuweza kupata uwezo wa kufanya kazi ya kuandaa watu na kuwaeleza mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni Ofisi za Wabunge. Namshukuru Mheshimiwa Waziri katika Jedwali la 21 ameelleza hali ya utekelezaji wa kuaandaa Ofisi za Wabunge. Katika Mkoa wetu naona jitihada imefanywa, Wabunge wote wanaonekana wana Ofisi, hata Mbunge wa Viti Maalum, ambaye ni mimi, nimekwishaonyeshwa Ofisi hiyo. Lakini ilikuwa haijakamilishwa na nadhani nikirudi kazi ya kwanza itakayofanyika, Mheshimiwa Mkuu wangu wa Mkoa na Mheshimiwa *RAS* wapo, itakuwa basi sherehe ya uzinduzi wa Ofisi hiyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi napenda niwashukuru viongozi wangu hao kwa kuniandalia Ofisi na kwa vyovoyote ni kutokana na kujua mchango wangu katika Mkoa wetu wa Kagera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba ifahamike wazi kwamba, Ofisi ile itakaa imefungwa. Labda nitakapokuwa nakwenda nikitoka hapa Bungeni mwezi wa nane, basi itakuwa inafunguliwa kwa vipindi ambavyo nitakuwepo wanafagia na kufuta vumbi, lakini nikondoka basi inafungwa. Hii ni kutokana na kwamba, sisi Wabunge wa Viti Maalum hatukupewa wasaidizi. Kwa hiyo, hizi Ofisi zitakaa zimefungwa. Sasa nini maana ya kuwa nazo hizi Ofisi mimi sioni mantiki. Mimi nitamlipa nini huyo msaidizi kama sikuandaliwa kama walivyopewa Wabunge wa Majimbo. Kwa hiyo, ombi langu hapa ni kwamba na sisi Wabunge wa Viti Maalum tupewe wasaidizi, tupewe uwezo wa kuwa na wasaidizi ili tuweze na sisi kufanya kazi zetu vizuri. Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo wengi wamekwishatambua umuhimu wetu kwa sababu kwa kweli tunasaidiana kazi mbalimbali katika Majimbo yao. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nikiamini kwamba hili limefika, naomba nizungumzie suala lingine ambalo linahusu utendaji kazi wa baadhi ya Maofisa katika Halmashauri zetu za Wilaya na Miji.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Watendaji hawa ni wazuri. Lakini wako wengine wanaoacha kufanya kazi zao wanajiingiza katika mambo ya siasa. Wanajiingiza katika mambo ya siasa kwa hiyo unakuta kwamba kazi zao zinakwenda vibaya, wanavuruga. (*Makofi*)

Hii hasa Mheshimiwa Spika, inatokana na Watendaji hawa wanapokaa katika nafasi zao kwa muda mrefu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa napendekeza kwamba, Mheshimiwa Waziri awe na utaratibu wa hawa Watendaji kuwa wanahamishwa kila ya baada ya muda angalau kila baada ya miaka minne mtu asikae katika Kituo cha kazi kimoja. Zaidi ya hapo kwa kweli ni kuanza kuvuruga, anaanza kuingilia katika kazi ambazo si zake na hata kuwazuia Waheshimiwa Madiwani kufanya kazi zao au Mwenyekiti kufanya kazi zake vizuri. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba nisemee hilo.

Mheshimiwa Spika, neno hili haliwezi likanipita mimi bila kulizungumzia, ni kuhusu Madiwani. Yako maandishi yaliyokwisha andikwa juu ya Madiwani kwamba Madiwani wanapaswa kuwa na kazi zao. Lakini wakawalinganisha na Wenyeviti wa Vijiji au wa Mitaa. Madiwani kwa kweli si sawasawa na Wenyeviti wa Mitaa au Wenyeviti wa Vijiji. Diwani ni Diwani eneo lake ni Kata. Lakini kazi zake hazitofautiani sana na kazi zetu. Kwa kweli tunafanya kazi kama timu.

Kwa hiyo, kuweka pengo kubwa sana kimaslahi kati ya Wabunge na Madiwani ni kujenga kitu kibaya ambacho ni kujenga chuki ambayo haina sababu. Kwa kweli kwa hatua hii naomba Mheshimiwa Waziri alone hili wazo la kusema kwamba, Diwani ni sawasawa na Mwenyekiti wa Kijiji au Mwenyekiti wa Mtaa, kwa kweli lisahaulike lakini akae chini aone ni namna gani hao Madiwani wanaweza wakasaidiwa nao wakafanya vizuri katika kazi zao. Kwa sababu kama tunavyojuja Diwani ni kiongozi

anayeongoza watu kwa hiyo, anapaswa kuwapa huduma za hapa na pale. Mgonjwa anamkimbilia, mfiwa anamkimbilia. Yeye anahitajika kuhani misiba yote inayotokea katika Kata yake. Diwani anahitajika kutoa michango katika miradi mbalimbali anapokwenda kuhamasisha wananchi kufanya kazi za maendeleo. Kwa hiyo na yeye ni lazima achangie.

Mheshimiwa Spika, Diwani kupewa shilingi 30,000/= ni pesa kidogo sana. Lakini pia nisisahau kwamba Madiwani kama tulivyo Wabunge hata Wabunge wa Vyama vyote tunategemewa kuvisaidia vyama vyetu ili viweze kufanya kazi zake za kununua hata *Stationary* na shughuli nyingine za chama kama zinavyojulikana.

Kwa hiyo, unakuta kwamba ile shilingi 30,000/= kwa kweli ni kiwango kidogo sana na kama wenzangu walivyozungumza, kweli ni vizuri Serikali ikafikiria, ili kumsaidia huyu Diwani naye aweze kufanya kazi zake vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, napenda kumkumbusha Waziri aziangalie Idara nyingine katika Halmashauri ambazo hazipewi fungu, mafungu ya *Other Charges* kama Elimu, Afya, Ujenzi na Kilimo, lakini zipo Idara nyingine kama Ushirika, Idara ya Maendeleo ya Jamii na kadhalika, hizi ni Idara muhimu sana. Lakini unazikuta zinafanya kazi katika unyonge mkubwa sana kiasi kwamba, kwa kweli unawahurumia. Wanatembea kwa miguu. Hata wanapotakiwa kusafiri kwa Maendeleo ya Jamii au wale wanaoshughulika na shughuli za vijana basi wanamega kwenye mafungu yale ya Mifuko ya Wanawake na Vijana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, unaona kwamba hakuna haki pale kwa sababu zote ni sawa na Idara nyingine, kila Idara ina majukumu yake. Kwa hiyo, si vizuri kuzibagua Idara nyingine na kusema kwamba hii ni Idara nyeti na hii ni Idara ovyo. Kama kama ni Idara ya ovyo basi ifutwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sina mengi na nisingependa kengele ya pili isinigongee kwa sababu nina nidhamu sana mbele yako. Kwa hiyo, nakushukuru na ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kuhusu Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza naunga inkono kabisa bajeti hii mia kwa mia. Lingine napenda kuipongeza sana Serikali kwa Bajeti nzuri na kodi na michango ya aina mbalimbali ambazo wamefutiwa wananchi. Kwa kweli tunaipongeza sana na kwa niaba ya wafugaji wenzangu, wafugaji wote walioko Tanzania, naipongeza Serikali kwa kufuta kodi ya mifugo. (*Makofi*)

Pamoja na kuwa kwenye Halmashauri yetu hatukuwahi kulipa kodi lakini nilifurahi sana jana wenzangu walipofutiwa kodi pamoja na kodi ya makanyagio. Hiyo kodi ya makanyagio ilikuwa ni kodi ya dhuluma. Kwa hiyo, tunafurahi sana Serikali kuiondoa. (*Makofi*)

Namshukuru sana Msemaji wa Upinzani, kwa mara ya kwanza kusimama pale na kuipongeza Serikali na hii nafikiri tangu tuanje Bunge hili miaka 7 iliyopita, leo ndiyo nimemsikia anaipongeza Serikali. Kwa kipindi hiki imeonyesha kwamba wamekosa kabisa la kusema. (*Makofi*)

Ningependa kuishukuru Wizara hii. Kwanza ningependa kusema kwamba, Wizara nyingine ziige mfano wa Wizara hii. Wizara ya Tawala za Mikoa ni Wizara yenye majukumu makubwa sana Tanzania nzima kwa sababu Halmashauri zote malalamiko yao wanaleta pale na malalamiko ni mengi. Hakuna sehemu yenye matatizo, malalamiko na vurugu kama Halmashauri zetu, zipo Halmashauri zipatazo 118. Ni vurugu tupu. Lakini Wizara inawasiliza na Mbunge yeoyote akienda pale Ofisini anasikilizwa. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri na Ofisi yako tunawashukuru sana kwa kutusikiliza. (*Makofi*)

Pamoja na hayo ningependa kusema machache, kwanza niliona Waziri katika hotuba yake uanzishwaji wa Halmashauri mpya katika ukurasa wa 10 mpaka ukurasa wa 11. Niliona uliweka utaratibu huo na tumesikia na tumesoma lakini mimi mwenye nina ombi, ukiangalia Tanzania yetu ni kubwa sana na sijui kama kila Waziri alitembelea maeneo yote ya vijiji au tarafa au wilaya. Kiografia nadhani kuna

Wilaya zinazoonekana tu kwenye ramani. Wilaya ya Monduli ina Majimbo mawili. Makao Makuu ya Wilaya ni Mondoli. Jimbo langu kijiografia utaenda mpaka utasema mwenyewe kwamba, Jimbo la Longido halipo Mondoli. Jimbo langu linaanza nyuma ya Mlima Kilimanjaro tunapakana na Mheshimiwa Mramba. (*Makofi*)

Kule Kamwanga, kuna Kamwanga ya Rombo na Kamwanga ya Monduli. Kwa hiyo, Jimbo linaenda *Lake Natron*, wananchi wanapata matatizo makubwa sana. Mtu aliyeo Kamwanga akija Wilayani mpaka azunguke apite Ngerenairobi kwa Mheshimiwa Mwanri aingie Hai, aende Arumeru Mashariki, aingie Mjini aende tena Arumeru Magharibi ndiyo aende Monduli. Kwa hiyo, watu hawafahamu Monduli iko wapi, ni watu wachache wanaofahamu Monduli. Ukiya huku Magharibi ni *Lake Natron*, kwanza kufika Longido ni kilomita 127, ndiyo afike Longido. Aende tena Monduli ni kilomita 126. Nauli ni Sh.10,000/= kwenda Wilayani. Sasa mwalimu aliyeo huko aende Wilayani ni Sh.10,000/= kwenda na kurudi ni Sh.20,000/= bila kula.

Takwimu ya wagonjwa mnayoona katika hospitali ya Wilaya, hawapo watu wa Longido. Hakuna mtu wa Longido anayekwenda hospitali ya Wilaya, hawaendi. Hospitali yao ni Arumeru na Arusha Mjini. Huendi Monduli kutafuta nini, ni mbali. Kwa hiyo, Seliani ile Hospitali ya *Mission* ndiyo hospitali yao. *Data* mnazozipata za wagonjwa wa Monduli hawapo watu wa Longido.

Kwa hiyo, naomba muangalie sana mtupe Wilaya. Naomba sana sana mtupe Wilaya, kwa sababu watu wanapata shida kabisa. Ukiangalia mambo ya Mahakama, watu wanapeana anachodaiwa ili usipelekwe Mahakamani kwa sababu Mahakamani ni gharama kubwa sana kwenda Mahakamani. Haiwezekani, wengine wanatumia Sanya Juu wanakimbilia Sanya Juu, ndiyo waende Mahakamani, wakienda kule wanaulizwa Wilaya yako ni wapi? Hawataki kwenda kabisa Mondoli. Kwa hiyo, naomba sana mtusaidie watu wa Longido tupate Wilaya.

Jambo lingine ambalo ningelipenda kulizungumzia ni tofauti za *data* za fedha kwenye majedwali. Kwa kweli nawaunga mkono sana kutoa taarifa hii na ningeomba hiki Kitabu chako kipelekwe katika Halmashauri zote Wakurugenzi waweze kukisoma kwa sababu siyo siri. Kwa hiyo, ningependa upeleke huko nao wakaisome, waone jitihada na mipango ya Wizara yako. (*Makofi*)

Kuna tofauti kubwa sana kati ya takwimu zilizopo kwenye majedwali haya na zilizoko Wilayani. Kwa hiyo, taarifa ambayo sisi tunayo Wilayani ni tofauti na hizi. Kwa hiyo, tunaomba sana. Hapa nimegundua kwamba, kumbe taarifa wanayopewa Waheshimiwa Madiwani ni tofauti na taarifa zinazotumwa kwenu. (*Makofi*)

Hasa ujenzi nimeona hapa ujenzi wa madarasa, majengo, nyumba za walimu, zilizojengwa katika Wilaya yetu. Tumejenga zaidi ya majengo yaliyoandikwa hapa na kuna fedha zingine ambazo sisi hatuzijui na Waheshimiwa Madiwani hawazijui ziko hapa. Tulikuwa tunauliza eti fedha za mikopo, Waheshimiwa Madiwani hawajui. Kwa hiyo, ningependa tu kusema kwamba, hizi taarifa mzicheki tena vizuri ili Wakurugenzi wasilete *data* ambazo hazipo.

Lingine ningependa kusema kama wenzangu walivyosema kwamba, Halmashauri zetu zina majukumu makubwa. Ningeomba Ma-DC na Wakuu wa Mikoa warudishiwe kabisa Halmashauri hizi wazisimamie. Ndiyo wanawenza wakasuluhisha migogoro, wakatatuwa migogoro mingi sana iliyoko katika Halmashauri zetu. Kama tulidhani kwamba Wakuu wa Mikoa hawana kazi, hawakuwa wanasaadidia, hapa ndiyo tumejuta. Kila mmoja anasema ni afadhali warudishiwe, tatizo likitokea hujui uende kwa nani. (*Makofi*)

Ma-DED yaani wamekuwa wajeuri kabisa ili tuweze kufikisha kwa Mkuu wa Mkoa. Baadaye iende hapo Wizarani. Sasa ije hapa Wizara, watu wameangamia kule. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba, Wakuu wa Mikoa, Ma-DC, warudishiwe kabisa wawe wahimili wa Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba ningependa kuzungumzia Ofisi zetu za Wabunge. Ukiangalia katika jedwali hili utadhani kila Mbunge ana ofisi, ni Wabunge wachache sana hawana Ofisi na mimi sijui kama nimeandikwa kwa mba ninayo sijui. (*Kicheko*)

Kwa sababu naona ni Wabunge wawili tu ndiyo hawana Ofisini. Sasa nashangaa mimi na nani? Kwa sababu mimi najijua mwenyewe. Sijui na nani mmoja mwingine kati ya Wabunge wa Mkao wa Arusha? Lakini tunalia kila siku hatuna maofisi. Sijui nyumba ya mtu kama una nyumba yako umefanya Ofisi, ndiyo ukahesabiwa kwamba una Ofisi sijui. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini tungeomba kwanza tufahamu fedha zinazotumwa kwa ajili ya Ofisi ya Mbunge. Sisi wenye we tuelewe, kwa sababu tunapokaa humu tunatofautiana. Mwingine anasema mimi napata Sh.50,000/=, mwingine anasema mimi nimepata shilingi milioni mbili, mwingine hajapata kabisa. Kwa hiyo, hii tofauti inatoka wapi? (*Makofi*)

Kwa hiyo, utaratibu huo na sisi tuuelewe kwamba fedha zilizotumwa kwa ajili ya Ofisi ya Mbunge, kwa ajili ya samani ni kiasi kadhaa, uelewe mwenyewe. Usiwe unasubiri mpaka *RAS* akueleze kwamba umetumiwa fedha kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni. Kipindi cha jioni kitaongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika.

(*Saa 06.54 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye hotuba yake ilikuwa imepita jana. Mimi sikuchangia lakini nampongeza sana kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na kwa hotuba nzuri ambayo imetolewa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niseme *with respect to* Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, anasema hotuba tunasema ni nzuri, nzuri. Sasa hotuba hii ni nzuri, *full-stop*, ni nzuri na mimi *nit substantiate*, nitaeleza vizuri kwamba kwa nini ni nzuri. Unaposema hotuba ni nzuri unaangalia matarajio na matumaini ya watu, kama yanakuwa *accommodated* humu ndani unasema ni nzuri. Nataka niizungumzie hii Wizara kidogo, nichukue muda hapa kuzungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na pia Katibu Mkuu wa Wizara hii, napenda kuwapongeza sana. Hawa ni watu makini na watu *serious* pamoja na wote waliopo pale, napenda kuwapongeza na nitaeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimsoma Che-Guivara, ukimsoma Fidel Castro, ukiwasoma hawa watu wenyewe mawazo ya kimapinduzi hawa na akina Samora Machel, wanakwambia Mapinduzi ni mabadiliko ya haraka ambayo yanaleta manufaa kwa watu na nimchukue Samora Machel. Samora Machel alisema, ukitaka kuleta Mapinduzi angalia ni kwa kiasi gani uko tayari kufanya kazi kwa muda wa ziada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka njielekeze kwa Wizara hii, mimi nataka nitoe ushuhuda. *Several times* nimekwenda kwenye hii Wizara siku za *weekend* ambazo si za kazi, nimemkuta Katibu Mkuu anafanya kazi, unakwenda Ofisini kwake saa mbili ya usiku unamkuta Ndugu Mmari anafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikifanya kazi nzuri tuseme imefanya kazi nzuri na tukiona *seriousness* tuseme kuna *seriousness*. Wizara nyine msijisikie vibaya leo tunaizungumzia Wizara hii mkija tutasema, kama mambo ni mazuri tutasema ni mazuri, Wizara hii isikilize hata namna inavyojibu maswali yake, *excellently*. Hawa walikuwa wanapata Hati Chafu ukiacha Halmashauri tatu, nyine zote zilikuwa zinapata Hati Chafu, leo ripoti hii inatuambia Halmashauri 68 zinapata Hati Safi. Mimi napenda niseme kwamba, viongozi hawa nawachukulia kama viongozi waliotukuka katika nchi hii, ambao naamini *they are very serious.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza habari ya maboresho, ukizungumzia habari ya MMEM hapa katika nchi hii unaipeleka kwenye Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ukizungumza habari ya maji unaipeleka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ukizungumza Ushirika na Masoko unapeleka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, *zingumzia* Wizara yoyote uniambie, *fall back position* yake ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa *in my own opinion* naiona Wizara hii kama roho ya Serikali, ukiivuruga hii utapata matatizo makubwa sana. Nadhani ninakubaliana na Mheshimiwa Rais, ndyo maana hekima na busara zilimpeleka kufikiri kwamba iko haja ya kuiweka Wizara hii chini yake, mimi nafikiri ni mawazo mazuri sana. Majukumu ya Wizara hii, ni majukumu makubwa na yameainishwa humu ndani. Mimi kilichonifanya niseme nita-*substantiate* kwa nini nimetoa sifa hizi. Kama mnakumbuka huko nyuma tuliwahi kuvunja kitu kinachoitwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tukaondoa tukazileta hapa baadaye tukaamua kurudisha. Majukumu yake ni mapana, Halmashauri zake ni 117 na wako Wakuu wa Mikoa hapa. Mkuu wangu wa Mkoa wa Kilimanjaro na *RAS* wake wa Mkoa wa Kilimanjaro, Bwana Chikira, mimi nawapongeza kwa ushirikiano ambao wanautoa Mkoani Kilimanjaro na katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Hai, wanafanya kazi nzuri na nitaeleza vizuri. Mimi leo nataka njiweke hapo hapo, niseme hapo hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisema unataka kudhibiti, kusimamia mapato na matumizi ya Serikali kwa Wizara kubwa kama hii, kwa Wizara yenye majukumu makubwa kiasi hiki ni lazima ufanye kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, lazima *u-create* kada maalum itakayofanya kazi maalum na humu ndani tumeambiwa habari ya mafunzo, tumeambiwa habari ya semina, tumeambiwa habari ya kwamba nchi ya Finland wanatusaidia mafunzo katika nchi yetu. Tumekwenda kwenye semina, sisi Waheshimiwa Wabunge tumehudhuria kwenye semina na pia Madiwani wetu wamesafiri wamelala huko wamekuja wakiwa wamepata kitu, *seriousness* unaiona kabisa, ni watu wanaotaka kuleta mabadiliko katika nchi hii. Ukisema kwamba, malengo yaliyowekwa hapa siyo mazuri, hayaelewiki, nitakushangaa! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kwanza, ni kupanga kada maalum katika *focal point*. Maeneo muhimu na nyeti ya maendeleo ya nchi hii huwezi kumpa mtu kama mtu tu na ndyo maana wanazungumza katika hotuba hii, sasa hivi wanafanya tathmini. Ukimwona yuko hapa *DED* wa Halmashauri haelewi kitu unamwambia *off you go* wewe hunisaidii, unamtafuta mtu ambaye anafanya kazi *twenty four hours seriously*, anataka kuleta *development* kwa ajili ya watu wake. Katika *record* hapa unamwona anachukua hela za Serikali anatumia ovyo ovyo, unamwambia kwaheri bwana fika salama na humu ndani tumeambiwa kwamba kazi hii imefanyika, hapa. Nchi hii huhitaji tu kuwa *intelligent, you got to have guts* kwa kufanya mambo yaani ufike mahali unafanya mambo Mheshimiwa Brigadia Jeneral Hassan Ngwilizi, watu wakuone kama mwendawazimu kidogo, ukisema tu unakwenda hivi mara hivi, nchi hii ni pana na kubwa namna hii hutaweza.

Mimi nakushukuru kwamba, unazunguka nchi nzima popote panapotokea matatizo. Sasa nikusaidie, natambua Katiba ya nchi Ibara ya 145 - 146 inatambua mamlaka na madaraka ya Halmashauri, nataka niseme hapa nisije nikafika mahali nikaonekana naji-*contradict*. *The idea behind* ni *give more powers to the people*, maana yake sisi Madiwani na *Councilors* tupewe madaraka na majukumu ya kusimamia mambo yetu sisi wenyewe, hiyo ndyo *assumption*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiwa Dodoma ukasema unataka kuidhibiti Halmashauri ya Wilaya ya Moshi au Hai bila kutambua kwamba unayo *extension* yako ya Ofisi ya Mkoa katika Mkoa pale na ukaipa mamlaka yale yale na madaraka yale yale ukasema *yes on, hands off*, watamaliza hela zote pale mzee wangu. Hawa wanaume hawa na akina mama walipo pale, Wakuu wa Mikoa wape madaraka wakati wowote mambo yakiwa hayaendi vizuri wafanye *intervention*, waingilie kati. Sauti hii imezoleka humu ndani, mzee wangu hakuna ugomvi hapa huu ni msisitizo tu. Sasa nisaidie kidogo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hili kwa sababu nimewahi kuwa Mkuu wa Wilaya. Kama Mkuu wa Wilaya nilikuwa ni jicho la Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa ndiye jicho la Serikali katika eneo linalohusika, yeze ndiye Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za Serikali katika Mkoa, yeze ndiye anayesimamia pale, ukisema tu demokrasi, Gorbachiov aileta demokrasi pale kwake *giving more power to the people liberty, independence* na nini wakaanza kunyanya pale Ukraine wakasema na sisi tunataka mahali pale. Demokrasi ambayo haina *limit in terms of responsibility* itatufikisha mahali pagumu, Wakuu wa Mikoa wapewe nafasi. Huo utaratibu tuliojiwekea hapa na maelezo haya ninayoyatoa hapa hayamaanishi kwamba tutengue utaratibu tuliojiwekea, lakini pale popote ambapo Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya amefika mahali anafikiri kuna kitu kinakwenda ovyo ovyo hivi aingilie kati mara moja.

Huwezi kukaa pale ukasema kwamba sasa hii najua wataniuliza, nikitoka nje watanibana, wewe bwana mdogo unaposema namna hiyo lakini unajua Sheria sisi haituruhusu kufanya hivyo, lazima tuweke kipengele, lazima tufikirie vizuri. Tutafakari upya majukumu ya Ofisi ya Mkoa kuhusu usimamizi wake wa Halmashauri hizi. *It is my sincere opinion* kwamba, kuna namna ya kutafakari tena upya *with due respect*, najua hii ilikuwa ni debate ndefu lakini lazima tulitazame hili. Ukimaliza unawapa majukumu mapya na majukumu mapya ndiyo haya yaliyotolewa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, panga makada katika *focal point*, kada hapa wala simaanishi hii ya kichama chama, *ideological*, ni kada ambaye yuko tayari kuifia nchi yake, kupigania nchi yake au kuwa *committed*, muweke pale na hawa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wawekwe pale. Huwa nasikiliza redio Wakuu wa Mikoa nawafahamu, hakuna mtu wa ajabu hata mmoja hapa, ni watu safi kabisa hawa. Wakuu wa Wilaya ni wachache na wale wachache ambao wamefanya vitu vya ajabu ndiyo hao umewashughulikia mzee wangu. Mimi nilipokuwa pale sikushughulikiwa mambo yangu yakienda vizuri, wewe ukisema kitu mimi nilikuwa nasimamia kama inavyotakiwa. Kwa hiyo, nilitaka nisaidie katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *debate* hii ya kwamba sisi ndiyo Chama Tawala na hii ni kwa rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, inasemwa sana na naomba nisaidie kidogo. Ukitsema chama hiki ni Chama Tawala, maana yake ni kwamba, chama hicho ndicho kinachounda dola, ndicho kinachokuwekea chombo cha dola pale. Kwa hiyo, ukisema Hai pale kwangu kwamba wewe Chama chako cha CHADEMA ni Chama Tawala, mimi sikuelewi kwa sababu ninajua Mkuu wa Wilaya aliye pale anapewa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ili aitekeleze. Kwa hiyo, Chama Tawala pale ni Chama cha Mapinduzi. Nataka ku-*underscore* kitu kimoja hapa katika hii *debate* ambacho hatuelewani, ni kweli kabisa kwamba ukiwa na *majority* na *Councilors* utakuwa na *advantage* katika maeneo makubwa matatu. Moja, katika ku-*influence* maamuzi, pilii, katika kuitishaa Bajeti na tatu, katika kuunda Sheria Ndogo Ndogo, maeneo matatu. Kwa hiyo, nataka niweke vitu vyangu sawa sawa hapa mzee wangu, nimetumwa na watu wa Siha kuja kusaidia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hicho kinachowafanya ninyi mnafikiri kwamba ni Chama Tawala, hayo maeneo matatu, ndiyo yanayowafanya ninyi mnafikiria hivyo, Chama Tawala ni *overall*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Clinton yeze hakuwa na Wabunge wengi wakati ule, Wabunge wengi walikuwa wanatoka *Republican* na yeze alikuwa ni *Democrat* lakini chama kilichokuwa kinatawala wakati ule ni *Democrat* pamoja na kwamba *Republican* walikuwa wengi. Sasa mimi nafikiri leo Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa tumeelewana hapa, mimi nafikiri hakuna haja tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuomba kitu kimoja kwa Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, ili aweze kunisaidia. Kule kwangu *West Kilimanjaro* hatuna utaratibu wa Vijiji, tunavyo Vitongoji tu, Lendrosi, Lemosho, Simba, Suzana, Ngarenairobi, Namwai mpaka Kamwanga hatuna utaratibu sisi wa Vijiji; je, kwa utaratibu huu wa Serikali kwamba sasa tutakuwa na Maafisa Watendaji, watakwenda kuniuliza kule kwa sababu ya mashamba makubwa makubwa, hatuna Vijiji kule, huko mbele ya safari ndiyo tuna-*plan*. Ningependa nielezwe hapa kwa ajili ya ufanuzi kwamba inakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ni kuhusu Madiwani wetu. Chonde chonde baba tunakuomba, kila siku tukienda Halmashauri wanatuambia Waheshimiwa Wabunge wetu mkienda kule mkatusemee. Hatuna haja ya kufikiria habari ya mishahara lakini tufikirie namna ya kuongeza posho za Madiwani wetu. Diwani kule kwetu ndiye Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa Kijiji na ndiye msimamizi wa miradi na shughuli zote, mipango yote tunayoizungumzia hapa ya MMEM na kila kitu, anayesimamia pale ni Diwani, hatuwezi *ku-marginalize* tukamwacha awe pale pembeni halafu huku chini yake kuna watu wengine wadogo kuliko yeye. Sasa hivi tunasema walipwe mshahara, haitawezekana hata kidogo. *Without financial muscle* huwezi kuwa na *political muscle*, lazima uwe na *political muscle* ambayo inatokana na hiyo *financial muscle* akiwa ni wa kuomba omba tu *petrol*, baiskeli na sijui nini yaani hana uwezo hataweza mzee wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na napenda niseme kwamba, mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Siha, ninaunga mkono hotuba hii na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuipitishe mara moja wala tusiwe na wasiwasi. Nashukuru. (*Makofi*)

MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hii hoja ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama katika *session* hii, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, waliokuja baada ya *by-election*, hasa wale ndugu zangu wa Bukoba Vijijini na Kigoma Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwapongeza marafiki zetu wa upande wa Upinzani waliookea Pemba kwa kuja Bungeni. Nafikiri uchaguzi mdogo huu umedhihirisha wazi nia ya CCM na Serikali yake ili kuhakikisha kwamba kuna demokrasia halisi ndani ya nchi hii na kwamba Serikali ya CCM na chama chake inafuata kikamilifu Muafaka amba CCM ilitia sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ielewewe kwamba, hapa Bungeni tunakuja kuisaidia Serikali, kuipa mawazo ya kuwaendeleza wananchi. Kwa hiyo, malumbano ambayo yako *misplaced* hayashauriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye hii hoja napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake na kwa Bajeti ya Wizara yake. Naomba niseme kwamba, nilishiriki katika ngazi ya Kamati katika kuijadili. Kwa hiyo, mawazo yaliyotolewa na Kamati hapa asubuhi ni mawazo ambayo nilishiriki katika kuya-*formulate*. Lakini kuna machache ambayo ningependa kuongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo katika *Local Government*. Sasa hivi tunalo tatizo kubwa sana hasa kwenye ngazi za chini kuhusiana na uwezo wa viongozi kujua uwezo wao na mipaka yao. Kwa hiyo, kule chini *kunatokea* kitu kama ushindani na mara nyingi kumekuwa na ushindani kati ya wanasiaya ngazi za chini na Watendaji ngazi za chini. Napenda kuipongeza Serikali kwa kufikiria umuhimu wa hii elimu hasa katika ngazi za Mitaa na ngazi za Kata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *concern* yangu kubwa ni pale penye Utawala Bora. Ninao wasiwasi sana juu ya uendeshaji wa Mabaraza ya Kata katika zile Kata. Mabaraza mengi sana ya Kata ambayo nimeduwa na uhusiano nayo, yameonekana yanafanya kazi zake kiholela na mara nyingi ndiyo wanaoweza kugawa ardhi halafu wanaandika *summons* ambazo hazifiki halafu wanahukumu hao hao. Nafikiri ni muhimu sana wafundishwe pia uwezo wao na namna ya kuutenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali kuhusiana na kuamua kuwalipa Maafisa Watendaji wa Mitaa na Vijiji mishahara. Lakini ningeomba Mheshimiwa Waziri aweze kutufafanunulia tofauti kati ya Afisa Mtendaji wa Kijiji, ambaye yuko kwenye hotuba yake na Afisa Mtendaji wa Kijiji ambaye yuko chini ya Kifungu cha 56(1) cha *Local Government District Authorities Act*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hii *Local Government Reform Program*. Napenda kuipongeza sana lakini *at the same time* naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge, ambao wameishauri Serikali juu ya nafasi ya *Regional Commissioners* na *District Commissioners* katika hiyo programu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi ya Sheria zetu tulizonazo sasa hivi, tuna *parallel system* ya Serikali ambayo kuna hatari, tuna-*marginalize Regional Commissioners* wetu na Ma-DC wetu. Ukweli ni kwamba, kufuatana na hizi Sheria za Serikali za Mitaa, walio na mamlaka ni zile Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Miji, hakuna nafasi ya *Regional Commissioner* wala ya DC katika *level* ya maamuzi. Maamuzi yote yanafanyika kwenye *level* ya *District Council*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwamba pamoja na zile Sheria za *Local Government* zinampa *Regional Commissioner* kazi ya *ku-coordinate activities* za Serikali Kuu katika Mkoa, lakini haimpi sauti yoyote katika ngazi ya maamuzi, *likewise DC*. Imeshatokea kwamba DC anataka kuingia katika Mkutano wa *Council* anaambiwa wewe siyo Mjumbe au anataka kushauri anaambiwa aah wewe ni mtazamaji tu. Hii ni hatari sana kwa sababu lazima tukubali kwamba wale watu wameteuliwa kwa sababu ya uwezo wao. Nafasi ya mwanasiasa ni miaka mitano na huenda ikiwa tunateuliwa kwa uwezo wetu wa kuchukua watu kwenye majukwaa lakini wale waliowekwa pale ambao ni Watendaji wa Serikali ni watu ambao wako pale kwa ajili ya uwezo wao, waifuje wasiifufe lakini ni wajuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii *Local Government Reform Program* mimi nilikuwa nashauri kwamba, kile Kifungu cha 174(a) cha *Local Government District Authorities Act* kiangaliwe upya, kwa kweli *devolution* na *decentralization* ni muhimu. Lakini una *devol* na una *decentralize*, unampa *autonomy* mtu ambaye anaewela anafanya nini na ana uwezo wa kufanya. Hakungekuwa na haja ya *ku-monitor* kama tusingejua kwamba kuna haja ya kupata ushauri mkubwa zaidi. Sasa kile kifungu cha 174(a) cha *Local Government Authorities Act, relations with Central Government, relation* ya *District Authorities*, mimi niliona kama kina *conflict* na *autonomy* ya *District Councils* kwamba *Regional Commissioner* ye ye anapewa kazi ya kufanya uchunguzi pale ambapo kuna ugomvi lakini pia hana uwezo wa kiutendaji, hana *executive power*, ye ye anafanya uchunguzi tu. Kuna *Council* moja ambayo *Regional Commissioner* alifanya uchunguzi na akasema hawa watu hamkuwaajiri ninyi, ni wafanyakazi wa Serikali Kuu, kwa hiyo, hamkuwa na uwezo wa kuwafukuza lakini ile *District Council* ikasema hatuwataki, haikumsikiliza *Regional Commissioner*. Sasa tunam-reduce *Regional Commissioner* kule Mkoani kwake na *District Commissioner* kule Wilayani kwake kuwa *Political Commissar*. *Political Commissar* kama hawataki kumsikia ni kwamba wanamdhara. Ninaomba hicho kifungu pamoja na Kifungu cha 54(a) cha *Local Government District Authorities Act* viangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo yangu ni kwamba ijapokuwa kuna haja ya *decentralization*, ile *decentralization* isifanyike *at the expense* ya kuleta *conflict* kati ya *Central Government* na *Local Government* au kuffiisha juhudzi za *Central Government* kuleta maendeleo katika Mikoa na Wilaya zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo niliyoyasema, napenda kusema kwamba, mengine nilishiriki kwenye ile Kamati, naomba niseme kwamba nampongeza tena Mheshimiwa Waziri na naunga mkono Bajeti yake kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nami nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wapya walioingia katika Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge wa CCM na pia hasa ndugu zangu wa CUF. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza zaidi Waheshimiwa Wabunge wa CUF kwa sababu wameonyesha kwamba wao ni ngangali na wana kipande chao cha Pemba ambacho ni kazi kukitoa kwao.

Kwa hiyo, nawapongeza sana na naomba muendelee na msimamo huo huo na kuendelea kuchukua Majimbo mengine ya CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee tena kumpongeza Ndugu Betty Mkwaswa, kwa ushindi wake alioupata juzi. Yeye ametuletea sifa kubwa kwa Tanzania na hasa kama Mama. Watu wengi na Watanzania wanafikiri wanawake hatuwezi lakini kumbe tunaweza, mfano wake wa kwanza ni huyo Ndugu Betty Mkwaswa na sisi Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum na Wabunge wa Majimbo, tunaweza na tunaomba wazazi wa watoto wa kike wawape nafasi ili waweze kuingia katika mashindano ya kilaa ina na kugombea uongozi katika ngazi zote na vyama vyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie sasa katika hoja yenye. Naomba twende kwenye ukurasa wa nane (8) kwenye taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati kuhusu Ofisi za Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum. Haki hudaiwa na wala usingoje mtu kwamba atakupa haki yako na sisi wengine tumezoea kushindana na kudai haki zetu, kwa hiyo, ukipewa peva hivi unaona kwamba ni *short*. Kwa hiyo, naomba basi nianze hapo hapo kwangu mimi mwenyewe kwamba, ni Mbunge wa Viti Maalum kutoka *UDP* lakini niligombea Jimbo la Bukene na huyu *DED* wa Nzega ndiye aliyekuwa Msimamizi wa Uchaguzi wakati nikiwa nagombea huko. Mpaka sasa hivi nasikitika kukueleza kwamba, hajaniruhusu kuingia katika Baraza la Madiwani pale Nzega kwa sababu zake mwenyewe, naweza nikasema labda kwa chuki binafsi au pengine anataka rushwa lakini rushwa hiyo ni ya namna gani kwa mtu kama mimi, hiyo ni *short*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kupitia Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, anisaidie ili niweze kupata haki yangu, maana yake ni haki yangu mimi kuingia katika *Council* ya Nzega na hata wewe Mheshimiwa Naibu Spika unajua katika Ofisi yako kwamba, mimi natoka Nzega na unanipa tiketi ya kwenda Nzega na kurudi kila Bunge linapokwisha. Sasa kwa nini huyu bwana hataki kuniruhusu mimi niingie katika *Council* yake, kuna kitu gani ambacho hataki nikijue. Naomba nipewe haki hiyo ili niweze kuingia na nivijue anavyovificha ambavyo hataki nivijue.

Nilikuwa nafikiri labda watu wa *Opposition* Viti Maalum ndiyo hatuingii pale lakini nimezungumza na mwenzangu mmoja hapa Mbunge wa Viti Maalum, ni kwamba wote wanaingia katika *Council* zao, mmoja wao ni huyu Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Kibaha. Yeye anasema aliruhusiwa baada ya kupata barua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana. Kwa hiyo na mimi naomba basi nipewe barua hiyo na vile vile huyu bwana naomba kwa kupitia Bunge lako Tukufu, aheshimu barua hiyo. (*Makofi*)

Naomba niende sasa kwenye hoja yenye. Napenda kuzungumzia kero za *VEOs*. Kero za *VEOs* zinajulikana sana na kila mtu anazifahamu na hawa kufuatana na historia ni kwamba, walikuwa ni Makatibu wa Matawi enzi hizo katika Mfumo wa Chama Kimoja, lakini tulipoingia katika Mfumo wa Vyama Vingi hawa wamekuwa wanafanya kazi katika Serikali. Wakapewa kazi na kazi mojawapo ni kukusanya kodi na nyngine ni kwamba walikuwa wanafanya ulinzi wa amani bila mipaka.

Katika huu ulinzi wa amani bila mipaka ndio walijiona ni Miungu watu, wametesa watu wengi sana kwa sababu wenyewe ndio walikuwa Polisi wakikamata watu, wakiwalipisha watu faini, wenyewe ndio Mahakama, wenyewe ndio kila kitu. Kwa hiyo, kwa kero hizo wakiwa hawapati mshahara, mshahara wao ulikuwa ni kulipisha watu faini ya kuku, balskeli, ng'ombe na pesa hizi zilikuwa nyngi sana wakizikusanya hawazifikishi hata kwenye Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mapato waliokuwa wamezoea kupata kutokana na kodi na faini walizokuwa wanawatoza watu sasa tunapozungumza tunataka kuwaingiza katika ajira je, Serikali itawalipa kiasi gani ili waweze kuridhika kutokana na mapato waliyokuwa wanapata zamani? Maana mapato yale waliyokuwa wanapata yalikuwa hayana kodi na makubwa sana. Mfano kama *VEO* anaweza kukusanya kuku 20 kwa siku na kuku mmoja ni shilingi 2,000 maana yake anapata shilingi 40,000 kwa siku, sasa mshahara wake huyu Bwana au Bibi *VEO* utakuwa shilingi ngapi ili uweze kukidhi mahitaji yake na aache kusumbua na kuondoa kero kwa wanavijiji wetu au tunaongeza kero zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *VEO* hawa wanalipwa na Serikali Kuu na wanaajiriwa na Halmashauri ya Wilaya, sasa huyu *VEO* atakuwa *answerable* kwa nani kwa Halmashauri Kuu au Serikali Kuu? Jibu la haraka haraka atakuwa *answerable* kwa Serikali Kuu kwa sababu ndiye anayempa mshahara. Kwa misingi hiyo basi, Serikali Kuu itakuwa inakwenda mpaka chini zaidi kwa *VEO* ambapo tunakuwa na mgongano wa Serikali mbili, Serikali Kuu inaishia wapi na Serikali za Mitaa zinaanzia wapi na zinaishia wapi. Serikali Kuu ikienda mpaka kwa *VEO* sasa Serikali za Mitaa itaishia wapi inakuwa kama inaingilia kazi za Serikali za Mitaa. Naamini sasa hivi ni wakati muafaka wa kugawa madaraka ya Serikali hizi mbili, Serikali Kuu iishie kwenye Wilaya na Serikali za Mitaa ianzie kwenye Wilaya ifanye kazi zake, ipewe madaraka na mamlaka yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Madiwani ni Bunge dogo katika Halmashauri ya Wilaya. Kwa hiyo, hawa wa Serikali za Mitaa wakipewa madaraka yao kama wanavyoweza kutunga sheria, waachiwe vianzio nya mapato ya kodi wawezekupata pesa za o wapange pesa za o wanavyotaka wenyewe kufanya hivyo wanaweza kuajiri hata *DED* ataajiriwa na Halmashauri, *Treasurer* ataajiriwa na *Council* na wafanyakazi wote waajiriwe kutokana na sifa na ujuzi wao. Lakini sasa hivi ma-*DED* wanaajiriwa na Serikali Kuu hawa ma-*DED* hawawajali wala hawawathamini Madiwani. Kwa hiyo, unakuta hawamsikilizi wala hawamuheshimu Diwani ye yote pale au Baraza la Madiwani wanakuwa *answerable* kwa Serikali Kuu na wanakuwa jeuri kama huyo wa kwangu wa Nzega kwa sababu wanajua huwezi kufanya kitu chochote. Lakini kama Baraza la Madiwani liko juu pale lina madaraka ya kuwaajiri, kuwapandisha vyeo, lina madaraka hata ya kuwa-discipline na kuwfukuza watakuwa na heshima na hivyo tutakuwa na *Council* za uhakika na tutapeleka madaraka kwa wananchi.

Naomba huo mgawanyo wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ueleweke na vile vile Serikali za Mitaa zipewe vianzio nya kupata mapato ili viwe na nguvu kiuchumi na ziweze kuajiri kwa madaraka hayo na kufukuza walio jeuri na walioza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *DED* au Mweka Hazina akiiba anahamishwa kutoka Nzega anapelekwa Morogoro, anatoka Morogoro ametibua pale anakwenda Moshi kwa sababu ana *Godfather* kule kwenye Serikali Kuu. Lakini kama tukiipa madaraka *Council* kama enzi zile za zamani tunaamini kabisa hawa ma-*DED* watafanya kazi kwa uhakika na walio wabovu watafukuzwa bila kuwaonea aibu na wenyewe wataheshimu kazi kwa sababu bila kazi ndio hivyo tena walio na kazi hawataki kutoka kwenye kazi amba hawajapata kazi vile vile wanataka waingie kwenye kazi na vijana wetu wanashindwa kuingia kwa sababu kila kazi inayotangazwa ina ujuzi unaambiwa uwe na ujuzi wa miaka mitatu sasa yule aliye-fresh ataanza lini kufanya kazi ambao hajaanza kupata ujuzi hata kidogo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwenye mikopo ya wanawake na vijana. Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo inapeleka pesa kwenye Halmashauri kwa ajili ya mikopo kwa vijana na wanawake na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto vile vile inatoa pesa kupeleka kwenye *Council* lakini ile 5% kutoka kwenye *Council* kwa ajili ya vijana na 5% kwa ajili ya wanawake hakuna.

Hii ni kwa sababu hao watu ni wajeuri kama nilivyosema wanatakiwa kufuatiiliwa kwa sababu Waziri alishapitisha *circular* hapa akawaambia wakate hizo pesa 5% kwa ajili ya mfuko wa vijana na 5% kwa ajili ya wanawake lakini mpaka leo ni hadithi tu vitendo havitendeki. Kwa hiyo, naomba basi Waziri mwenye dhamana ahakikishe hizo 10% zinaingia katika mifuko husika ili vijana na wanawake wapate haki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mikopo hiyo inatakiwa kupewa watu bila kujali itikadi, lakini unakuta watu wengine wanapelekewa fomu nyumbani wajaze wala hawajui kama kuna mkopo lakini wengine wanasota mpaka kiatu kinakwisha. Kwa hiyo, naomba mikopo hiyo ipewe watu wote vijana na wanawake bila kujali itikadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ni habari nyepesi, nyepesi ni kuhusu Chama Tawala na Serikali ya CCM. Napenda kueleza kwamba ukisema Chama Tawala maana yake unataka kutumia ubabe. Mtu ye yote anayetawala hana demokrasia ni ubabe, ni nguvu, lakini ukisema kwamba ni Serikali yetu sisi wote amba tunakusanya kodi na tunalipa waajiri wa nchi hii lakini ukisema ya CCM maana yake unataka kutuambia CCM ina ubabe, haitendi haki na hiyo sio nzuri kwa wapiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. ABU T. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza kwa hotuba yake nzuri, yenyewe mwelekeo na hasa ukifikiria kuwa imelenga kuwapunguzia kero watu wa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina machache ya kuchangia kwenye hotuba ya Waziri hususan kwenye Ibara ya 16 inayozungumzia uteuzi wa viongozi ili kuboresha utawala na hususan watendaji kulipwa mshahara. Ninaamini kabisa na nia yote njema, Serikali kwa kugharamia zoezi hilo itahitaji pesa, tumefuta Kodi ya Maendeleo lakini nadhani kuna nafasi ya kuwapa Uhuru Halmashauri wasibweteke na jukumu lao la kukusanya mapato na kuwapa uwezo wa kufikiria vyanzo vingine vya mapato sio kwa wanyonge bali kwa wale wengine ambao wanaishi kwenye Majimbo haya ambao wana vipato vya juu. Nazungumzia watu ambao huingia kwa ulangazi au njia nyininge kuchota mali za Majimbo haya lakini hawachangii na kurudisha mapato haya. Mheshimiwa Waziri angeelekeza pia sehemu hiyo ili hayo mapato yasaidie iwapo Serikali kwa bahati nzuri au mbaya lengo la kufidia upungufu wa kodi halifikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwenye taratibu za Halmashauri, suala lililolalamikiwa muda mrefu ni ubadhirifu, nazungumzia Fungu la Maendeleo. Mara nydinge waamuzi kwenye Fungu la Maendeleo huenda wakachukua nafasi ya kutowashirikisha wahusika wote kwenye uamuzi nyeti hivyo kupoteza kabisa dira ya maendeleo.

Naomba taratibu zifanyike kuhakikisha uamuzi hasa kwenye matumizi ya maendeleo inashirikisha wadau wote wa uamuzi pamoa na Wabunge. Kuna muda Halmashauri zinakaa wanaamua wakijua kabisa kwa muda huo Wabunge wako Bungeni, kwa hiyo, mchango wao hautapatikana hivyo maamuzi mengine yakafanyika yakaathiri Jimbo, lakini siku za usoni zitakapokuja atakayelaumiwa ni Mbunge. Naomba Waziri aliangalie hilo pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nydinge inahusiana na taratibu za kuboresha uongozi kwenye Serikali za Mitaa hususani upande wa Wilaya. Naamini kabisa Chama cha Mapinduzi ndio Chama Tawala, ndicho kilichounda Serikali kwa hiyo, kina jukumu la kuhakikisha yale Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliahidi wananchi inatekeleza bila vikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia kwenye Kurugenzi za Tume za Uchaguzi. Wakurugenzi wengine kwenye Tume za Uchaguzi kwa mwelekeo wao wanaoujua wao wenye wenelemea kwenye Vyama vingine kiasi cha kufanya uchaguzi usiwe wenye dira kamili ya wananchi kwa sababu yeye kama kiongozi ni shinikizo kwa wale wa chini wanamfuata kwa hiyo kuharibu na kutotekeliza kabisa lengo na matarajio ya kura. Naomba Mheshimiwa Waziri uangalie suala hili kwenye uteuzi ili mtu atakayechaguliwa awe *neutral*. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ndiyo.

MHE. ABU T. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nydinge ni upande wa afya, umezungumzia taratibu za kuboresha afya kwenye Ibara ya 64 na mwanzo kabisa umemzungumzia mama na mtoto. Kero kubwa vijijini ni usafiri wakati akina mama wamefikia kwenye hatua ya kwenda kujifungua, kero ni juu ya *ambulance*. Watu wengine kama vile Madaktari, Manesi wanalahimisha wapewe fedha za kufidia mafuta, naomba utaratibu huo Mheshimiwa Waziri uangalie kwa sababu wakati ule sidhani kuwa huyu mama mjamzito kwa hali hiyo anaweza kweli kuwa na haki ya kukerwa na kitu hicho kama ni taratibu basi zifanyike baadaye. Serikali iandae taratibu kuhakikisha huduma hii inatolewa bila kero. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu jana na huko nyuma sikupata nafasi kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye Wizara ya Sheria na Katiba, naomba nichangie kwenye upande wa

mirathi. Naamini kabisa taratibu zinakuwa ngumu kwa sababu wanaohusika ni Mahakama za Mwanzo. Suala moja linaweza kuwa uwezo wa hawa Mahakimu kuhimili.

Naomba kwa sababu haki inayotakiwa ni ya yule mtu ambaye hawezi kujitetea ni maiti, marehemu na wale walibakia hawatakuwa na uwezo wa kujitetea, iundwe taasisi maalum kushughulikia suala hilo na wajuzi, Wanasheria waliohitimu sahihi wafanye kazi hiyo. Kuna kero nyininge ndogo ndogo zinaendelea huenda ni kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kitaalamu kumaliza mambo haya kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana hususan kwenye suala la Tume Huru. Nasema hivyo kwa sababu ilikuwa ni kitu ambacho Wabunge wenzangu pia wangeona ni kuwa uamuzi ni kura. Mwaka 2000 tulimchagua Rais akapata ushindi wa 72%, sauti ya Rais ni sauti ya umma atakachoamua ni uhuru tuliomba sisi. Kwa hiyo, uteuzi wa Tume ya Uchaguzi ni sauti ya Tume Huru kwa sababu ndiye tuliyempa *mandate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo juu ya hoja hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa hongera zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Mikoa na ma-RAS wote kwa kazi nzuri ya kuileta Bajeti inayoonyesha mwelekeo mzuri. Pia nawapongeza Wakuu wa Mikoa na ma-RAS kwa kweli haijawahi kutokea wao kuja kwa wingi kusikiliza hotuba hii. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Haijawahi kutokea.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Hajawahi kutokea kwa kweli. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, mimi ni mjambo wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa hiyo, mambo mengi yanayohusiana na hotuba hii niliyaona wakati tunajadili hotuba hii ya Waziri kwa hiyo nitakuwa na machache ya kuboresha hasa yale maeneo yanayohusiana zaidi na eneo ninalotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri ni ya kutia
mkubwa nataka kuelekeza katika suala
limeonveshwa katika hotuba hii ya Wazir.
moyo, mchango wangu
zima la Utawala Bora ambalo nalo

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu, nataka kuleta masikitiko kwamba daima ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inaonyesha kwamba Mikoa yetu na hasa Wilaya nyingi zinakuwa na ripoti mbaya za mapato na matumizi ya fedha za Serikali. Hii mara kwa mara inatokana na kwamba Maafisa Wahasibu hawawi makini sana au kunakuwa na njama mbalimbali za kutaka kuhujumu mapato ya Serikali na hivyo maendeleo kwa wananchi baadaye yanakuwa hafifu. Ni Mikoa michache, iliyopata Hati Safi na hata Wilaya pia nazo ni chache sitaki kuzitaja lakini nafikiri tumeshaona katika orodha ambayo tumepewaja ingawaje hivi sasa wanasema kwamba kuna matumaini kwamba hali hii inaanza kubadilika kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la utawala bora, nataka kutoa mfano wa Halmashauri yangu ya Masasi. Nakumbuka mwaka 2001, Madiwani wa Halmashauri walipitisha Azimio la kutokuwa na imani na uongozi wa juu wa utendaji wa Halmashauri. Baada ya kutokuwa na imani, tulitegemea kwamba Serikali ingechukua hatua madhubuti katika kukubaliana na Madiwani jinsi gani ya kuondoa utendaji ule mbovu. Wizara iliunda Tume kuja kuchunguza na bahati nzuri pia Mheshimiwa Waziri pale naye alikuja Masasi kuangalia hali hiyo, lakini nasikitika kuliambia Bunge lako Tukufu toka mwaka 2001 ripoti hiyo ya Tume mpaka leo bado haijawa tayari, mimi sijaiona. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea pale kwamba Madiwani wetu walifedheheshwa kwa kuonekana kama ni watu wa majungu, wameleta majungu dhidi ya watendaji jambo

ambalo sio zuri. Wakati huo huo tulikuwa tunakosa taarifa halisi ya Tume. Kwa hiyo, hali iliendelea kuwa ya ovyo ovyo mpaka sasa na siwezi kuwa na uhakika ni mambo gani zaidi yanayotendeka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini juzi wakati Waziri wa Fedha aktusimulia zaidi juu ya *Unit Trust of Tanzania (UTT)* katika maelezo yake, nilishikwa na butwaa kwa sababu alitoa mfano kwamba kuna Wilaya mbili ambazo zinafanya vibaya sana kimahesabu na hali ya ubadhirifu ni mbaya. Akazitaja Wilaya hizo kwamba ni Wilaya ya Mbulu na Masasi. Sasa wakati Waziri wa Fedha anatoa tamko hili hakuwa ameonana na mimi wala hakuwa ameonana na Madiwani wa Masasi, sasa mwenye majungu hapo ni nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri wa Fedha anasema kwamba Wilaya hizi zina ubadhilifu wa hali ya juu na ametamka juzi juzi kwenye Bunge na wakati huo huo Tume ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa wanaona kuwa Madiwani wangu wana majungu. Sio majungu jamani huu ni ushahidi tosha kuwa kuna ubadhirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaofahamu hali ile ni Madiwani wa pale, wananchi wanawaona baadhi ya hao watendaji jinsi walivyofika katika Wilaya ile na hali walionayo sasa hivi, raslimali walizozikusanya katika kipindi kifupi haya yote yanaonekana. Sasa hatuna sababu ya kuvutana sijui majungu au nini tuseme wazi kwamba jamani pale sasa hivi tuparekebishe kiutendaji ili tupanyooshe, tafadhali sana Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasubiri sana kusikia tamko la Waziri juu ya hii Halmashauri yetu kwa sababu Halmashauri ya Masasi inaongoza katika nchi hii kwa kukusanya mapato achia zile za Dar es Salaam - Manispaa ya Temeke, Ilala na Kinondoni hizo zinaongoza lakini katika Wilaya, Halmashauri ya Masasi inaongoza ilikuwa inakusanya zaidi ya bilioni moja na milioni mia tatu kwa mwaka. Halmashauri yangu hiyo hiyo ndio inaongoza kwa matumizi mabaya ya fedha, kutakuwa na maendeleo gani sehemu ya namna hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana ukifika leo Masasi barabara zile tulizokuwa tunafikiri ni barabara ni mitaro na mifereji ya kuptishia maji hakuna barabara Masasi fedha zote zinakwenda kwa baadhi ya watumishi wachache wenye nia mbaya kwa hiyo maendeleo ya dhahiri hayawezi kuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunachotaka sasa na ninachotaka kuchangia ni kwamba kuwepo na *Surgical Operation* kuokoa hali hii baada ya kubaini ubadhirifu huu ambao umeshathibitishwa na Waziri wa Fedha. Naomba zichukuliwe hatua za kiutendaji tusije kulazimishana kuanza kuondoa mashilingi bila sababu.

MBUNGE FULANI: Mashilingi?

MHE. RAYNALD A. MROPE: Sio jina lake Mashilingi, nia yangu ni kusema tusiondoe shilingi bila sababu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nataka kuzungumzia juu ya utaratibu wa Bajeti hii wa kuwa na zao moja la biashara na zao moja la chakula. Napendekeza kwa dhati kabisa kwamba zao la korosho katika Wilaya ya Masasi liwe zao kuu kwa ajili ya kupatiwa aina yoyote ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji sana Serikali isaidie hasa katika upande wa pembejeo, ununuzi wa *Biofidan, Sulfur*, Pampu zake na pembejeo nyininge. Kwa kweli korosho ndio zao pekee linaloweza kuokoa karibu Mikoa yote ya Kusini na hata kuliokoa Taifa hili kwa fedha za kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo, naomba ianzishwe sera ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na mafunzo kwa ajili ya ubanguaji wa korosho. Huko India tunasikia kwamba hawana viwanda vikubwa lakini korosho zinabanguliwa na akinamama wengi vijijini kwa mamilioni lakini kwa utaratibu maalum kwa kutumia vyombo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaomba katika hili tuanzishe utaratibu ambao utahakikisha kwamba korosho zetu nyingi tunazibangua pale pale Masasi ili tuweze kuuza korosho zilizobanguliwa. Hii ni kutekeleza sera ya Serikali kama ilivyo katika Bajeti ya mwaka 2003/2004. Naamini tukifanya hivyo basi tutakuwa tumewasaidia sana wananchi wa Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba mimi naona Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imekuwa kubwa mno jamani tenganisheni *Local Government* iwe kwenu na *Central Government* yaani ma-*DC* na ma-*RC* waende kwa Waziri Mkuu. Utaratibu huo utawasaidieni sana kiutawala. Sasa hivi jinsi mnavyochanganya mambo mengi si mnaona kuwa utawala wenyewe unakuwa mgumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu waliopo *Government* mambo yao ni hivyo hivyo *native authority* ya ki-local yashughulikiwe na Wizara moja lakini mambo yanayohusiana na utawala wa Mikoa na Ma-*DC* kwa kweli yashughulikiwe na Wizara nyingine. Zamani ilikuwa hivyo hivyo, kwa upande wa Waziri, lakini mimi nafikiri angekuwepo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anashughulikia *Local Government* na pia Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa kufanya hivi tungewenza kuwa-serve watu vizuri kuliko hii vurugu iliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo nataka kwa dhati kabisa kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ambayo ipo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake ya bajeti ambayo aliitoa Jumatatu, lakini vile vile kwa majumuisho mazuri ambayo aliyatoa jana, Jumatano, hapa Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa hotuba yake nzuri sana ya Bajeti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii niwapongeze kwanza Naibu Waziri katika Wizara hiyo, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa na wafanyakazi wote kwa kufanikisha hotuba hiyo ya bajeti. Hongera sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajielekeza kwenye maeneo machache katika hotuba hii. Hasa nikichukulia Jimbo langu la Nanyumbu. Kwa muda mrefu sasa kuna Mitaa kadhaa ambayo ipo ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu ambayo imeomba iandikishwe kuwa Vijiji, wapatiwe hati za Vijiji ili kuweza kuharakisha maendeleo yake. Katika Jimbo langu la Nanyumbu Mitaa ambayo mpaka sasa hivi imeshaprocess kwenye ngazi za chini ili kuomba kuandikishwa kuwa Vijiji ni Mitaa ya Nawaje na Mkolomwana ambayo ipo kwenye Kata ya Mikangaula. Mtaa wa Mtawatawa ambao upo kwenye Kata ya Nanyumbu, Mtaa wa Kazamoyo kwenye Kata ya Napacho, Mchenjeuka na Changwale kwenye Kata ya Lumesule. Mitaa yote hiyo kama nilivyosema imeshapitisha maombi yake kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, lakini kwa muda mrefu sasa hawajapata taarifa juu ya kukataliwa au kukubaliwa kuwa Vijiji.

Kwa hiyo, naomba Serikali ijenge tabia ya kujibu maombi ya wananchi badala ya kukaa kimya kama ilivyo hivi sasa. Kwa kukaa kimya Serikali au wananchi wanadhani kuwa Serikali haiwajali. Sasa na mimi nina imani sana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwa ni Serikali sikivu na ambayo inawajali wananchi. Kwa hiyo, naomba basi Serikali ikawajibu wananchi juu ya maombi hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kuwa mimi mwenyewe nimetembelea kwenye Mitaa hii mara kadhaa na hali nilivyoiona Mitaa hii inastahili kupewa hati ya kuwa Vijiji kamili. Wananchi wana mwamko mkubwa wa maendeleo na wanajitolea kwa wingi kabisa kuliko hata kwenye Vijiji mama vyenyewe. Miradi mbalimbali ya maendeleo inatekelezwa katika Mitaa hiyo tena kwa njia ya kujitegemea

na mafanikio ni makubwa kabisa. Kwa hiyo, kuwanyima kuandikishwa kuwa Vijiji kwa kweli ni kuwakatisha tamaa na kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mitaa hii kwanza ipo mbali na Vijiji mama na Mitaa mingine inabidi uvuke mito mikubwa, upite kwenye misitu au kwenye vichaka ambavyo vimejaa wanyama wakali. Kwa hiyo, naomba basi nichukue nafasi hii kuiomba Serikali ifikirie maombi hayo kwa haraka zaidi na ikiwezekana kuwapatia usajili wa kuwa Vijiji kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie vituo vyaya afya. Vituo vyaya afya vyote ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu vinakabiliwa na matatizo kadhaa ambayo yanaathiri utoaji wa huduma za vituo hivyo. Kituo cha afya cha Nanyumbu nina hakika Mheshimiwa Ngwilizi anakifahamu kwa sababu aliwahi kukitembelea, kinakabiliwa na tatizo la umeme. Kituo kina majengo mazuri kabisa baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa, lakini majengo yale nina hakika yatachafuka haraka sana kwa vile wagonjwa sana sana wanatumia vibatari na kandili. Kwa hiyo, naomba basi kituo hiki kifikiriwe kupatiwa ume me ili hali ile ambayo inaonekana sasa hivi iendelee kuonekana kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kituo hiki kinakabiliwa sana na tatizo la ukosefu wa gari la wagonjwa. Kwa sababu kituo hiki kiko mbali na hospitali ya Wilaya kiasi cha kilomita 80 hivi na kiko mbali na barabara kuu inayotoka Masasi kwenda Tunduru kiasi cha kilomita 30 kwa kukosa gari ya wagonjwa. Wananchi wanapata shida hasa pale wanapoambiwa wawapeleke wagonjwa wao hospitali ya Wilaya.

Kwa hiyo, usafiri ambao mara nyingi unatumika ni wa balskeli. Sasa wananchi wengi wamepoteza maisha wakati wakisafirishwa kutoka kituoni kuelekea kwenye hospitali ya Wilaya iliyopo Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Nanyumbu vile vile kinakabiliwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi. Nilipokwenda mwezi Mei, 2003 kilikuwa na wafanyakazi nane tu, nao walilalamika kuwa wanashindwa kukidhi mahitaji ya wananchi kwa sababu ya uchache wao.

Kwa hiyo, naomba vile vile suala la kukipatia kituo hiki cha Nanyumbu wafanyakazi wa kutosha likaangaliwa kwa upana wake. Kinachoshangaza ni kwamba tatizo hili kila mwaka lipo, kwa hiyo, inaonekana kuwa hakuna juhudzi zozote za kuhakikisha kuwa tatizo hili linatatuliwa. Sasa tatizo ni nini kwa sababu hatuoni matangazo ya kutafuta wafanyakazi. Kwa hiyo, naomba suala hili nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya kituo cha afya cha Nanyumbu ndiyo yapo kwenye kituo cha afya cha Michiga ya kukosa wafanyakazi, ukosefu wa umeme na ukosefu wa maji. Kwa hiyo, naomba vile vile kituo cha Michiga nacho kiangaliwe ili matatizo hayo yapatiwe ufumbuzi ili wananchi waweze kupata huduma inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha afya cha Mangaka ni kipyaa na kinaendelea kujengwa. Kituo hiki kimejengwa kwa *speed* kubwa tu na majengo mengi yamekamilika lakini bado huduma haijaanza kutolewa. Sasa mimi nilidhani kwa *speed* ambayo kituo hiki kimejengwa, wananchi wangeweza kupata huduma kwa haraka zaidi. Naomba huduma kwenye kituo cha Mangaka zianzishwe mapema zaidi, kwa hiyo, Serikali ihakikishe vifaa *vinapelekwa*, wafanyakazi wanaajiriwa ili kituo kile kianze kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye suala la kugawa Wilaya ya Masasi. Wilaya hii inachukua 53% ya Mkoa wa Mtwara na ina wakazi ambao sasa hivi wanakaribia 500,000. Kwa hiyo, 47% iliyobaki ndiyo unapata Wilaya za Newala, Tandahimba, Mtwara Vijijini na Mtwara Mjini. Sasa naomba Wilaya ya Masasi ifikiriwe nayo kuigawa katika Wilaya mbili. Jinsi Wilaya ilivyopanuka kuna maeneo kama ya Jimbo langu la Nanyumbu kwa kweli ni mbali kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hiyo, wananchi wanapata usumbufu mkubwa wanapofatilia huduma kutoka Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye barabara. Kuna barabara kadhaa ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu ambazo zimesahaulika bila kufanyiwa matengenezo kwa muda mrefu. Barabara ya Mangaka-Sengenya-Mkumbaru-Matekwe, ipo kwenye hali mbaya sana kwa kukosa matengenezo.

Barabara hii ni muhimu sana kiuchumi kwa wananchi wa maeneo hayo. Barabara nyingine ambayo imesahaulika kwa muda mrefu ni ya Chipuputa-Chimeka-Kazamoyo hadi Napacho na barabara hii ikiwa ni pamoja na daraja la Mto Lukwika.

Kwanza barabara hii ni *shortcut*, kwa hiyo, Serikali iitengeneze na kuipatia daraja kwenye Mto Lukwika ili iweze kurahisisha mawasiliano kati ya Kata ya Napacho na Kata ya Chipuputa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zingine ambazo zipo kwenye hali mbaya hivi sasa ni zile za Michigan-Nakopi-Napacho-Mpombe ikiwa ni pamoja na ujenzi wa daraja la Mto Lukwamba ambalo lilizolewa na maji msimu huu uliopita. Barabara nyingine ni ya Chitowe-Malatani-Songambele ambayo nayo inahitaji matengenezo makubwa ikiwa ni pamoja na kuimarisha madaraja yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nanyumbu-Namijati-Chilunda hadi Mbangala Mbuyuni na barabara ya kutoka Namijati-Njisa-Mitumbati - Nomalomba - Mbangala Chini, hizi nazo zinahitaji matengenezo makubwa. Barabara hiyo zamani ilikuwa ni ya ulinzi lakini sasa hivi ni muhimu kiuchumi kwa wananchi ambao wanakaa kwenye Vijiji hivyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali vile vile itengeneze barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofī*)

MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika hoja ya Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais anayeshughulika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Awali ya vote naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa umahiri wao pamoja na ofisi yake na Wakuu wa Mikoa ambao wapo hapa na Ma-RAS wao, wanafanya kazi nzuri ambayo kusema kweli sisi Wabunge tunawaunga mkono katika kazi zao wanazozifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, dhana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni ambayo inatuelekeza sasa kwenda kwa wananchi ili tuwe karibu nao katika kuwapatia madaraka na utendaji kazi. Hivyo nadhani katika utekelezaji pamoja na marekebisho yanayofanywa katika Serikali za Mitaa basi lazima kuwe na uwiano baina ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kwa sababu zote ni Serikali na ili kwenda pamoja au sambamba ni lazima upatikane ufanisi katika sehemu zote mbili. Hapa namaanisha kwamba yanayofanyika katika Serikali za Mitaa ndiyo chanzo cha kuelekea katika Serikali Kuu na yanayotokana na Serikali Kuu ndiyo chanzo cha kuelekea Vijijini katika Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, ni lazima kuna kuumana meno ambayo yote yanaelekea siyo kuumizana bali *supplement* yaani kila mmoja anamsaidia mwenzake.

Nasema haya makusudi kwa sababu kodi, kwa mfano, Kodi ya Maendeleo imefutwa katika Serikali za Mitaa. Hii haina maana kwamba basi Serikali za Mitaa ziumie kwa sababu ya kufuta kodi za maendeleo, hapana. Ni kama tulivyoambwa kwamba kutakuwa na ruzuku ambayo itakuwa imeziba pengo la zile kodi zilizoondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomaanisha ni kwamba basi kuwe na kama alivyozungumza Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kwamba hawa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wasionekane kuwa ni kioja katika utekelezaji wa mambo mbalimbali katika Halmashauri zetu hapana, wawe ni watu ambao wanahusika hasa katika maendeleo pamoja na kuzilea na kuzikuza hizi Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya tatu, ni kuhusu Mfuko wa pamoja wa Afya kwenye Ibara ya 64 mpaka 66 katika ukurasa wa 32. Mimi katika Jimbo langu kuna kituo cha afya kimoja ambapo kulikuwa lazima kuwe na vituo vya afya vitatu au vinne, lakini kuna kimoja tu katika Makao Makuu ya Jimbo.

Katika maeneo mengine yote hakuna kituo cha afya hata kimoja na suala hili nimelizungumza kweli kweli tena kwa uchungu, hatimaye ikabidi niache kuuliza maswali Bungeni wala kumwendea Waziri

mhusika. Mara ya mwisho nimemwendea Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na amenisaidia lakini bado suala hilo lipo pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *Delta* ya Mto Rufiji ikaonekana kwamba hakuna kituo cha afya kinachoweza kuwasaidia watu hawa, ikaamuliwa zahanati moja ibadilishwe iwe kituo cha afya kwa kufanyiwa marekebisho. Lakini tangu 1994 ilipoamuliwa jambo hilo mpaka leo ninavyosema kituo cha afya kile kimebakia zahanati na kinafanya kazi ya zahanati mpaka leo ambapo kuna Visiwa karibu 16 vidogo vidogo, lakini hakuna kituo cha afya. Kituo cha afya kile kimeachwa ambapo kwa muda wa miaka kumi sasa hakuna chochote kilichofanyika. Sasa ninajiuliza kwa nini jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linazungumzwa vizuri katika ukurasa wa 32 kubadilishwa ama kuimariswa vituo vya afya au kubadilishwa zahanati kuwa vituo vya afya, lakini hili kwa muda wa miaka kumi limetendeka na halijakamilika.

Naomba kwa kupitia kwako suala hili Waziri pamoja na Naibu wake walivalie njuga kwa sababu watu wa *Delta* kule wanapinduka kila siku na mitumbwi kwani ndiyo usafiri wao. Aidha, kwenda Mafia kwa Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah, hutumia majahazi au mitumbwi, kwenda Muhoro ambako ni hatari kweli kweli, kwa mama mjamzito inakuwa tabu.

Sasa kuunganisha na kituo cha afya hiki ambacho kusema kweli masuala yake anayajua vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri, nimemwendea mara nyingi ofisini kwake na hivi juzi ameniambia nimweleze mapungufu na kila kitu lakini nimeamua niyazungumze hapa ili niweze kupata nguvu zaidi. Lakini kusema kweli sehemu ile ya *Delta* njia ambayo inaweza kuunganisha kule ni njia ya kutoka Muhoro mpaka Mbweria. Njia ile imekufa tangu mwaka 1974, karibu miaka 20 imepita, Halmashauri haiwezi kutengeneza kwa sababu njia ile ina madaraja mawili. Tumeomba suala hilo lishughulikiwe lakini kusema kweli halijashughulikiwa na watu wa kule wanakufa kama ngedere. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, ninaiomba Wizara hii kusema kweli ifanye jitihada vinginevyo watu wale watabakia milele, hawaijui hii karne ya 21 na wala hawana habari nayo. Itakuja karne ya 22 hivyo hivyo mpaka ya 30, hakuna kitu.

Sasa naomba suala hili litiliwe mkazo ama ipatikane barabara hii ya kutoka Mbwela mpaka Muhoro ili iwe rahisi kupeleka wajawazito. Pia kituo kile cha afya au ile zahanati ya Mbwela igeuzwe kuwa kituo cha afya kama lengo lilivyokusudiwa hapo awali. Aliniahidi hapa Mheshimiwa KingungeNgombale-Mwiru, wakati alipokuwa Waziri, akasema wazi kwamba mimi nimeishi maeneo yale na ninakijua na kwa maana hiyo nitatekeleza kabla sijatoka katika Wizara hii. Lakini mpaka anatoka katika Wizara ile hali ipo vile vile.

Sasa nawaomba walioko sasa hivi *Brigade General* mstaafu pamoja na mwenzake wafanye juhudi kabla hawajamaliza kipindi hiki mambo yaye mazuri. Nawaomba pia washughuliki na barabara hii ya kutoka Muhoro kwenda Mbwela ambayo kusema kweli ni donda ndugu tangu yale mafuriko ya 1974 mpaka hii leo haijafunguliwa kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaki kupigiwa hata kengele ya kwanza, katika Halmashauri zetu tuna wafanyakazi waliofanya kazi kwa muda mrefu sana. Je, Wizara hii haioni vema kuwabdalisha hawa wafanyakazi kwa sababu wengine wamekaa miaka saba au miaka kumi kiasi mpaka imekuwa kama mahali pao na wanaweza kufanya wanilotaka. Jambo hili kusema kweli Wizara iliangalie ili wafanyakazi hawa wabdalishwe ili kuwe na uhai mpya katika hizi Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa sababu Wilaya ya Mafia zamani ilikuwa ni Tarafa ya Wilaya ya Rufiji, kusema kweli suala la Gati ni la muhimu sana ingawa si katika Wizara hii na hasa hasa kwa sababu kituo cha afya hakuna na barabara ya kutoka Mbwera mpaka Muhoro hakuna. Kwa hiyo, tunategemea kwenda Mafia ndiyo tupate usafiri kwenda Dar es Salaam, kwa hiyo gati pale ni muhimu kweli kweli. Naomba hili litiliwe mkazo kwa namna yoyote na naiomba Wizara iiukume Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ili gati lijengwe haraka ili litusaidie na sisi wakati huu ambapo barabara hakuna kutoka Mbwera mpaka Muhoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachoomba kwamba Mawaziri wamesikia kilio changu cha kituo cha afya na kwamba siyo naomba kwa ajili ya Mbweru tu, hata Tarafa ya Kikale nzima haina kituo cha afya. Kwa hiyo, naomba kuwe na kituo cha afya katika Tarafa ya Kikale na watu wapo tayari kuchangia na kufanya kazi ya kujitolea. Basi naomba katika Tarafa hizi mbili Mbweru na Kikale ziwe na Kituo cha Afya kwa sababu nina kituo cha afya kimoja tu, hakuna kingine chochote.

Kwa hiyo, nawaomba Mawaziri jambo hili liangaliwe na hawa wafanyakazi katika Halmashauri zetu ambao wapo kwa muda mrefu, naomba wabadilishwe na barabara hii ya kutoka Muhoro mpaka Mbweru iangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina lingine isipokuwa naunga mkono na nashukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri na wataalam katika Wizara hii kwa jinsi wanavyosughulikia Wizara iliyio kubwa sana na ambayo ina matatizo mengi na hasa matatizo yanayohusu wananchi. Katika nchi yetu ya Tanzania hakuna mahali popote ambapo wananchi hawa hawaguswi na Wizara hii kwa sababu ni Wizara ya Msingi na ni Wizara ambayo inashughulikia matatizo yao. Hivyo nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu suala la ufutaji wa kodi. Hili suala wananchi katika Jimbo langu la Kalambo wamefurahia sana na kwa taarifa yako kuna Mtendaji mmoja wa Kijiji baada ya matangazo tu Waziri wa Fedha alipotangaza kwamba kodi ya maendeleo imefutwa alikuwa hajasikia taarifa hiyo na akaendelea kukusanya kodi. Akapata kipigo kutoka kwa wananchi wakamwambia wewe husikilizi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na wananchi walivyokuwa wanakerwa na jambo hilo nchi nzima. Kwa kweli tunashukuru sana. Napenda niipongeze Wizara hii kwa kazi nzuri iliyofanya katika suala la utawala bora kwa kuanzisha Mitaa na viongozi hawa Watendaji wa Mitaa, Vijiji pamoja na Kata kwamba watalipwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Utawala Bora ni kwamba unaelekezwa uende mpaka kwa mwananchi au unakwenda karibu na wananchi, hiki ndicho kitu tunachohitaji. Naishukuru sana Serikali kwa kuweza kuwafikia wananchi mpaka kwenye ngazi ya Mtaa kwa sababu matatizo ya wananchi yataweza kusikilizwa kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nizungumzie kuhusu fedha za maendeleo zinazotolewa katika Mikoa. Suala hili nimelizungumzia mwaka 2002 kwenye Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji na mwaka 2003 nimelizungumzia tena wakati nikichangia hotuba ya Bajeti. Kwa bahati mbaya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji wala hakutaka hata kulizungumzia. Nikachukua takwimu nikampelekea Waziri Mkuu ambazo ni ukweli usiopingika. Nimekwenda *Library* kufanya uchunguzi, Mkoa wa Rukwa kwa kipindi cha miaka kumi mfululizo, umekuwa ni Mkoa wa mwisho kupewa fedha za maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu alipokuwa anajibu alijaribu kueleza kwamba inawezekana kuna fedha zilizojificha ambazo hazikutolewa, lakini kwa nini Serikali ifiche? Mzieleze waziwazi ili wananchi waweze kuelewa jambo ambalo linafanywa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa Mkoa wa Rukwa watazungumza habari ya barabara kwamba fedha zipo ni kweli na mimi nakubali ingawa hazikuonyeshwa hapa. Lakini nasema na Mikoa ile mingine ambayo inaonyesha inapewa fedha nyingi nina hakika kuna mambo mengine yaliyojificha ambayo sisi hatuyaelewi. Tunachoomba suala la Mkoa wa Rukwa kupewa fedha kidogo na Mkoa wa Kigoma kupewa fedha kidogo za maendeleo, Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Singida kupewa fedha kidogo za maendeleo

naomba Serikali suala hili ilione. Hatupendi kila siku tuwe tunakuja kusimama tunazungumzia kuhusu kutopewa fedha za maendeleo, kwa sababu na sisi ni Watanzania na tunahitaji maendeleo. Tunaomba sana suala hili Serikali isilipuuzie na tunapouliza tunaomba tuwe tunapewa majibu. (*Makofii*)

Naomba nizungumzie kuhusu upungufu wa watumishi katika Halmashauri zetu. Pamoja na takwimu nzuri ambazo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa amezitaja hapa kwamba kutakuwa na ajira ya walimu katika Wilaya zetu, tunashukuru sana. Lakini upungufu uliopo ni lazima Serikali ione ni jinsi gani ya kuweza kuupunguza ili wananchi waweze kupata watu watakaowasaidia katika kazi hizo. Kwa mfano, hao walimu na Maafisa wa Kilimo, Mkoa wa Rukwa umezungumziwa kwamba unafanya vizuri katika kilimo hasa cha mahindi. Lakini Maafisa Kilimo bado hawatoshelezi, kwa sababu vijiji vingi havina Afisa wa Kilimo, hata Kata zingine hazina Maafisa Kilimo hivyo inakuwa ni vigumu kupata ushauri wa kilimo ili waweze kulima vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, waganga katika Zahanati zetu hawatoshelezi na kila siku ni kilio na malalamiko na siyo wataalam hao tu Tarafa yangu ya Matai baada ya Hakimu aliyeuwepo kufariki Tarafa nzima haina Hakimu, Tarafa ya Kasanga haina Hakimu, ni Tarafa moja tu ya Mwimbi ndiyo ina Hakimu. Sasa haki ya wananchi kweli itatendeka. Tunaomba Ofisi yako Mheshimiwa Waziri ifanye kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba angalau wataalam wanaweza kupatikana kiasi cha kutosha.

Nataka kuzungumzia kuhusu suala la Ukimwi. Suala hili la Ukimwi ni janga kubwa la Kitaifa ambalo kwa kweli limeikumba nchi yote. Si mijini hadi vijijini wananchi wote wanalia, kwa sababu suala hili limekwishawakumba. Ninachoomba fedha hizi zilizotengwa za *TACAIDS* ziwafikie wananchi wote walioko Mijini na Vijijini. Kwa sababu tusipofanya hivyo wananchi wa vijijini ambao hawawezi wakapata taarifa vizuri kuhusu ugonjwa huu na wasipopewa madawa ya kuweza kujitibu katika ugonjwa huu basi hali itakuwa mbaya sana sana katika vijijini vyetu na hasa sisi vijiji ambavyo viko mbali kutoka sehemu ya utawala wa Serikali Kuu, tutapata matatizo sana. Tutaendelea kuzungumza lakini watu wala hawakumbuki kwamba kuna raia wapo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Elimu Msingi katika nchi hii. Wananchi wanashukuru sana jinsi Serikali ilivyoweza kuwapunguzia mzigoto kuhusu suala hili. Lakini inasikitisha kuona kwamba yaliyotokea Kamati za Elimu hazikupata kuelimishwa vizuri ni jinsi gani ziweze kufanya kazi na yametokea matatizo katika utekelezaji wa mradi huu. Tunaomba Serikali ihakikishe kwamba Kamati za Elimu zimeelimishwa kiasi cha kutosha ili waweze kusimamia vizuri hizo fedha. Kwa sababu bado zinaendelea kutolewa na zinahitaji kuendelea kusimamiwa vizuri ili zisiwe kufujwa. Naelewa Wilaya yangu ilikuwa ni moja kati ya Wilaya ambazo hazikufanya vizuri katika eneo hilo. Lakini ili waweze kuendelea kufanya vizuri ni lazima elimu itolewe na usimamizi uweze kufanywa vizuri na wananchi washirikishwe kikamilifu.

Kuhusu suala la Afya. Ninavyo Vituo vya Afya vitatu katika Jimbo langu. Kituo cha Afya cha Matai, Kituo cha Afya cha Mwimbi na Kituo cha Afya cha Ngorotwa. Umbali wa Vituo hivi vya Afya Matai ni kilomita 50, Mwimbi kilomita 65 na Ngolotwa karibu kilomita 70 kuja mjini Sumbawanga. Vituo hivi vyote vya Afya havina magari, wagonjwa hao wanafikishwa viyi katika hospitali ya Wilaya na Mkoa?

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aone ni jinsi gani watakavyosaidiwa wananchi hao. Lakini papo hapo naomba Mheshimiwa Waziri aone ni jinsi gani anavyoweza kutusaidia katika Kata ya Legezamwendo na Kalembe ambazo ziko mpakani na Zambia na ziko karibu na mpaka wa Wilaya ya Mbozi. Hizi Kata kwa sababu ziko umbali wa kilomita karibu 45 kutoka Kituo cha Afya cha Mwimbi basi na wao wapatiwe Kituo cha Afya kule kule ili wasilazimike kutembelea kilo mita karibu 45, ni wananchi waliotengwa wanapotaka huduma za afya inabidi waingie nchini Zambia na nchini Zambia kule wakiingia wanakwenda wananyanyaswa, wanaambiwa kwani Serikali yetu haitengi fedha kwa ajili ya matibabu, hivyo ni wananchi wanaonekana kabisa kwamba wamesahauliwa. Tunaomba sana waweze nao kuhudumiwa kama wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Afya mimi nasema hivi maji safi yanaweza kusaidia kuondoa karibu nusu ya magonjwa au maradhi yanayowapata wananchi vijijini. Naomba sana suala la maji

safi kwa vijiji vyetu litiliwe mkazo. Tunaishukuru sana *TASAF* imetusaidia sana katika suala hili. Lakini tunaomba Serikali nayo iendelee kutusaidia katika jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa kuzungumzia kuhusu suala la barabara. Naomba sana Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itusaidie kutengeneza barabara ya kutoka Kakozi katika Wilaya ya Mbozi kuptitia Namchika, Ilonga katika Wilaya ya Sumbawanga, Kalembe, Mwimbi, Matai hadi Kasanga, hii ni barabara ambayo ilikuwa inatumika na Wajerumani kutoka Kasanga kwenda Tukuyu. Sehemu nyingi za barabara hii ni nzuri lakini sehemu inayounganisha Wilaya ya Sumbawanga na Wilaya ya Mbozi si nzuri ikiweza kutiliwa maanani na kuweza kutengenezwa, wananchi wa Wilaya ya Sumbawanga hasa katika Jimbo langu la Kalambo wataweza kuingia katika Mkoa wa Mbeya na kufika Tunduma kwa urahisi zaidi kuliko kutumia barabara kuu inayojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza na mimi niseme naiunga hoja hii mkono toka mwanzo na nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Naibu Waziri wake kwa kuongoza Wizara kubwa kiasi hiki na kwa kweli ni Wizara ambayo ni kubwa na pana.

Nafikiri niungane na Mheshimiwa Raynald Mrope, kwamba kwa kweli kwa vyovvye vile ni vyema Wizara hii ikagawanywa. Mambo yanayohusu Mikoa yaende kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na iundwe Wizara ya Serikali za Mitaa na Maendeleo Vijijini basi halafu iwe na Waziri wake na Naibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwa hali ilivyo kwanza nawaonea sana huruma wale watu wawili, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake na kwa umakini wa Mheshimiwa Naibu Waziri anamsaidia sana Mheshimiwa Waziri wake kwa kweli anajitahidi. Lakini ni Wizara ambayo inaonekana kila Wizara iko pale, ukienda kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, anasema tutaongea na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ukienda kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, anasema tutaongea na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kila unakokwenda wanakwambia wataongea na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sasa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imekuwa ni *everything*.

Mimi nafikiri kwa kweli tuwashauri wanaohusika na kugawa Wizara, hii ni Wizara kubwa na kwa kweli haiendesheki hata kidogo na wale watu wanaumia. Kuwe na hiyo Wizara na Tawala za Mikoa iende kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu au watakavyoona wenyewe inafaa wanaogawa. Lakini hiyo nyingine iwe ni Wizara ya Serikali za Mitaa na Maendeleo Vijijini au na kitu chochote watakachotaka wao wenyewe, hapo itakuwa nafuu kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo. Nianzie alipoachia Mheshimiwa Ludovick Mwananzila. Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na mimi tunapakana katika Majimbo yetu. Barabara aliyoisema ndiyo fupi kuliko zote kwenda Sumbawanga. Pale kwenye kona alipopazungumzia mkiachana na mwenzako akaenda njia hii iliyoko sasa ambayo Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi anataka kuiwekea lami. Mkiachana na gari mwenzako anakwenda huko na wewe unakwenda katika barabara hii ambayo ameisemea Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, basi wewe uliyekwenda kwenye barabara aliyoisemea Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, utamsubiri mwenzako saa tatu unamsubiri umeishafika Sumbawanga zamani. Sasa mambo ya siasa yalipita pale na *Chiefdom* ukapita kidogo pale, ikabidi iende huko, halafu ianze kuzunguka kurudi huko. Lakini Mjerumani alishaichora zamani ilikuwa inakwenda moja kwa moja kutoka Tukuyu kwenda Abercon ambapo amepasema Mheshimiwa Ludovick Mwananzila. Sasa tumepoteza fedha za Serikali bure ni barabara ndefu na *shortcut* ipo haina mito na wala haina milima. Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, pale Tunduma ni mji mkubwa kuliko miji mingine. Kwa Sensa ya juzi Tunduma ina watu 35,000. Zahanati iliyopo ni ile ya 1966 na mtu akifa tunapeleka maiti *mortuary* ya Zambia na ni aibu sana.

Kwanza sasa hivi nchi ya Zambia uchumi wake umeshuka watu wote wanashinda Tunduma pale. Lakini akifariki mtu tunakwenda kukodisha *mortuary* ya Zambia *everytime*. Hata hivi ninavyoongea inawezekana maiti wa Tanzania wako *mortuary* ya Zambia kwa kibali, lazima upate kibali kwa ajili ya maiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo zahanati imejengwa 1966 wakati mimi nasoma sijui darasa la nane, sijui la saba, sijui la ngapi. Hili sina haja ya kulipigia kelele. Mheshimiwa Naibu Waziri mwenyewe anapita pale pale, njia ya kwenda Sumbawanga, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, anapita Tunduma. Kwa hiyo, sina haja ya kuzungumza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya maendeleo tumeiondoa na kwa kweli watu wengi hasa wapiga kura wangu baada ya kodi ya maendeleo kuondolewa wamefurahi sana na watu wote wamefurahi na simu zimepigwa kwa kila Mheshimiwa Mbunge kuonyesha kwamba watu wote wamefurahi kuondolewa kwa kodi ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kweli kabisa Halmashauri nyingi sana zilikuwa zinategemea kodi ya maendeleo kwa sababu ndiyo ilikuwa na uhakika. Sasa maadam mzigo huu tumeiondoa tunaipongeza sana Serikali. Lakini hiyo habari ya kufidia ruzuku, tunaomba sana isicheleweshwe vinginevyo Halmashauri nyingi zitasimama katika kuendesha shughuli zake haziwezi kuendelea. Tunaomba sana hilo pengo lizibwe na Serikali Kuu kama walivyotuhidi ili kusudi Halmashauri ziendelea na shughuli zake. Haya ya kwanza manne. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho hata nashindwa nilianzie wapi. Lakini nitajitahidi linahusu Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Ile Halmashauri ya Mbozi kwa sababu wewe Mheshimiwa Naibu Spika umekaa muda mrefu na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge amba tulikuwa nao toka mwaka 1995 unaelewa ugomvi na migogoro iliyokuwepo pale. Ilifika mahali ile Halmashauri ilivurugika haijapata kutokea na Waheshimiwa Wabunge wa zamani wanakumbuka hilo na hasa Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru, anakumbuka sana hilo maana alikuwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vurugu ile haijapata kutokea, tukaamua mimi na Mhesimiwa Edson Halinga, kwamba sisi hatuwezi tena kuhudhuria vikao vya Halmashauri, kwanza tulibaguliwa na Mwenyekiti yule, sasa wanafanya wao wenyewe sisi wanatuacha. Vikao nyeti wanafanya wao sisi wanatuacha, basi tukaamua na Mheshimiwa Edson Halinga, kwamba sisi kwanza tuna Bunge, ya nini kupata tatizo na tunapata chocchote kwenye Bunge kikubwa tuna tatizo gani.

Kwa nini tuumize vichwa, tunataka kwenda kusaidiana na wenzetu kuhusu masuala yanayowasumbua, wao wanafahamu kuliko sisi. Basi mimi na Mheshimiwa Edson Halinga, tukaamua kuacha. Baadaye wazee wakaingilia, wako wazee akina Davison Simbeye aliyekuwa *bodyguard* wa Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, wako wazee akina Sinkoko mnawafahamu wengi hapa wakaingilia wakatuita, katika maongezi ikaonekana kweli Mwenyekiti ana makosa mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kingunge Ngombale -Mwiru anajua. Lakini vita viliendelea, Mwenyekiti ana miaka 18 anatawala tumekaa naye. Imeingia tena vita nyininge tumegombana sasa siku ile mzee Kingunge Ngombale-Mwiru ilibidi aje mwenyewe kama Waziri amefika pale tunaongea kama kawaida wao wakasema haya, tukumbatiane jamani yamekwisha. Nikamwambia Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru, nataka nikwambie leo sikumbatii mtu mimi hapa. Wote hawa ni wanafiki hawa, tumeshakumbatiana mara nyingi, lakini tukiondoka yanaendelea yale yale, mimi sikumbatii mtu hapa. Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru yuko hapa ni shahidi. Bahati mbaya Dr. Deogratias Mwita hayupo alikuwa Naibu Waziri wa Mheshimiwa Kingunge Ngombale -Mwiru wakati huo, Halmashauri ilikuwa imeoza na ilikuwa mbaya sijapata kuona. Sasa mzee Kingunge Ngombale-Mwiru alisuluhiha tunakupongeza sana Mungu azidi kukuzidishia umri. Tumekaa vizuri sana, aah, hatujapata kuona mimi na Mzee wangu Mheshimiwa Edson Halinga, *we are real very comfortable.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kila mahali pana shetani wametuletea DT, hawa hawa akina nani. Halafu mimi pale huwa sielewi huyu wanayemuita sijui Mkurugenzi wa TUMITAA, sielewi mama Tarishi yeche ni nani na huyo mwingine wanamuita nani wa TUMITAA, aah, halafu ndiyo na

Mmari hapo mimi wala hata siwaelewi jinsi
ni matatizo tu. Lakini wametuletea.

mambo yao yalivyo. Lakini kila unayemwendea

Lakini Waheshimiwa Wabunge hapa alikotoka huyo *DT* wakatueleza, wakasema jamani msimpokee, nasema mimi ni mtoto wa *pastor*, Mungu ni shahidi, msimpokee mtapata shida. Mimi na Mheshimiwa Edson Halinga tukaenda kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake tukawambia jamani, mbona hawa wanamsema hivi na kwa kweli Mungu amewajalia *Diplomacy* hasa Mheshimiwa Naibu Waziri ana *Diplomacy* nzuri na mungu azidi kumlinda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumjaribishe haya Mzee Edson Halinga, akasema bwana mdogo, mimi nakwambia tumkatae, nikasema aah, tumjaribishe mzee, akasema haya bwana mdogo. Tumekaa kidogo tu *DT* akazua jambo, mtu ametengeneza barabara vizuri na kwa kweli kila mmoja ameridhika akalipwe huyo, *DT* akasema mpaka nikakague mimi. Tukasema hapana mbona tumegawana madaraka, si kuna yule Mhandisi wa barabara wewe *DT* ukakague namna gani, yule Mhandisi wa barabara si yupo, *DT* akasema nitakagua mimi. Mkurugenzi akasema aah mlipeni maana yake barabara tumeshaikagua, *DT* akasema aah mpaka nikakague mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *DT* akasema watu wa kabile yake ni wakubwa. Tumekaa kwenye kikao tunaongea kwa nini msimlipa mtu huyu na tumeona barabara, na bahati nzuri ni barabara inayokwenda kwangu na mnajua mimi nilivyo siwezi kukubali kitu cha ovyo. Nikamwita Simbeye msaidizi wangu tupande gari tukaiangalie barabara, pale Tunduma mpaka kule ni kama kilomita 23, tuchukue njia ya Zambia mpaka Zambia nikiwa na bendera ya CCM kufika pale mpakani mwa Zambia nikaitoa ile bendera ya CCM nikaificha. Halafu nikakimbia kule ndiyo naingia, yule *DED* amepasua barabara ya dakika 15 imepotea saa nzima na kule Zambia sipiti, nikasema Mungu wangu, huyu alipwe haraka sana, hiyo fedha hakulipwa bwana. *DT* anataka kwenda kukagua. *DT* mwenyewe hana sifa ya kuwa *DT* kwa sababu haina elimu ya kuwa *DT* bado analindwa tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *DED* ameandika *cheque* alipwe, ni mdogo wake Japhet Kamala, aliyekuwa *DAP* hapa Ofisi ya Bunge. Yule *DT* alikuwa amejifanya ni mgonjwa hata kwenye Kikao cha Kamati ya Fedha hakuja, aliposikia *cheque* imeandikwa amekuja ofisini, akawauliza wale wafanyakazi ile *cheque* iko wapi, hii hapa akaii-*cancel cheque* ya *DED*, hawa wanampenda *subordination of that sort why not wanampenda?*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaitisha kikao wewe ulikuwa mgonjwa umekujaje *ku-cancel hii cheque*, kweli kumdhalilisha *DED* kiasi hiki maana yake ni nini. Akasema sheria inasema hivi, halafu ndiyo maana tunaweka *DED* kashindwa *ku-prove*. Lakini baadaye nikamwambia wewe hustahili kuwa mtumishi na tutakufukuza kazi. Akapiga magoti nimetu, nikasema baba aliniambia mtu akitubu msamehe, nikasema jamani tumsamehe, Mheshimiwa Edson Halinga, akasema tumsamehe haya njoo ofisini, kama kuna jambo utwambie, hakutwambia. Lakini hiyo ya kwanza tukamsamehe haijapita muda mrefu wagonjwa hawana chakula, ikatoka maneno mengi mengi, Kamati yetu ya Fedha tumekwenda kukagua zimelipwa milioni moja chakula hakuna, tumekwenda tumekagua kweli, huyu anasema mimi sijapoea, lakini wao wamelipa *cheque* ambayo ni *closed*, wamesema hii ni haraka hakara mlipe, amelipwa lakini hakuna chakula. Habari hii ni ya kweli na Mungu ni shahidi. Wamemlinda wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa juzi nasikia Katibu Mkuu wa Rais sijui ameagiza kule haya mambo yachunguzwe na *DED* naye ana mambo yake haya. Nime wambia jamani kama mtoto amevunja kikombe unamwadhibu yeze aliyejunja kikombe.

Sasa kama kuna wengine huwa wanavunja vikombe tusubiri siku zao. Kama *DED* ana matatizo hatumteteti. Lakini shughulika kwanza na huyu aliye-*cancel cheque* na vile vile amenunua chakula hewa shughulika naye, wanasema ooh, kuna watu wakubwa wametoka sijui *State House*, ndiyo wanataka kwenda kukagua huko, waone madhambi ya wengine na nini. Hiyo ndiyo hali halisi ilivyo na tumeshaongea na wenzao wote hawa, mimi na Mheshimiwa Edson Halinga, tunesema kuliko kurudi kumtesa *DED* wa watu hata kama ana makosa, lakini siyo katika hili, mmekamata manyoya, kama ana makosa mgojeeni wakati wake. Lakini sasa hivi tunashughulikia huyu aliyefanya makosa yanayo julikana. Huwezi kumtetea tena kuanza kusema na huyu na huyu, aah, shughulika kwanza na huyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme mbele ya Bunge lako Tukufu, mimi na Mheshimiwa Edson Halinga hatupokei *DT* mwingine, yule hatumtaki na huyu mganga aliyepokea chakula hewa hatuwataki na kwa kweli kama *DED* yule anaondoka basi bora tuishi bila *DED*. Kwa sababu tutapata shida tena, tunakumbuka vidonda vya nyuma kule ambavyo Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, alishavitatua. Leo tena hawa wanatutumbukiza. Halafu *DT* anakwenda anamkamata *DED* anataka kumpiga ngumi, na anafuata chooni ili ampige *DED*. Halafu acae naye, watakaaje pamoja naye wakati anataka kumpiga risasi, halafu wanamlinda, *Jesus Christ* na wote hawa nimeishaongea nao. Na tumejitalidi tunawapigia simu, wengine wanaenda kwenye vikao na nini. Sasa liko hapo. Hatuna uamuza wa mwisho. Lakini kweli hatutaki Wilaya ya Mbozi iharibiwe. Tumeshachoka, tumeputa matatizo vya kutosha, tunataka kufanya kazi na maendeleo yameonekana sasa, tunayaona sisi. Sasa ambaye hayaoni, anasema analindwa sijui na vyombo gani huko huyo siyo Mtanzania halisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli naomba wenzetu watuelewa, tunawapenda wanachapa kazi vizuri. Lakini kwa nini wanakuwa na kigugumizi cha kuamua jambo limechukua muda mrefu mtu anafanya mambo yako *obvious* kila mmoja anamtetea mtu, anasema kule TUMITAA kuna mtu mkubwa, hata mimi simfahamu jina, sijui anasema nani yuko kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja hii mkono. (*Makofi*)

MHE. RAMADHANI H. KHALFAN: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba ya hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa aliyoisoma leo asubuhi. Wakati akisoma hotuba hii asubuhi alitugawia vitabu hivi viwili.

Mimi mazungumzo yangu nitajitalidi yafungamane na vitabu hivi alivyovitoa. Ingawa kwa bahati mbaya nitakapoanza inaonekana kama patakuwa naendeleza pale alipoishia mchangiaji aliymaliza sasa hivi. Nimeangalia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 4 anazungumzia mafunzo kwa viongozi. Hii mimi imenipa moyo sana nikaona kwamba kwa mwelekeo huu tutakuwa tunakwenda vizuri. Mimi nadhani tatizo kubwa ambalo liko katika Halmashauri zetu ni Watendaji wetu labda wanahitaji kusaidiwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nadhani eneo moja ambalo linatusumbua sana sasa hivi kwa jinsi nilivyoiangalia mimi tu kwa upande wangu nadhani ni upande wa Maafisa Utumishi kwenye Halmashauri ndiyo hasa wanaoleta matatizo makubwa kwenye Halmashauri na wakati wao ni kiungo kati ya Madiwani na Watendaji. Kwa nini nasema hivyo, nasema hivyo kwa sababu nadhani Afisa Utumishi ni mtaalam wa masuala ya sheria na mtaalam wa masuala ya utawala, pengine baadhi ya mambo ye ye angekuwa ni mtu wa kushauri kwamba hili lingetakiwa lifanywe hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata inapofikia mahali pa kusema labda mfanyakazi fulani achukuliwe hatua za nidhamu, ye ye ndiye angekuwa anajua taratibu za kisheria zinazowe za kuchukuliwa ili hatua za kinidhamu zichukuliwe bila kuleta bughudha baadaye lakini haifanyiki hivyo. Afisa Utumishi anapopewa nafasi hiyo atahakikisha anafanya makosa katika kumfukuza kazi mfanyakazi yule kusudi zogo lizuke, arudishwe, wanalindana kwa mtindo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mmoja nataka niutoe hapa uko Bagamoyo na uko wazi kabisa. Kuna Mheshimiwa mmoja alikuwa mtumishi kwenye upande wa Idara ya Afya, wagonjwa wanachangia fedha pale, kumbe walikuwa wanachangia ye ye, akazichukua pale milioni 1.7 tukamkamata.

Katika kumshughulikia tukaona la kufanya hakuna, kwa sababu rekodi yake ya kudokoa dokoa ni ya siku nyingi, tukasema aah, muondoeni huyo. Afisa Utumishi akatwambia sawa hakuna tatizo, tutafuata sheria zipo tutamfukuza, akafukuzwa, cha kushangaza mtu huyo aliyefukuzwa kazi, huyo huyo Afisa Utumishi alikuja kumjazia *data sheet* mfanyakazi huyo huyo aliyefukuzwa kazi akahamishwa kupelekwa Halmashauri nyingine, si maajabu makubwa haya? Mtu atahamishwaje kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine wakati kishafukuzwa kazi. Nani kamjazia *data sheet*?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika kuchunguza sana tukaambiya ana ndugu mahali fulani anamlinda. Mimi sijali ndugu yake alipo ila naangalia Afisa Utumishi pale Wilaya ya Bagamoyo huyo

ndiyo anatuvuruga sisi. Linaeleweka hili suala kwa wenzetu wa TUMITAA na tunaomba wakumbuke hiyo kesi na ziko kesi nyingi za namna hiyo ndiyo zinaleta matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapozungumzia mafunzo kwa viongozi, mimi linanipa moyo, wafundisheni kweli kazi na anzeni na upande wa Maafisa Utumishi, wawe kiungo kizuri cha Watendaji na Madiwani kwa kuwaelekeza taratibu nzuri za kiutawala. Lakini kwa bahati mbaya hali ilivyo sasa hivi kwa kweli wanatuvuruga sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 6 kuna suala la Utawala Bora limeelezwa vizuri sana, mimi nashukuru. Lakini nilivyosoma hapa, niliwahi kumwambia siku moja Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hotuba zake ni nzuri sana, kweli ukitaka kuona hotuba iliyoandikwa vizuri sana nenda Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Lakini utekelezaji ndiyo tatizo letu kwa upande wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, sijui wanahuruma sana au ni watu wema sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kusema kweli mimi nilikuwa naomba kwa haya walijotuweka kwenye hotuba yao ya Utawala Bora hatuvezi kuyaboresha zaidi ya hivyo ulivyoyaweka, lakini ukiyaweka kwenye vitendo kweli Utawala Bora utakuwepo. Wakiuacha tu kwenye vitabu hapa ndiyo itakuwa kila siku migongano hiyo ambayo inajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 8 kuna suala la vita dhidi ya rushwa. Basi tufuate walivyoelekeza hapa tutegemee haya yatatekelezwa tuweze kui-*contain* kwa namna fulani. Yameandikwa mazuri mno hapa, lakini tuyatekeleze haya, tujaribu kuona kama inaweza kutufikisha mahali kweli matatizo ya rushwa haya yakapungua kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya Serikali za Mitaa ukurasa wa 12, hapa nitataka kuzungumza kidogo. Mapato ya Serikali za Mitaa yapo ukurasa wa 12 na vilevile kwenye kitabu hiki cha majedwali iko katika ukurasa wa 11 mpaka ukurasa wa 15.

Mimi ninataka nizungumzie dogo tu. Tumefuta kodi ya maendeleo nadhani ni uamuzi mzuri sana ambaeo unaungwa mkono na kila mmoja wetu. Sasa watu wanaanza kuwa na wasi wasi hii kodi imefutwa mambo yatakuwaje, sijui nini. Ukiangalia ukurasa wa 15 wa kitabu hiki cha majedwali. Mwaka 2003 makusanyo ya Halmashauri yalikisiwa kuwa jumla ya 73,638,339,955/= . Sasa kutohana na *figure* hii au kiwango hiki cha matarajio ya makusanyo na ufutaji wa kodi makusanyo yatakaposhuka kitakachozungumzwu haraka haraka bila kufanya uchambuzi ni kufuta kodi, lakini si kweli. Kwa nini nasema si kweli.

Kwanza hii Bajeti ya shilingi 73,638,339,955/= kwa kweli ni kuwa *over ambitious*. Kwa nini nasema hivyo. Angalia Hesabu za mapato halisi ya mwaka 1999, 2000, 2001 na 2002 wastani wa makusanyo ni shilingi bilioni 48.5. Leo mwaka 2003 tunakuwa na makisio ya shilingi bilioni 73. Kwa hiyo, asilimia 52 juu ya kiwango ukishindwa utakuja kusingizia kodi, si kweli. Kodi inafutwa katika uamuzi safi kabisa wa halali kabisa wakishindwa hapo kufikia tuwe tayari kuwaeleza kwamba sio suala la kodi? Lakini walikuwa na makisio ambayo sio *realistic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hesabu za Halmashauri ukurasa wa 13. Halafu vile vile katika kitabu cha jedwali ziko kwenye ukurasa wa 58 na 62. Mimi nimefurahi sana kusikia kwamba sasa kuna mabadiliko au kuna mambo mazuri yanatokea kwenye eneo hili la hesabu za Halmashauri. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilikuwa imezungumzia eneo hili na akaeleza vizuri kwamba Hati Safi mwaka 2001 zimefikia 68 ukilinganisha na hati tatu za mwaka 2000. Ni kweli kabisa lakini ninaomba niwe mkweli inahitaji watu waelewe kuwa mchango wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliwabana sana Halmashauri na kuwarudisha kila walipoleta vitabu vichafu na mpaka ikafikia mahali kwa kweli wakaweza kufikia kufanya kazi hii nzuri. Kwa hiyo, ningiomba Kamati ya Bunge ya Hesabu ya Serikali za Mitaa, iendelete mwenendo huu wa kuwabana kusudi tupande kutocha Halmashauri 68 tufikie hiyo Halmashauri 114 kama zilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya Halmashauri yapo ukurasa wa 14 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na vile vile yako kwenye ukurasa wa 63 na 68 kwenye jedwali. Ukurasa 14 haya madeni yanatisha sana shilingi bilioni 36 kwa Halmashauri 117 nchini. Madeni hayo ni fedha ambazo watu walikatwa kwenye mishahara yao zilitakiwa zipelekwe kwenye Taasisi nyingine hazikwenda zikatumia tu. Hapo ndio utakuta kwamba kuna Halmashauri 24 tu mchango wao katika deni hili ni asilimia 70.

Sasa hili nashukuru kuona kwamba Waziri anasema Ofisi yake inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha kuangalia uwezekano wa kulipa madeni hayo kurudisha imani ya wazabuni na watumishi. Mimi naomba hilo wenzetu wa Wizara ya Fedha watakapolipata walipokee na walitekeleze kwa huruma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, TUMITAA mimi nadhani tuwaombe wajirekebishe. TUMITAA wanachangia sana kwenye matatizo tuliyonayo kwenye Halmashauri. TUMITAA hawatusaidii ndio wanaoleta vurugu hii ya kuajiri watu na kupendelea pendelea ovyo na kuwalinda. Kwa hiyo, naomba kwa kweli watusaidie kuweza kuwasaidia wenzetu wa Wizara hii wafanye kazi nzuri ambayo wamekwishaianza. (*Makofi*)

Halafu kwa sababu muda unakwenda haraka nije kwenye Mfuko wa Barabara. Mfuko huu umezungumziwa ukurasa 35 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 27 na 30 ya jedwali. Bagamoyo kwa mwaka mzima fedha za barabara zile zimezuiwa kwa sababu watendaji wa Halmashauri kwa matatizo yao wenye walihamisha fedha wamepeleka huku na huku kwa hiyo wananchi wa Bagamoyo kwa mwaka mzima hawakupata huduma ya namna yoyote ya ku tengenezewa barabara zao vijiji hata mjini.

Leo hii ukifika Mji wa Bagamoyo ni mashimo matupu kila upande. Pale inapoishia barabara ya kutoka Dar es Salaam kuingia Bagamoyo ndio umemaliza utamu wa barabara lakini kuanzia pale kama unaelekea kwenye mahoteli ya kitalii wewe mwenyewe hamu ya kwenda kwenye mahoteli utakuwa huna. Lakini cha kushangaza huyo aliyesababisha matatizo hayo mpaka leo yuko Bagamoyo na hakuna matumaini yoyote ya mtu yule kuondolewa. Juzi Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi akatueleza kuna Wahandisi *fake, bogus* wasiokuwa na sifa amewataja idadi yao watano na wako Mkoa wa Pwani wenye Wilaya sita. Nina hakika hata yule wa Bagamoyo atakuwa kundi hilo, analindwa na nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nakuja kwenye mapitio ya Bajeti ambayo yako kwenye ukurasa wa 36. Mimi sina matatizo na Bajeti. Kwa kweli nilipata bahati ya kuiptia wakati tuko kwenye Kamati na leo imerudi hapa kama kawaida yangu nimepitia mahesabu yote mimi nayaona yako sawa mazuri kwa hiyo hakuna ubishano. Mimi naiunga mkono hoja na nitapenda niwaombe wenzangu wengine tuiunge mkono kwa sababu sioni tatizo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda baada ya hayo ni aibu kugongewa kengele ya pili ningekuwa na mengi nitatafuta wakati mwingine wa kuyazungumza. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi nichangie Wizara hii. Lakini uniruhusu kidogo nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kazi zake zote anazofanya za kila siku. Bajeti yake jana tulipokuwa tunaiona wote tulisherehekeea. Kazi hiyo anayoifanya sisi sote tunasema tuko pamoja na yeze kwa sababu kila jimbo amefika kwa kipindi chote cha miaka 7 ambacho yuko madarakani. Lakini na matatizo tunamwambia. Kila anapofikia Waziri Mkuu katika zunguka yake tunamwambia matatizo. Hata Rais tunamwambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitazungumza kidogo sana tena kwa ufasaha. Nampongeza sana Waziri Mstaafu Brigidia Hassan Ngwilizi kwa kazi nzuri ya Wizara hii. Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, Wizara hii sisi tunataka tuseme ukweli wewe ndio umebaki na kazi, sisi wote humu tunaweza tukapiga maneno tu. Kwa sababu wewe umeachiwa wananchi, TAMISEMI ni dudu zito sana hili, sisi tutakulilia hapa dunia nzima sasa inasema shughuli ziko TAMISEMI. Nguvu kazi tunayoisema iko TAMISEMI. Watu tunaosema wako TAMISEMI. Wewe umebaki peke yako.

Sasa tatizo unapewa watendaji wabovu. Tukikuwekea mizania hapo ulipo na watendaji waliko ni mbali ndio tatizo lake hilo tu. Sisi hii tunapitisha na hata tungenesema fedha zote tukupitishie wewe kwa sababu ukisoma kila Idara itakayozungumza hapa itazungumza watu na watu unao wewe ndiyo maana yangu. Utazungumza barabara wanapita watu, utazungumza afya wanapita watu, utazungumza elimu wanasoma watu, sasa wewe ndiyo mwenye watu.

Tunakushukuru sana na tunakupongeza sana na Naibu wako, Katibu wako na wataalamu wako. Lakini tukubaliane kwamba tunaposema humu ndani Wabunge tumeyaona kwamba Wizara hii kwa ukubwa iliyonayo na uzuri iliyonayo na heshima iliyopewa hao wataalamu wachujwe upya. Huu mtindo uliotupa wa kuhamisha Mhandisi ameharibu Ngara anapelekwa Kilosa. Mhandisi akiharibu Kilosa anapelekwa Ngara haitatufikisha mahali popote. Hili tunalipigia kelele kila siku lakini tunasema bahati nzuri kwenye maswali tunapouliza baadhi ya majibu mnasema wataalamu hawatoshi, hivi ni kweli wataalamu Tanzania hakuna, Wahandisi wa Ujenzi hakuna, leo tunahumizwa kabisa na Wahandisi wa Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilosa pale juzi tulikuwa tunazungumza na *Road Board* ya Mkoo, nikamwuliza mbele ya Mwenyekiti wa *Road Board* Mheshimiwa Mashishanga, Mkuu wa Mkoo. Mhandisi tulikutaka daraja la Zombe kwa sababu tulikuwa tunataka kufufua kilimo cha pamba pale, akasema sina uwezo nahitaji Wahandisi wa Mkoo wafanye *drawing* pale. Mhandisi wa Mkoo aje pale kwa nini usijiuzulu, akasema naomba mtusamehe.

Basi tuktaendelea kukaa mpaka lini na mtu kama huyu. Ndio wataalamu ulionao wewe. Hakuna Mhandisi Kilosa. Sasa unapozungumza kuondoa umaskini huna Mhandisi utauondoaje. Unazungumza kuondoa umaskini wa elimu huna Afisaelimu mzuri utauondoaje na ndio watu wako hao na fedha hizi tunazotaka kuzizungumzia hapa zinakwenda kukita Wilayani, nyingi sana. Leo tunapiga kelele Bajeti iliyoletwa ile ukiwaliza Wabunge hapa nani amehudhuria vikao hivi ya Bajeti mpaka zinafika hapa Wakurugenzi wako wanatuficha. Sasa ndiyo hayo unataka tuiseme humu. Lazima tuseme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nazungumza hapa nimesifia habari ya ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuja Waziri Mkuu jimboni kwangu amekuta sina Ofisi nimekubali, ndicho mlachoamua Serikali Wabunge tusiwe na Ofisi. Haiwezekani kama Mbunge wa miaka nane sina Ofisi leo nikasema mnanifikiria, si kweli. Sasa kilichotokea siwezi kunong'ona na Waziri Mkuu maana yake nikitaka kunong'ona naye si lazima nimkaribishe mimi Ofisi kwangu asaini nimwambie na matatizo ya karibu. Nikatokea jioni amekuta Mpinzani aliyekuwa anagombea ubunge analalamikia watendaji wadogo tu ambao hawakustahili hata Waziri Mkuu aambiwe, mtendaji wa Kata. Anachukua ardhi ya watu anauza nikamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa chakula cha jioni badala ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kupumzika tunamwambia matatizo ya kiwanja kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nikamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuachie watu wa namna hii tutawakusanya tutawapiga *carpet* nyekundu, hatuwezi kukaa na watu kama hao na ndio kazi yetu hii tutakusaidia. Juzi namwuliza yule Mkurugenzi Mtendaji amefikia wapi, mimi nilitaka kumhamisha amezuiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri. Sasa hao ndio watendaji unaotaka kutupa sisi yaani yule mtu Waziri Mkuu ameagiza huyo ashughulikiwe, yeye amekaa kumhamisha Mwenyekiti wa Halmashauri amemwambia hapana huyu namtaka mimi kwa mambo yangu. (*Makofii*)

Nimekuwa nikisita sana kuja kukwambia hili lakini hapa nalisema tu kwa sababu liko ndani ya uwezo wangu lakini tunapata shida. Sisi tunapofika mahali unamwambia Mkurugenzi hili naweza likamalizika anasema naomba niacie naye yule Mkurugenzi kwa sababu historia nafahamu alikotoka alikataliwa kila maeneo. Wewe unajua alikataliwa kila maeneo, Kilosa tunataka tumwangalie na sisi tumwondoe hatujafikia kumwondoa. Lakini kama mahali hata Waziri Mkuu anaagiza yeze anajitahidi kuzuia tutafikia kumwambia aondoke. Ndio utaratibu na hatutamwondoa kwa visa tutamwondoa kwa ushahidi na kukosa nidhamu ndani ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sheria sisi hatuwezi tukawa tunakosa vikao tunakuja hapa tunazungumza hapa hata haieleweki kwa sababu vikao vyetu vimepita tu wakati hatupo, hatuitwi na vikao vingi ya maana vinakaa kipindi ambacho Wabunge wako Bungeni maana yake nini? Inasaidia nini kwenye nchi hii hilo. Wewe na mimi, Mheshimiwa Waziri sisi tunachaguliwa wote mimi na wewe

tumebakiza vipindi nya miaka miwili huyo ataendelea kuhama hama tu kama unavyomhamisha. Pengine wewe mwenzangu hutarudi na mimi sitarudi, je tumebaki? Kubaki kwetu sisi ni kufanya vizuri katika sera ya Chama cha Mapinduzi. Wewe ni Naibu Katibu Mkuu haya tumerudia haya ni wewe mwenyewe unatutuma tufanye tujadili pande zote mbili. Ukija kwenye CCM upo mkubwa wetu, huku ndani kwenye linchi kubwa kama wewe ndio mkubwa unalishikilia, sasa tukilalamika tusikilize. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuja kutuambia hatufai, tunafahamu sana wewe ukiweka mkono wako pale kwenye Chama cha Mapinduzi sirudi. Ni mtu mkubwa bwana. Sisi tunasema humu Sheria za Bunge tu na Katiba ya Bunge inayotufanya tusemeseme hivi na wewe. Wewe ni mtu mkubwa. Hatustahili tukusemeshe semeshe namna hii. Lakini tunasema yale yale uliyotutuma kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na sera zake, ndio. Tunataka tkuombe kwamba kwa kweli wataalamu wako Wilayani kule wana majibu mepesi sana, sjui wanayapata wapi. Wana majibu mepesi sjui kwa sababu hawana uwezo na zile Wilaya. Humu ndani kuna mtu wametoa majibu Mkoa wa Morogoro wamekupa wewe majibu hayo wana Ofisi tisa za Wabunge 13. Sasa mimi nikasema na Bajeti mmetupa shilingi milioni 15 sasa Ofisi hizo wewe pamoja na ziara yako ni kweli hapa njiani Gairo kuna Ofisi ya Mzee Chiduo hapa. Gairo iko Ofisi pale. Ebu sema siku moja umepita pale ukasaini kwa Mzee Aaron Chiduo, mimi kwangu, ukaenda Mbeya pale umewahi kusimama pale umewahi kukuta Ofisi. Sasa hizi Ofisi tisa sjui labda kwa Mheshimiwa Semindu Pawa. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa ndio tumesema majibu mepesi haya wanapata hizi Ofisi 9 za Wabunge. Halafu imekusababisha wewe uweke fedha ndogo kwa sababu humu wameandika Ofisi 9 maana yake wewe uweke fedha ndogo. Ofisi hewa. Sisi tulichosikia ni kwamba fedha zilikuwa zikienda inawezekana wamechora chora maneno huko kwamba zimejengwa Ofisi hizo, tunataka hili lipatikane jibu sahihi, hakuna Ofisi kule.

Mimi sina Ofisi, Mzee Aaron Chiduo, hana Ofisi, Mheshimiwa semindu Pawa hana, Mheshimiwa Alhaji Shawej Abdallah hana. Mimi sitaki kusemea sana mtasema Mheshimiwa Christopher Wegga ametaja majimbo ya wengine anayataka, lakini nasema. Niseme hata Viti Maalum tunao akinamama watatu Dr. Lucy Nky, Mheshimiwa Shamim Khan, Mama Margareth Mkanga, pale pamoja ni Mbunge wa Taifa, lakini wanatoka Morogoro hawana Ofisi. Huo ndio ukweli wenyewe. Sasa hizi Ofisi 9 ziko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza tunasikia Wabunge wenzetu kwamba kuna Wabunge wamekuwa wakitumiwa fedha hata kidogo. Mimi toka nianze sina hata *single penny* ya hela. Hizo hela kama wanantumia mimi basi kuna Wegga mwingine *copy*, mimi Wegga hapa sijawahi kupata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo tunalo jambo la upimaji pale kwa vijana wa upimaji katika eneo letu la *National Park* bado ni tatizo. Tulizungumza na Waziri wa Maliasili na Utalii akapeleka fedha Kilosa zikaliwa, lakini nimshukuru tu Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ndio maana kwenye hotuba moja nilimsifia sana hapa nilipompa hiyo taarifa aliifuatilia sana yule bwana mbadhirifu wamemfokuza kazi na sasa yuko *bench*. Huo ndio utendaji tunaoutaka. Sasa pamoja na kufukuzwa bado upimaji haupo tunaomba Mheshimiwa hawa watu wako chini yako pamoja wanatoka Wizara ya Ardhi tuainishe vizuri mipaka ya *National Park* na ardhi ya wananchi.

Nashukuru sana suala la Mikumi kupandishwa kuwa mji sasa ndio utaona tatizo lake. Mikumi imekuwa Mji, Mbunge hana Ofisi. Mimi Mheshimiwa Waziri natembelewa sana pale na watalii, watu wote wanaokwenda Kusini, ni aibu kwa kweli. Anakuja *Comrade* pale Mzee Jackson Makwetta, anataka asimame anywe maji kidogo. Mzee Eliachim Simpassa, pale anataka asimame anywe maji kidogo. Mzee wangu Yetu Mwalyego, anywe maji kidogo pale. Sasa Mbunge sina Ofisi unabaki tu hotelini unaona aibu, mwisho kama una deni unasema hapo usiingie leo ulikopa deni. Haya mambo ya ndani. Ofisi yangu inatakiwa iwe na jokofu kidogo na soda mbili, sisi ni viongozi bwana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa eneo hili nimalizie msitari kengele isinigongee nioimbe sana sana dhana hii ya kuwasahau Madiwani Serikali ifikirie sana. Sisi mtu ambaye tunamtegemea sana kufanya kazi yako kule jimboni ni Diwani. Kule jimboni mimi ni Diwani, sina mtu mwingine. Nikitoka pale

Mwenyekiti wa Kata na Katibu Kata. Lakini kwanza nitafika na Diwani niambie hali ikoje, utendaji unakwendaje, wananchi vipi. Kuhusu maendeleo wanayofanya umewahamasisha vipi. Sasa mtu anaingia unamwuliza maswali yote hayo. Wewe umekuja na shangingi umekuja na tai na kadhalika halafu unamwambia namna gani bwana, vipi watu tofali tulizosema za Serikali umeshahamasisha vipi, hela ya elimu umesimamiae, fedha za afya, vyote viko kwake Diwani. Sasa huyu mtu kama tatizo ni sheria leteni hapa. Leteni tuibadilishe.

Mimi siwezi kuwa na mdogo wangu ambaye hana kandambili, mimi nikawa na suti na kiatu safi. Huo Wabunge utakuwa ni utovu wa nidhamu. Hatuwatendei haki Madiwani wale hiyo sheria hakuna sheria nyingine nchi hii sheria hii ni ya kwetu wenyewe. Kama ni mbaya kiasi hicho basi leteni tuibadilishe. Sasa ajabu tunasema Mtendaji wa Kijiji atakuwa na mshahara, Diwani aning'inie huko huko juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema habari za ukubwa wa kuning'inia usiokuwa na maslahi hapa kwamba Serikali tatu maana yake itakuwa na Marais watatu na Rais wa Jamhuri ya Muungano atakuwa hana cheo, sasa Diwani kama ye ye ananng'inia tu, Mtendaji wa Kata ana mshahara, wa Kijiji ana mshahara, Mbunge ana mshahara ye ye yuko hewani, anachujwa huyu mtu siku ya kuchaguliwa tuwanadi wale kichama Diwani, Mbunge na Rais. Leo huyu mtu hamumkumbuki kweli. Mimi napata aibu kidogo, naona aibu nitasema nini kwa hili. Hebu tufikirie sana. Tatizo lake ni nini? Naunga hoja mkono. (*Makofi*)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu kwanza kwa kumpongeza sana Waziri wetu pamoja na Naibu Waziri bila kumsahau Katibu Mkuu Mzee Mmari, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli ingawa Wizara zote zinafanya kazi nzuri za kuwahudumia watu, lakini naamini kabisa Wizara ya TAMISEMI ndio inayogusa maisha ya kila siku ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze na ile kauli aliywahi kuitoa Baba wa Taifa katika uhai wake alitamka kwamba kama kuna jambo analolifikiri kwamba aliwakosea Watanzania ni kuzivunja Serikali za Mitaa. Baba wa Taifa ali-regret kwa hilo. Sisi sote tulikuwa tunazona Serikali za Mitaa zilivyokuwa zinakwenda baada ya kuvunjwa. Lakini chini ya uongozi wa Rais wetu tumeamua kuwapa madaraka wananchi. Kuwapa madaraka wananchi ni pamoja na kuwawezesha na kuwapa uwemo wajitawale wao wenyewe. Katika maamuzi kama haya hakuna kurudi nyuma tena. Demokrasia yoyote ni gharama.

Mimi nashangaa watu wanapozungumza kwamba *Act 174*, ile ina kasoro kwa sababu tunarudisha madaraka kwa wananchi au ni kasoro ipi hasa inayozungumzwa.

Haiwezekani, tumeamua kwamba Serikali za Mitaa zitajitawala zitajiongeza zenyewe na uzuri wake mipaka ipo. Kama kuna mtu hatambui nafasi ya Mkuu wa Wilaya, kuna mtu hatambui nafasi ya Mkuu wa Mkoo kwamba hao wanawakilisha Rais huyo atakuwa na utovu wa nidhamu na hiyo haiwezi ikawa sababu ya kuhalalisha kwamba sasa tuamue Serikali Kuu iende mpaka kule chini.

Kwanza nchi zote zilizoendelea wameachana na hali hiyo. Mimi natambua kwamba Bwana Matheo Qaresi ni Mkuu wa Mkoo, anamwakilis ha Rais na DC wangu Bwana Moshi Chang'a, ni Mkuu wa Wilaya wote hawa wanawakilisha Rais. Lakini Halmashauri imekuwa ikifanya kazi nzuri, Baraza la Madiwani limekuwa likifanya kazi nzuri pamoja na Mstahiki Meya wangu, wakiongozwa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Mbeya, wakisaidiwa kwa karibu zaidi na Mkuu wa Mkoo Bwana Matheo Qaresi na Mkuu wa Wilaya Bwana Moshi Chang'a. Sasa mimi ninapata ushirikiano wa kutosha na sijaona ni mahali gani kada ya Mkuu wa Mkoo au Mkuu wa Wilaya inaonekana kama inatetereka au inadharaulika.

Ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuwe macho kama tumeamua kuwapa wananchi ambaa ndio wenyе nchi nafasi ya kujitawala na kujiongoza basi tuwapatie madaraka hayo kwa moyo wote. Mipaka ya kazi ipo ukimwona mtu anataka aingilie kufanya kazi ya mtu mwengine basi huyo ana kasoro.

Kwa hiyo, hili nilikuwa naomba niwakumbushe usemi wa Baba wa Taifa: "tumeamua kwamba madaraka hayo wanapewa Serikali za Mitaa na ndio uamuzi ambaa ni muafaka na tunapeleka madaraka kwa wananchi, hakuna kurudi nyuma tena." (*Makofii*)

Naomba nizungumzie kwa haya yafuatayo, kwanza nizungumzie juu ya Hospitali ya Mkoa wa Mbeya. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kunikubalia mwaka 2002 kunipatia Hospitali ya Mkoa ambayo kwa kweli inahudumia wananchi wa Mbeya Mjini. Tatizo la Hospitali ya Mbeya Mjini ilikuwa ni tofauti kidogo na matatizo mengine. Hospitali ya Mkoa ilivunjwa ikapisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa. Mbeya kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2002 tuna watu karibu 270,000 na hawana mahali pengine pa kukimbilia ilikuwa ni kwenye Hospitali ya Rufaa. Lakini baada ya kupewa msaada wa Hospitali ile kwamba ianze angalau sasa hivi wananchi wamefarijika huduma sasa zinagawiwa kwa sababu Hospitali ya Rufaa haipati mzigo zaidi wa kubeba wagonjwa wanaoumwa hata mafua, umejikwaa unaenda Hospitali ya Rufaa. Hospitali ya Rufaa haikuwa ya Mbeya peke yake ilikuwa ni pamoja na Ruvuma, Iringa, Rukwa na Mbeya kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini limejitokeza tatizo kubwa sasa Hospitali ile haina wodi za kuweza kuwalaza wagonjwa. Akinamama na watoto wanapata shida kubwa sana. Sasa nabaki najiuliza ni nani mwenye wajibu wa kuzijenga hizi wodi ili watu wa Mbeya nao waanze kupata matunda ya sera safi za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nguvu zilivyo sasa hivi, wenzangu wote wa Wilayani ninapo jenga hoja kwenye *RCC* kwamba tusaidiane kujenga Hospitali ya Mkoa wanasema, sisi mwelekeo wetu ni Hospitali zetu za Wilaya ndizo tunazokazania kuziimarisha. Wazo la Mkoa limetoka na ile iliyokuwa ya Mkoa imevunjwa, nimililie nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia katika hivi vitabu, tulikuwa tumezoea kila mwaka angalau tunatenga shilingi milioni 20, lakini safari hii sikuona kama kuna fedha iliyotengwa! Basi kama inaonekana kwamba Mkoa hauwezi kuiendesha Hospitali hii, naomba ikabidhiwe Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya ili iwe ndiyo Hospitali ya Wilaya, angalau nikijipanga vizuri na Madiwani wangu tuweze kwa kujitolea kujenga *ward* ili tuokoe Wananchi hawa ambaa walitupa heshima ya kutuweka madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kingine ambacho napenda kukizungumzia ni Utawala Bora. Halmashauri nyingi hasa kubwa likiwepo Jiji la Dar es Salaam pamoja na Halmashauri yangu ya Mbeya, ili kulinda usafi wa Mji na Sheria ndogo ndogo kuna Mgambro wa Manispaa na wa Jiji, wanajitahidi kufanya kazi nzuri, lakini nafikiri lipo tatizo kidogo, watu hawa wanahitaji mafunzo ya kuzijua sheria na hasa hasa haki za binadamu. Wamekuwa wakifanya mambo ambayo ni ya ajabu sana, ambayo kama nikileta mkanda kwamba hili ndiyo tukio lililokuwa linatoka, hakuna hata mmoja atakayefurahia hali kama ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama hasa wa maeneo ya Sinde, Magege na Ilemi, wamekuwa wakinyang'anywa chakula na bahati mbaya katika hali ya njaa, chakula kile wanakimwaga chini au wanamwaga mtoni na mwenyewe nikiwa nimeshuhudia vitendo kama hivyo! Wakati mwagine nikifuatilia na kwenda kwa wenzangu nakuta Mkurugenzi hana habari, Meya hana habari, wamejichukulia jukumu la kwenda kufanya kazi hiyo.

Ukiona maisha ya namna hiyo huwezi ukaamini kwamba tuko Tanzania! Mtu ameamua kujitafutia, hata kama anafanya biashara mahali ambapo siyo penyewe, lakini sheria zetu zinasemaje? Mbebe mchukulie chakula, halafu mpeleke kwenye sehemu zinazostahili, siyo kitendo cha kutumia nguvu kupita kiasi ikiwa ni pamoja na vipigo ambavyo wanavipata! Sina sababu ya kusema uongo katika Bunge hili, nimejaribu mbinu zote kujadiliana na wenzangu, ndiyo maana namwombwa Mheshimiwa Waziri, alipatie ufumbuzi suala hili na siyo Mbeya peke yake! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo makundi ya vijana (Wamachinga) na wenyewe wanasumbuliwa sana. Wanavamiwa saa tisa usiku, meza zao wanazofanya biashara zinang'olewa zinaondolewa! Ni kweli tunahitaji kufanya Miji yetu iwe safi, lakini unapofanya Mji uwe safi ni kwa ajili ya maendeleo ya watu na ni lazima uwajali hawa watu, usipowajali watu hawa huo usafi wako utakuwa ni kwa ajili ya nani?

Ninazungumza haya, nilikuwa Meya wa muda mrefu, hatukuwa na hayo na bado Mji ulikuwa safi! Naomba tuliangalie sana suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukatai kutengeneza mazingira, lakini kama vijana wanakuwa na matatizo, tuwaambie ni mahali gani waende kufanyia biashara na wako tayari, elimu ya sisi wawakilishi itangulie kwanza kabla ya maguvu. Nchi hii imejitawala muda mrefu hatustahili kutumia nguvu bila sababu! Unapokuta makundi ya watu wanasononeka, wanalamika, wanasikitika ndani ya nchi yao, ndani ya Serikali ambayo waliiweka madarakani wao wenyewe, haipendezi hata kidogo! Ni lazima Serikali iwe na jicho la huruma katika haya. Hawa vijana ni wa kwetu sisi wenyewe, hawa Wanawake ni wa kwetu sisi wenyewe, ni lazima tuwajengee mazingira mazuri, tuwaeleze kwamba hapa hapastahili kufanya biashara ni barabarani. Unamuweka pale, akikataa basi ndiyo taratibu nyingine zichukuliwe na si maguvu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kuzungumzia suala la maslahi ya Madiwani. Diwani ni mtu mkubwa sana na ana kazi nzito sana. Yote haya tunayozungumza juu ya mradi wa MMEM kufanikiwa katika Shule za Msingi, wengi waliosimamia fedha hizi ni Madiwani. Bila usimamizi wa Madiwani kwa hakika tusingefikia haya tunayozungumza leo, lakini hawa wenzetu kidogo wamewekwa pembedi kwa upande wa maslahi. Sasa hivi kila Mbunge akitoka hapa anawasiliana Jimboni na Mheshimiwa Diwani kutaka kujuu huko kuna nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeweka kwamba kila Halmashauri ni shilingi 30,000/=, basi kuwe na nguvu fulani hivi ya Serikali kuu ku-*top-up* kiwango kile kinachotolewa na Halmashauri, kwa sababu Halmashauri zetu tunazifahamu hali zake zilivyo. Kama Serikali ita-*top-up* angalau na mwenzetu aseme ninaacha shughuli zangu hizi za shamba au za biashara ninakwenda Halmashauri kuwashughulikia wananchi. Kipindi hiki ambacho tunapeleka mabilioni ya fedha za maendeleo tunaacha zinaelea Diwani anabaki kuwa ni mtu mwenye masononeko anaona kama anamfanya mtu mwininge kazi.

Kazi ya Madiwani ni kubwa na ni nzito na wanastahili kuenziwa kwa wanaacha kazi zao kwa ajili ya kujenga Halmashauri. Ni mwaka wa pili sasa hivi tumekuwa tukilizungumza suala hili na ninaamini kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali iliyobobe katika usikivu italicifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimalizie kidogo kwenye mahusiano kati ya hizi Wizara nyingine na Baraza la Madiwani. Nimeagizwa na Madiwani wangu kwamba nilizungumze hili hasa kwenye Kamati za Shule, kwamba hakuna *coordination* ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana kwamba kwenye Kamati za Shule siku hizi baada ya kuanza kupokea hizi fedha, Madiwani wanakuwa *sidelined*, wanapelekwa nje, wao wakiwa kama wasimamizi na kama Wenyeviti wa maendeleo ndani ya Kata. Kumetokea mgogoro, Diwani anaingizwa pale anapoambiwa kuna kufyatua matofali ama kuna kuhamasisha watu, lakini akitaka kujuu kitu gani kinaendelea kwenye Kamati za Shule, wanasema unaingilia kazi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachofahamu ni kwamba, Diwani ni Mwenyezeki wa Maendeleo wa Kata, shughuli zote za maendeleo iwe ni elimu, afya na kadhalika, *overall in-charge* ni Mheshimiwa Diwani. Ni haki ya Diwani kujuu matumizi ya fedha za Shule, katika taratibu za kawaida za vikao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Madiwani hawapo kabisa wanawaambia, aaah, mnatueleza hilo, hatujui Kamati huko huko! Hawa wenyeviti wa Kamati wameanza kuwa na kiburi kidogo, wanajiona kwamba wao sasa ni *separate entity*, hawana uhusiano na Diwani ambaye ndiyo mwenye Kata, tusipoangalia *coordination* ya namna hii itatuletea shida kidogo. (*Makofi*)

Diwani anaingilia pale anapoona kuna kazi ya mitulinga/kufyatua matofali isiyokuwa na maslahi, lakini inapokuwa imekuja *cheque* ya fedha za Baba Joseph Mungai, basi anafichwa fichwa, hata kama anatembelea Shule anaonekana ni mkorofu au ni *auditor*, vitu hivi siyo vizuri, tujaribu kuvirekebisha. Diwani ni Mwenyezeki wa Maendeleo, miradi yote katika kata iko chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini siyo Sera ya TAMISEMI wala ya Serikali, bali ni wakorofu wachache ambao wanataka kupunguza hii hadhi na ngazi ya Mheshimiwa Diwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nakushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hautoshi mtu mwininge kuweza kuchangia. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

(*Saa 1.38 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa
Tarehe 27 Juni 2003 Saa Tatu Asubuhi*)

